

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Arobaini na Tisa - Tarehe 17 Agosti, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Kikao cha 49. Leo ni Ramadhani 17.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA: Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2010/2011 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maliasili na Utalii Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 435

Kuigawa Kata ya Isansa - Mbozi

MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS aliuliza:-

Kata ya Isansa iliyoko Wilaya ya Mbozi ina jumla ya Vijiji 12 na idadi ya watu takribani 38,000 hali inayosababisha upatikanaji wa huduma za jamii kwa wananchi kuwa ngumu sana:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuigawa Kata hiyo ili kupata Kata mbili ambazo zitakuwa Kata ya Isansa na Kata ya Magamba?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) aliibuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi iliwasilisha maombi ya kugawa Wilaya, Kata, Vijiji na Vitongoji katika mwaka 2009/2010. Halmashauri ilifanikiwa kupata Kata mpya sita (6), vijiji vipyta 24, pamoja na Wilaya mpya ya Mombasa na Halmashauri ya Mji wa Tunduma.

Kata mpya zilizoanzishwa baada ya kukidhi vigezo vinavyotakiwa ni Nzoka, Bara, Ipunga, Mpapa, Mkulwe na Nanyala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ilipokea maombi mengine mapya ya kuzigawa Kata za Isansa, Chiwezi na Isandula baada ya maombi hayo kupitishwa na Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi na kuridhiwa na Baraza la Madiwani.

Aidha, ili Kata hizo mpya ziweze kuanzishwa inabidi vigezo na taratibu za kugawa eneo la Halmashauri katika Kata zizingatiwe ikiwa ni pamoja na kujadiliwa na kupitishwa na vikao viliviyowekwa Kisheria ambavyo ni Kamati ya Maendeleo ya Kata, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo maombi yaliyowasilishwa yatakidhi vigezo viliviyowekwa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa -TAMISEMI itayashughulikia kwa mujibu wa Sheria zilizopo ili kutimiza azma ya kuigawa Kata ya Isansa kuwa na Kata mpya ya Magamba kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS: Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kwa kuwa tulipokuwa katika ziara katika kijiji hicho hicho cha Isansa Jimbo la Mbozi wananchi wengi walikuwa wakilalamika kuhusiana na kwamba hawapati huduma kutohana na Kata kuwa kubwa na kwamba umesema ili igawanywe lazima watimize vigezo.

Je, sasa hatuoni kwamba kunahitajika msukumo kwa watendaji wetu kufuatilia katika kutimiza vigezo vyta kugawa Kata hizo? Nashukuru.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani anachosema ni sahihi kwa maana yake wananchi wakisema wanalamika kwamba Kata ile haijagawanya maana yake unachotaka ni nini pale, unachokitafuta wewe unatafuta kwamba huduma iweze kuimariswa kwa maana ya kufanya eneo liwe dogo ili uweze kutoa huduma zaidi, kwa maana ya ku-create efficiency. Lakini *issue* hapa siyo wananchi kulalamika tu, *issue* ni vyombo vinavyohusika kuleta jambo hili rasmi kwa kupitia vikao hivi nilivyovizungumza hapa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu hana tatizo kabisa na kuanzisha Kata mpya. Lakini *the bottom line is* lazima ahakikishe kwamba Vikao vyote vinavyohusika vimefanya hivyo. Tumekuwa na utaratibu hapa unaweza ukaanzisha Kata hapa kesho yake asubuhi unapata maandamano hapa watu wanakuambia kwamba hatuitaki hiyo Kata. Imetoka wapi?

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu lazima ajiridhishe aseme kwamba hili jambo hili ikishaletwa hivyo siyo kwamba tunapokea tu tunasema sawa. Tukimaliza tunachukua tena tunarudisha na wataalam wetu wanakwenda mpaka kwenye Halmashauri hiyo inayohusika na kwenda kwenye Kata inayohusika kuangalia mipaka, kuangalia idadi ya watu, kuangalia huduma zilizoko na kadhalika.

Kwa hiyo ikifanyika yote hiyo ikiletwa hapa hakuna matatizo. Msisahau kwamba ni Kata nyingi watu wengi Tanzania nzima, Mtwara, Mwanza, Siha kule wote wanaomba hizo Kata.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru muuliza swali la msingi Mheshimiwa Raya. Lakini pia niseme kwamba ni kweli Kata ya Isansa iko jimbo la Mbozi Mashariki. Lakini pia ni kweli kwamba Kata ya Isansa na Kata ya Isandula zilishakaa kwenye Vikao vya Wodi C vikapeleka Wilayani, baadaye vikao vya RCC Mkoa na Maombi haya yalipelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Lakini katika mazingira ya kushangaza tulipofuatilia katika Ofisi ya Waziri Mkuu tuliambiwa kwamba maombi hayo hayakufika. Sasa naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri je, kama tukileta sasa rasmi maombi haya upya tena Ofisi ya Waziri Mkuu itatuhakikishia kwamba Kata hizi zinaanzishwa pale 2014 ili viweze kushiriki katika uchaguzi na wananchi waweze kupata nafuu kabisa katika huduma hizi zinazowahusu? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashukuru kwamba swali linaulizwa na Mheshimiwa Zambi kwa sababu sisi wote tulikuwepo hapa wakati tunapitisha Kata. Katika zoezi hili lillolokuwa rational hapa Tanzania la kuanzisha Kata, hakuna zoezi lillolokuwa rational kama hili lillopita. Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza akasema kwamba tulete *proposal* yote ya Kata zote ya nchi nzima, ziletwe hapa zipewe Wabunge.

Wabunge waangalie wao wenyewe na wakiridhika kwamba hizo walivyoomba ndivyo, basi irudishwe tena pale. Karibu muote kibiongo kwa sababu ya hilo jambo. Wakapitisha hapa wakasema hii imesahaulika, hii haiku, hii haipo, zoezi lile likamalizika na nyinyi Waheshimiwa Wabunge especially wale ambao walikuwako safari iliyopita miliona tulivofanya pale. Mimi nataka nijibu tu Mheshimiwa Zambi wala awe na amani moyoni mwake. Hapa *we give you what you need*. Lakini hapa tutakwenda kwa vigezo. Yeye kama kuna maombi yalishaletwa yalipita katika vikao hivyo ambavyo nimevitamka hapa haraka mwambie afanye mpango alete hapa. Sisi tukimaliza tutaweka pale. Mheshimiwa Waziri Mkuu ataangalia sasa akiona sasa wote mmekidhi vigezo hakuna tatizo. (*Makofii*)

Na. 436

Utaratibu wa Kuzuia Uvuvi Haramu

MHE. MKIWA A. KIMWANGA aliuliza:-

Nchi za jirani zinazotumia Ziwa Victoria zimefanikiwa sana kuzuia uvuvi haramu wa kutumia baruti na nyavu zilizozuiwa kwa kuwabadilisha wavuvi nyavu nzuri bila malipo na pia kuimarisha doria:-

Je, Serikali inashindwa nini kuiga utaratibu huu na kuachana na tabia ya kukamata nyavu za wavuvi na kuzichoma moto?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Kenya, Tanzania na Uganda ambazo zinasimamia uvuvi katika Ziwa Victoria zinashirkiana kwa pamoja katika menejimenti ya rasilimali za uvuvi kwenye ziwa hilo kupitia Taasisi ya Uvusi ya Ziwa Victoria (*Lake Victoria Fisheries Organization*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kuwabadilishia wavuvi nyavu nzuri anaouzungumzia Mheshimiwa Mbunge, mpango huu umetekelizwa kwa ufanisi na Serikali yetu katika Halmashauri za Ukanda wa Pwani kupitia Mradi wa MACEMP, ambapo wavuvi 874 wamenufaika na mpango huo. Mpango kama huu haujawahi kutekelezwa katika eneo la Ziwa Victoria kutohana na ukosefu wa fedha. Hata nchi za jirani za Kenya na Uganda hazijawahi kutekeleza mpango kama huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina utaratibu wa kuchoma nyavu za wavuvi kwa makusudi bila sababu yoyote. Naomba kutoa wito kwa wavuvi wafuate taratibu zilizowekwa kisheria ili kuepukana na hasara wanayoweza kupata kutohana na adhabu inayotolewa kwa mujibu wa Sheria.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba mpango huu wa kubadilisha nyavu umefanyika katika ukanda wa Pwani.

Je, Serikali sasa haioni kwamba ni wakati muafaka kutoa boti za kisasa kwa wavuvi angalau vikundi vya kuanzia kama watatu ili wavuvi hawa waweze kuvua katika maji marefu na waweze kukidhi haja za maisha yao?

Swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema hawachomi nyavu, na kwa kuwa nyavu za milimita 8 zinazuwa hadharani madukani, lakini nyavu hizi za milimita 8 inapoingia ndani ya maji inaitwa nyavu haramu.

Je, ni nyavu za milimita ngapi zinazotakiwa kutumika katika Ziwa Victoria?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, moja:-

(a) Serikali na Wizra yangu ipo tayari kushirikiana na Halmashauri husika pamoja na makundi ya wavuvi wadogo wadogo kuona jinsi ya kupata fedha ya kununulia boti hizo anazosema Mheshimiwa Mbunge ili kweli wavuvi hawa waweze kunufaika na shughuli hiyo ya uvuvi. Ila ni lazima tushirikiane kwa pamoja na fedha ndiyo itakayoamua kwamba shughuli inaweza ikafanyika lini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nyavu zilizoruhusiwa kihalali ni nyavu kwa upande wa uvuvi wa sangara ni nyavu za inchi 6. Kwa upande wa dagaa ni nyavu zenye milimita 8 hadi milimita 10. Kwa upande wa *tilapia* ni nyavu zenye inchi 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kupitia Bunge lako Tukufu nimwombe Mbunge pamoja na wavuvi wadogo wadogo wanaovua katika eneo la Ziwa Victoria wafahamu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 18 mwezi wa kwanza 2010 aliandika barua kwa Wakuu wote wa Mikoa akisisitiza kwamba ili kudhibiti uvuvi haramu ni lazima wahusika wote kwenye mkufu wa uvuvi waweze kuhusika kwamba wadhibiti na kuhakikisha kwamba nyavu haramu hazitengenezwi, hazisafirishwi na hazitatumwa na wavuvi wadogo.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa wanaovua bahari kuu ambaa hutumia *long line* ni waharibifu wakubwa sana wa mazingira na uharibifu wa vizazi vya samaki baharini.

Je, Serikali inachukua hatua gani kuwadhibiti hao kwa sababu wamesababisha hata wavuvi wadogo wadogo sasa wakose samaki kutoptera na nyavu wanazozitumia wao kule na ile teknolojia wanayotumia?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, tayari mamlaka iliyoundwa inayoitwa *Deep Sea Fishing Authority* wamekuwa wakifanya doria katika eneo hilo la maji marefu na tayari meli tatu ambazo zimeshikwa zikivua kiharamu bila ruhusa hizi zimeshikwa na kesi zipo zinaendelea. Lakini pia tutakumbuka meli na kesi ilijojulikana kwa jina maarufu la Samaki wa Magufuli kwamba pia kushikwa kwa meli hiyo ilikuwa ni sehemu ya jitihada hizo.

Kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada hizi za doria zitaendelea na kama Sera kuna mpango wa kujenga bandari ya uvuvi ili kuweza kudhibiti zaidi wale wanaokuja na kwenda kuvua na wanapovua waweze kuwa na mahala pa kupita ili wakaguliwe na kuhakikisha kwamba walichovua ni kile walichoruhusiwa.

Na. 437

Mpango wa Kuupatia Mji wa Sumbawanga Jenereta Nne

MHE. ROSWEETER F. KASIKIILA aliuliza:-

Serikali ilikuwa na mpango wa kuupatia mji wa Sumbawanga jenereta nne (4) ifikapo Mei, 2011 na baada ya jenereta hizo kupatikana mji wa Namanyere ulioko Nkasi utafaidika na umeme unaotokana na jenereta hizo:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaanza kusimika nguzo na nyaya toka mji wa Sumbawanga hadi Namanyere?
- (b) Je, Serikali inawaahidi wananchi wa Nkasi kupata umeme huo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kuupatia Mji wa Sumbawanga jenereta nne za ukubwa wa MW 1.25 kila moja ulianza mwezi Januari, 2011 na kukamilika mwezi Julai, 2011. Majoribio ya kuendesha mitambo hiyo yalianza mwanzo wa mwezi huu yalianza tarehe 3 Agosti, 2011 na majoribio hayo kwa maana ya Kamisheni imekamilika kwa mafanikio tarehe 11 Agosti, 2011. Kwa sasa majoribio yamekamilika na mitambo ipo tayari kwa kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu jana tarehe 15/8/2011 swali Na. 432 la Mheshimiwa Ally Kessy Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini mradi wa kupeleka umeme Nkasi ulianza kutekelezwa mwezi Desemba, 2010. Mradi huo unatekelezwa kwa pesa zilizotolewa na Serikali kuitilia Wakala wa Nishati Vijiji (*REA*) mkandarasi akiwa ni Kampuni ya *Rousant International* Afrika Kusini na kusimamiwa mradi huo na *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya upimaji na usanifu wa njia za umeme kukamilika, uchimbaji wa mashimo ya kuweka nguzo za nyaya za umeme pamoja na usimikaji nguzo unaendelea ambapo hadi sasa asilimia 91 nguzo zote zimeshachimbwa na nguzo asilimia 35 zimeshasimikwa.

Kwa njia hii ya kilomita 90 kutokea Sumbawanga hadi Namanyere vijiji na maeneo yatakayopata umeme ambayo yamefanyiwa tathmini ya kupatiwa umeme ni pamoja na Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi, Kanondo, Mtendo, Rezelwa, Mkundi, Kipande, Kamtawa, Milundikwa, Kasu, Chala, Kacheche, Mtatombila na Nakanazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na mkataba kati ya Mkandarasi na *TANESCO* kazi ya kujenga njia za usambazaji umeme na kuunga kwa wateja zitakamilika mwezi Desemba, 2011. Hivyo basi, kama tulivyoahidi hapa Bungeni Serikali itahimiza kwa kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mradi huu, ili wananchi wa Nkasi wapate huduma hii kwa muda huu uliopangwa. Na maeneo yatakayopata umeme ambayo yamefanyiwa tathmini ya kupatiwa umeme ni pamoja na Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi, Kanondo, Ntendo, Zezelwa, Nkundi, Kipande, Kantawa, Milundikwa, Kasu, Chala, Kacheche, Ndumtumbila na Nyakanazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na Mkataba kati ya Mkandarasi na *TANESCO*, kazi ya kujenga njia za usambazaji umeme na kuunga wateja zitakamilika mwezi Disemba 2011. Hivyo, basi kama tulivyoahidi hapa Bungeni, Serikali itahimiza kwa kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mradi kuu ili wananchi wa Nkasi wapate huduma hii kwa muda uliopangwa.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ninayo maswali mawili ya madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa umeme unatoka Sumbawanga kwenda Nkasi, na kwa hilo tunashukuru sana. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutoa umeme huo wa Jenereta kutoka Sumbawanga na kwenda Wilaya mpya ya Kalambo, yenye Makao yake Makuu Yamatai?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swalii la pili ni kwamba, Mkoa wa Rukwa ni tajiri sana kwa vile una rasilimali za aina zote zinazoweza kutuwezesha sisi kuwa na viwanda mbalimbali; lakini mkoa wa kwetu uko nyuma sana kimaendeleo. Hii ni kwa sababu, ya kutegemea hizo jenereta ambazo kwanza, haziko sehemu zote ziko Sumbawanga tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali hii siku ya CCM, Serikali makini, Serikali yenye huruma, itatuhurumia watu wa Rukwa, kutuletea umeme wa gridi ya Taifa, ili na sisi tuweze kuwa na maendeleo ya Mkoa wetu, lakini na kwa Taifa kwa jumla?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru kwa kutambua kazi nzuri iliyofanywa na Serikali. Kwa sababu, Mkoa wa Rukwa ulikuwa haupati umeme, yaani pale Sumbawanga kulikuwa hakuna umeme wa jenereta.

Umeme uliokuwa unatoka pale ulikuwa unatoka Zambia, ulikuwa unatoka Mbala, mimi mwenyewe nimekwenda mpaka Zambia kuzungummza na ZECO, nikongoza Ujumbe wa TANESCO, kujaribu kuuboresha, kwa miaka miwili hawakufanya chochote. Kwa hiyo, katika hali ile watu wa Rukwa walikuwa wanaendelea kupata tabu, hasa wa pale Sumbawanga ambaa umeme ule ulikuwa unatoka Rukwa. Umeme wenyewe ulikuwa ni wa *Mega Watt* 3 tu, kasoro kidogo na kila siku ulikuwa unakatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hayo, Serikali imepeleka majenereta manne ambayo jumla ya uzalishaji ni *Mega Watt* 5, sasa hiyo *Mega Watt* 5 kwa uzalishaji huo ndio unaweza kupeleka sasa umeme kilometa 90, kwenda mpaka Namanyere. Ndio kama alivyokuwa anafuatilia kwa karibu Mheshimiwa ali Kesi; namshukuru na yeze anafuatilia sana kwa karibu mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunasema hivi, kwa sasa hivi mradi uliokuwepo ni wa kupeleka umeme kwenye hivi vijiji kama 10 ambavyo vinapita njiani kwenye Kilometra hizi 90. Kweli kuna Wilaya hii mpya ya Kalambo, iko kwenye utaratibu wa kupelekewa umeme chini ya mfumo wa Wilaya zote mpya, kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Kwa hiyo, Kalambo ipo katika utaratibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili la kupata umeme ni kweli, mradi wa gridi ule mkubwa unaotoka Nyakanazi unazunguka huku nyuma mpaka Kigoma, lakini ni mradi unaokwenda kwa muda mrefu. Sasa mimi nadhani hizi *Mega Watt* 5 tayari hazijacheuwa bado pale Rukwa, lakini ikifika hatua kwa sababu pana uwekezaji mkubwa kweli unavyosema, tumeuona. Ukiongezeka uwekezaji ule, kama ilivyo kwa mkoa wa Kigoma ambaa unategemea jenereta, na kama ilivyo kwa Songea, kwa mikoa inayotegemea jenereta, *off grid*, kama ikionekana mahitaji ni makubwa, tutaongeza uwezo wa jenereta nyingine. (*Makof!*)

MHE. PUDENSIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri. Je, Serikali ina mpango gani pia wa kupeleka umeme katika Kata za Ilunde, Nsekwa, Ilela, Ikola, Karema, Mamba na Majimoto?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, unaweza ukafafanua hizo Kata ziko kwenye Wilaya gani?

MHE. PUDENSIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hizo ziko katika Wilaya ya Mpanda, Mkoa mpya wa Katavi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nadhani tukubaliane na Mheshimiwa Kikwembe, kwamba tatizo la Mpanda, kwanza ni kupatikana umeme wenyewe. Kwa sababu, umeme unaopatikana Mpanda sasa hivi haupo *reliable*, yale majenereta yanaingia na kutoka kila siku na sasa hivi tuna tatizo nadhani la *transformer* ambazo zinatoka *TANELEC* zinapekwa Mpanda kwa dharura ili umeme upate kuzalishwa kwa *stability* nzuri zaidi kidogo kuliko sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Kata alizozitaja ni nyingi na kwa kawaida siwezi kujibu kusema tutapeleka Kata zote hizo bila kuwaliza *TANESCO* kama wamezifanyia tathmini na kujua zitafanyiwa kuunganishwa umeme kwa kiwango gani na kwa muda gani.

Kwa hiyo, ninaomba nizipokee hizo Kata, nitawapa *TANESCO*, lakini nadhani tukubaliane tu kwamba jambo kubwa la msingi kwa Mpanda ni kuhakikisha kwamba, panapatikana umeme wa uhakika zaidi kuliko unavyopatikana sasa hivi. (*Makofii*)

Na. 438

Kupeleka Umeme Kwenye Vijiji vya Masasi

MHE. JEROME D. BWANAUSI K.n.y. MHE. MARIAM REUBEN KASEMBE aliuliza:-

Mji wa Masasi utakuwa na umeme wa uhakika wa *Mnazi Bay*:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika vijiji vya Mbonde, Nmkungwi, Chingulungulu, Namalembo, Mwenge, Songambele, Sululu, Lisekese, Nangose, Marokoopaleni, Nanyindwa, Lilala, Chiwale, pamoja na Chikunja, ambao tayari wameshapeleka maombi yao tangu miaka mitatu iliyopita?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya kupatiwa huduma ya umeme kwenye maeneo aliyyotaja Mheshimiwa Mbunge, yaliyopokelewa kwenye Ofisi za *TANESCO* wilayani Masasi mwaka 2008, wakati *TANESCO* inajienda kukabidhi shughuli za kusambaza umeme kwa kampuni ya *Umoja Light*, ambayo ni kampuni tanzu ya *Artumas* ambayo ilikuwa na jukumu la kusambaza umeme katika Mikoa ya Mtwara na Lindi, badala ya *TANESCO*. Hata hivyo, kampuni ya *Umoja Light Ltd*, ilishindwa kufanya kazi hiyo kutokana na kukosa mtaji wa kuendesha shughuli hizo kulikosababishwa na m dororo wa kifedha na kiuchumi duniani kwa wakati huo. Kazi hiyo sasa tumekubaliaa ifanywe ma na *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kwa sasa tumekubaliana kwamba, Ofisi za *TANESCO* zisifungwe wilayani Masasi, maana wakati huo ziliikuwa zinaanza kufungwa, tathmini inafanywa upya kujua gharama halisi za utekelezaji wa miradi ya umeme, yaani kupeleka umeme kwenye vijiji kama 8 alivyovitaja Mheshimiwa Kasembe, kujua gharama halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo na kuweza kuomba fedha hizo kwenye bajeti ya *TANESCO* ya mwaka 2012. Zoezi la tathmini ya gharama za ujenzi wa miradhi ya umeme katika vijiji hivi, linatarajiwa kuanza mwezi Machi, 2012 na kukamilika mwezi Aprili, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nishati na Madini aliyoifanya kwenye maeneo ya mradi huu Januari, 2011, masuala ya usambazaji wa umeme kwenye vijiji hivi, na masula mengine husika yalijitokeza. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba,

Serikali inayatafutia ufumbuzi wa haraka matatizo haya ili kuwapatia umeme kwa ufanisi wakazi wa Lindi na Mtwara, unaotokana na mradi huu.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa wa Mtwara na Lindi kwa sasa ndio mikoa pekee ambayo imekuwa na uhakika wa umeme kutoptanaji wa gesi kule *Mnazi Bay*. Lakini tatizo kubwa liliopo sasa ni uchakavu wa miundombinu iliyopo, hasa nguzo. Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza kuwahakikishia wananchi wa maeneo haya uhakika wa kupata nguzo nyingine ili umeme ule wa uhakika uweze kuwafikia wananchi vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, aliyahi kuliahidi Bunge hili kwamba, katika vijiji vya Nanjota, Ruatala na Mchauru pamoja na Mnavila, vingeweza kupatiwa umeme katika kipindi hiki cha mwaka 2011/2012 na pia kuvipatia *transformer* vijiji vya Mbuyuni, Mkangaula, pamoja na vijiji vingine ambavyo vinapitiwa na umeme hivi sasa, ikiwa ni pamoja na Chidya.

Je, ahadi ile bado ni ya kweli? Kwa sababu, miezi mitatu ambayo Mheshimiwa Waziri aliitoa, ili *TANESCO* waweze kwenda kufanya tathmini ya kujua garama, haijafanyika hadi sasa.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Bwanausi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba, mradi huu unakabiliwa na tatizo la nguzo, hasa kwenye kile kipande cha *line* kinachotoka Newala kwenda mpaka Masasi. Hivi vipande vingine huku kwenye *Northern Feeder* huku Ndanda na Nyangao, ubadilishaji wa nguzo ulishafanyika. Kwa hiyo, tatizo kusema kweli liko kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tatizo labsda niseme wakati wa Ziara, tatizo liliojitokeza ni kwamba, kuna *vi-circuit breaker* pale ambavyo vilikuwa vinaonesha kwamba, ikitoka nguzo moja, *system* nzima inatoka. Kwa hiyo, palikuwa na matatizo ya kiufundi ambayo wakati tumefanya ziara na watu wa *TANESCO* tumewaomba kwamba, kazi hii ya kuboresha ubadilishaji wa nguzo ambao wakati huo ulikuwa ufanywe na *Umoja Light*, sasa unafanywa na *TANESCO*, ufanywe lakini pia uzingatilie ufanisi; kwa mfano nguzo ikitoka isiwe tena *system* nzima imetoka. Kwa hiyo, ni kweli kwamba, pana taizo kubwa la miundombinu la uchakavu, limefanyiwa kazi wakati huo palikuwa na guzo kama 480 ambazo zinahitaji kubadilishwa. Naamini tunakwenda tunazibadilisha polepole kwa sababu nguzo 480 ni nyangi, lakini tumedhamiria kwamba, kwa kipindi kifupi kijacho kazi hii imalizike.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la Nanjota, Nalietarwa, na hivi vijiji vingine, pale pana vijiji vya aina mbili; kuna vijiji ambavyo ile *transmission line* yenye inapita juu yake. Tulishakubaliana kwamba, vijiji vyote vinavyopitwa na *line* hizi ikiwa kwenye *line* ya Kaskazini au *line* ya Kusini, vipatiwe umemem baada ya kufanya tathmini ya kujua umeme ule utatumika na watu wangapi na kama unakidhi vigezo; kwa hiyo, pana vijiji vingivingi pale, baada ya ile pesa ya *ORET* kukosekana, vimekwama kidogo, lakini Serikali imeji-commit, alisema Waziri miezi mitatu lakini imeonekana kwamba, pana matatizo ya kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba, mimi mwenyewe ndiye niliyekuwa nafuatilia mradi huu. Kwa hiyo ninaufahamu vizuri sana. Ninajua kwamba, pesa zikipatikana tutakwenda kwa awamu ili kukamilisha vijiji vyote vilivyo katika awamu hii mpaka Nachingwea na kule Ruangwa. (*Makof!*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, mahitaji ya umeme ni ya nchi nzima. Kwa kuwa, Serikali imeshaahidi mara nyangi kupelekwa umeme tarafa ya Sepuka, kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mohammed Missanga. Na kwa kuwa, juhudhi za Mbunge, zimefanyika sana lakini bado mpaka sasa hivi hakuna utekelezaji wowote unaonekana. Je,

Serikali, itasema nini katika kupeleka umeme katika Tarafa ya Sepuka, ili Mbunge, apungukiwe maswali kwa wapiga kura wake?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli. Pale kwa Mheshimiwa Mohammed Missanga, palikuwa pana miradi miwili mikubwa, mmoja ulikuwa kwenda Ihanja na mmoja ulikuwa kwenda Sepuka. Ule wa Ihanja, kama kilometra 13, umeshakamilika na wananchi tangu mwaka jana wanapata umeme Ihanja. Huu wa Sepuka una kama kilometra 23 hivi. Kwa sasa hivi pana Hospitali imejengwa pale katikati imefikiwa umeme. Kwa hiyo, pana kazi iliyobaki kama ya kilometra 15 tumekubaliana na Mheshimiwa Missanga, kwamba tutaenda kuiangalia lakini pia kuzungumza na wananchi ili wapate kujua kwamba, Serikali imedhamiria kutekeleza mradi huu haraka iwezekanavyo.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Zaidi ya *Mega Watt 400* zinapatikana katika Mikoa wa Lindi na Mtwara. Lakini pamoja na hivyo Mikoa ya Lindi na Mtwara, haipo katika katika gridi ya taifa.

Je, Serikali ina mpango gani katika kutoa mrahaba kutokana na mauzo ya gesi hiyo katika mikoa hiyo ya Lindi na Mtwara?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Barwany, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba niseme tu kwamba, ni kweli hili jambo la mrahaba au mapato yanayotokana na gesi, kwa kujalibu kuliangania na utaratibu unaofanya kwenye madini ni jambo ambalo mimi nimeingia kwenye Wizara hii miaka 4 iliyopita na nimelikuta lipo. Ni jambo ambalo kusema kweli ni jambo kubwa na wananchi wenyewe wanalitaka, lakini kwa sababu halijaingia kwenye Sheria ile ya kwanza ya uzalishaji, *Petroleum Act*. ya mwaka 1980 na *Petroleum Act*. ya mwaka 2008, tunachosema ni kwamba tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, wa maeneo ambayo gesi inatoka waendelee, tuendelee kukutana na Wizara yangu na Serikali kwa ujumla ili tuone utaratibu huu tutafanyaje ili pawe na mapato maalum yanayotokana na gesi kama ilivyokuwa kwenye madini kwenda kwa Wilaya hizi ambazo ni Kilwa na Mtwara kule kwa Mheshimiwa Hawa Ghasia, na kadhalika, ili nao wapate kufaidika na rasilimali ambayo inatokana na Jimbo lao. Kwa hiyo, jambo lake linalelewaka na ninaomba tulifanyie kazi kwa pamoja ili lipate utekelezaji na linasikika.

Na. 439

Barabara za Kigomba Kupandishwa Hadhi

MHE. FELIX F. MKOSAMALI K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO aliuliza:-

Mwezi Disemba 2010, Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Kigoma, ilipitisha barabara za kupandishwa hadhi kutoka ngazi mbalimbali:-

Je, ni lini Serikali itatangaza uamuzi wa kupandishwa barabara za Pasua – Mhembe – Kalinzi, Mwandiga – Bubango – Mkongoro na Kagunga – Kigoma, ikizingatiwa kuwa zimekidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Barabara Mkoa wa Kigoma, kupitia barua yenyewe Kumb. Na. CE. 61/230/01 ya tarehe 23/07/2010, iliwasilisha maombi Wizara ya Ujenzi kuhusu kupandishwa

madaraja barabara 42 katika ngazi mbalimbali. Aidha, barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, ambazo ni Pasua – Mahembe – Kalinzi, Mwandinga – Bubango – Mkongoro na Kagunga – Kigoma, haziko kwenye orodha ya barabara zilizopendekezwa na Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Kigoma na kuwasilisha Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Barabara Na.13 ya Mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009 imeweka utaratibu wa kuziweka kwenye madaraja stahili barabara zote nchini. Namshauri Mheshimiwa Mbunge, afuate utaratibu uliopo kwenye sheria ikiwa ni pamoja na kupitisha maombi kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa (*Regional Road Board*).

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. kwa kuwa, barabara hizi ni muhimu sana kwa uchumi wa vijiji hivi na Kata hizi na Mkoa mzima wa Kigoma. Je, Serikali iko tayari kuangalia na kufuatilia ni kwa nini barabara hii haiko kwenye orodha na wakati ni muhimu sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili. Kwa kuwa, barabara nyngi za Mkoa wa Kigoma, zimepandishwa hadhi. Je, Serikali iko tayari kutenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa lami kwenye barabara hizi? Ikwemo barabara ya kutoka Kibondo kwenda Mabamba mpaka kufika Burundi? Kwa sababu ni muhimu sana kwa uchumi wa Kigoma.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Felix Mkosamali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine Mheshimiwa Mbunge, hakunisikia vizuri kwenye jibu langu la msingi kwamba, barabara alizokuwa amezitaja Mheshimiwa Zitto, katika swalı lake, haziko kwenye orodha hiyo ya barabara 42 ambayo tumeipata. Ndio maana sina kawaida ya kutembea na mafalli ya Ofisi, lakini leo nimekuja na faili kabisa linalohusiana na hizo barabara. Kuna barabara kutoka Kigoma, ipo hapa ina barabara 42, lakini hakuna hizo barabara alizozitaja Mheshimiwa Zitto. Ninachosema tu ni kwamba, kama Mheshimiwa Zitto, anaona hizo barabara zinastahili kupandishwa, afuate tu utaratibu apeleke kupitia Bodi ya Barabara ya Mkoa, tutaziangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, na swalı lake la pili linatokana pia na *assumption* kwenye swalı la kwanza kwamba, barabara hizo 42 zimepandishwa hadhi! Bado hazijapandishwa hadhi; bado ziko kwenye mchakato na sikishamalizika huo mchakato, tutakutaarifu Mheshimiwa Mbunge. (*Makofî*)

MHE. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Suala hilo la Kigoma linafanana kabisa na suala la barabara inayotoka Kalenga, kwenda Kiponsero – Wasa mpaka Lugoda, katika Jimbo la Kalenga. Katika kikao cha RCC, ombi la kuipandisha barabara hii katika hadhi ya Mkoa, lilipitishwa na kuwasilishwa Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua kama barabara hii nayo iko katika kukubalika ili nasisi tuweze kunufaika na upandishwaji wa hadhi ya barabara hii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi ningependa kujibu swalı la nyongeza la Mheshimiwa Mgimwa kama ifuatavyo. Ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mgimwa, kwamba barabara ya Kalenga tumepokea maombi yake ya kupandishwa daraja.

Lakini vile vile niombe nimtaadharishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa zoezi hili tumelisitisha kwa muda kwa sababu tunapandisha barabara nyngi madaraja bila kuongeza mfuko wa pesa wa kuweza kuzihudumia. Kwa hiyo, asitegemee kwamba baada ya muda si mrefu pengine hiyo barabara tutakuwa tumeshaichukua, mchakato unaenda polepole kufuatana na pesa ambayo tuliyonayo ya kuweza kuzihudumia hizo barabara.

Vigezo Vinavyotumika Katika Kumpata Mshauri Ufundii Katika Ujenzi

MHE. HAROUB MOHAMMEDI SHAMIS aliuliza:-

Katika miradi mikubwa kama ya ujenzi wa barabara Serikali, huweka mshauri kiufundi (*Consultant Engineer*); lakini baadhi ya miradi imeshuhudiwa ikiwa hafifu mara tu baada ya kukabidhiwa:-

- (a) Je, ni vigezo gani vinavyotumika kumpata Mshauri huyo na Ufundii?
- (b) Je, ni kwa nini baadhi ya miradi inaharibika mara baada ya kukabidhiwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, nappenda kujibu swali la Mheshimiwa haroub Mohammed Shamis, Mbunge wa Chonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ujenzi wa miradi ya barabara inahitaji maandalizi yanayohusisha upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na tathmini ya athari kwa mazingira na kijamii. Aidha, wakati wa ujenzi unahitajika usimamizi thabitili kukidhi ubora kulingana na usanifu wa viwango vilivyoko kwenye mkataba. Ili kuongeza ufanisi na uwazi katika kutekeleza kazi hizo, mara nyingi Serikali huweka Wahandisi Washauri wa kufanya usanifu na kusimamia kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vinavyotumika kumpata Mhandisi Mshauri, ni pamoja na:-
 - (i) Uzoefu wa Kampuni ya ushauri kwa kulinganisha na mradi husika.
 - (ii) Uzoefu na kiwango cha elimu kwa wataalamu wanachitajika kwa kufanya kazi husika (*Consultancy Services*).
 - (iii) Gharama iliyopendekezwa na Mshauri kwa ajili ya kufanya kazi husika (*Consultancy Fees*).
- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, barabara inaweza kuharibika mapema baada ya ujenzi kutokana na Mkandarasi kujenga barabara chini ya ubora katika viwango vilivowekwa na Mhandisi Mshauri, kukosa umakini katika kusimamia na kudhibiti ubora wa kazi wakati wa ujenzi. Aidha, usanifu (*Design*) hafifu wa barabara husika nayo inaweza kuwa sababu.

MHE. HAROUB MOHAMMEDI SHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana ninayo maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Bidhaa zisizo na viwango kama bidhaa za *electronic* za umeme uchomwa moto au hupondwa pondwa kwa burudoza au tinga tinga. Je, barabara zisizo na viwango hufanywa nini?(b)Hivi karibuni tumeshuhudiwa Serikali kupitia Waziri wake wa Ujenzi Dkt. John Pombe Magufuli, akiikataa barabara iliyojengwa kutoka Mivinjeni mpaka Mbagala kwa sababu ya kwamba haina viwango.

Je, ni nini kauli ya Serikali na hatma ya barabara hii?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shamis kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu Mheshimiwa Mbunge atambue kwamba kwa kweli Wizara ya Ujenzi tumekuwa wakali sana kwa barabara zinazoharibika mapema, siyo kwa maneno tu bali hata vilevile kwa vitendo kama vile ambavyo bidhaa duni zinavyotupwa kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Nimtolee mifano michache tu, barabara ya Nangulukuru, Mpwenkuru, kwa wale wanaoifahamu hiyo barabara sasa hivi hiyo barabara inafanyiwa marekebisho na mkandarasi kwa gharama zake mwenyewe kwa sababu udhaifu wa hiyo barabara aliufanya yeze mwenyewe, barabara ya Kilwa ambayo ameiongelea Mheshimiwa Mbunge, hiyo barabara Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Dkt. Pombe Magufuli alikataa kuipokea hiyo barabara na sasa hivi mkandarasi, mhandisi mshauri pamoja na wataalam wetu wa TANROADS wapo katika kufanya uchambuzi na uhakiki na uchunguzi ni nini kiini cha udhaifu wa hiyo barabara ili tukimpata aliyesababisha ajenge kwa gharama yake sehemu iliyoharibika, Senkenke mpaka Sheruhi, ni mfano mwingine ambapo tayari tunafanya utafiti uchunguzi kwenye maabara yetu kuu tukimjua mtu ambaye ni responsible atafanya kwa gharama yake mwenyewe. Barabara ya Kyamyla, Buzilayombo, vilevile nayo iko chini kwa hiyo iko mifano mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kidogo tu kwamba suala la kuhakikisha ubora wa barabara zetu, suala la kuhakikisha kwamba barabara zetu zinabeba thamani ya pesa, siyo wajibu wa Wizara ya Ujenzi tu lakini wajibu wetu wote tuliomo humu ndani ya jengo. Kila barabara inapojengwa katika mkataba inakuwa defect liability period, kipindi cha uangalizi wa uzima wa hiyo barabara, barabara za lami mara nyingi inakuwa mwaka mmoja, sisi tumeongeza mpaka miaka mitatu, hata za changarawe ni zina miezi sita, kwa hiyo ningeomba Waheshimiwa Wabunge katika hicho kipindi, msitusubiri sisi tu lakini mnaweza na nyie mkachukua hatua pale unapoona kuna dalili ya udhaifu katika barabara tufahamishwe ili aliyejenga au mhandisi mshauri kama ndiyo alisababisha wajenga hizo barabara kwa gharama zao wenyewe. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Kwa majibu hayo yanayotosheleza sasa tuhamie Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nimwite Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi.

Na. 441

Kuhusu Kuviwezesha vituo vya Utafiti katika Kilimo

MHE. AMINA NASSOR MAKILAGI aliuliza:-

Matumizi ya mbolea hutegemea aina ya udongo na tunavyo vituo vya utafiti katika kila kanda ambavyo vinakabiliwa na changamoto mbalimbali katika kufikia utekelezaji wa majukumu yake.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha inatenga fedha za kutosha ili kuviwezesha vituo vya utafiti kutekeleza wajibu wao kikamilifu?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wea Viti Maalum na Katibu Mkuu kama ifuatavyo:-

Matumizi ya mbolea yanategemea aina ya udogo na zao husika hapa Tanzania utafiti wa mbolea na mazao unafanya katika kanda saba zilizoundwa kulingana na mazingira ya ki-ikolojia. Kanda zilizopo na majina ya vituo vyake vya utafiti katika mabamo ni kanda ya Mashariki ambayo kituo cha utafiti kiko llonga - Kilosa, Kanda ya Magharibi kituo cha utafiti Tumbi - Tabora, Kanda ya

Kasakazini kituo cha Selian - Arusha, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kituo Uyole Mbeya, Kanda ya ziwa kituo cha UKiriguru - Mwanza na Kanda ya Kusini kituo cha Naliendele - Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazovikabili vituo vya utafiti ni pamoja na kupungua kwa watafiti kwa sababu ya kustaafu na uhaba wa fedha za kufanya utafiti. Ili kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imeazimia kuongezea fedha za utafiti kufikia angalau asilimia 1 ya pato ghafi la taifa. Katika kutekeleza azma hii, Serikali itatumia takriban shilingi bilioni 30 kupitia Wizar ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuboresha shughuli za utafiti.

Katika mwaka 2010/2011, Serikali imetenga shilingi bilioni 19 kwa ajili ya mafunzo ya watafiti katika ngazi ya shahada na shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu, yaani *Bachelors, Master* na *Ph.D. Degrees*. Aidha, mwezi Juni, 2011 Serikali imetoea tena shilingi bilioni 15 kupitia *COSTECH*, kwa ajili ya kugharamia utafiti na kuboresha miundombinu katika vituo vya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ku pitia progamu ya kuendeleza sekta ya kilimo na programu ya kuendeleza tija na uzalishaji katika Afrika ya Mashariki yaani *Eastern Africa Agricultural Productivity Programme* itaendelea kukarabati na kujenga nyumba mpya katika vituo vya utafiti, kununua vitendea kazi, vifaa vya usafiri ikiwa ni pamoja na magari na pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni ukame unoathiri mara kwa mara mashamba ya utafiti na uzalishaji wa mbegu. Wizara yangu imeanza kukabiliana na tatizo hili kwa kuanza kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba yote ya utafiti. (*Makofii*)

MHE. AMINA NASSOR MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza, naomba kuuliza maswali hayo kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Serikali imeanda mpango mzuri sana ya kukarabati na kujenga vituo vya utafiti vilivyopo katika baadhi ya mikoa yetu. Je, sasa Serikali haioni ipo haja sasa ya kujiandaa vizuri na kutenga fedha za kutosha ili kuzalisha watafiti wa kutosha, kwa sababu wataalam wa sekta hii ya utafiti walio wengi wana umri mkubwa sana na baadaye tutakosa wataalam katika sekta hii? (*Makofii*)

Swali la pili, kwa kuwa katika baadhi ya maeneo hasa katika mikoa ya kanda ya ziwa, na kanda ya kati hizi pembejeo za vocha bado hazijawafikia kikamilifu. Je, Serikali sasa ina mkakati gani kuhakikisha na mikoa hii sasa inapata pembejeo za vocha? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana swalii la Katibu Mkuu wa UWT ni swalii la kinamama wote majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Chakula na Ushirika. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali mazuri sana ya Mheshimiwa Makilagi kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, tumedhamiria kwamba tutenge angalau asilimia 1, ya pato la taifa. Na kwa nyakati tofauti wale mnaofuattilia Mheshimiwa Rais mwenyewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu, wamekuwa wakitembelea vituo vya utafiti na wameona changamoto zinazowakabili, na Mheshimiwa Rais mwenyewe ameshatoa na maelekezo kabisa ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kutosha kama nilivyosema katika majibu ya msingi, na pamoja na kutoa motisha kwa watafiti na tayari tumekwishaanza kutekeleza.

Lakini pia naomba nimfahamishe Mheshimiwa Makilagi, kwamba tayari tumeshatenga fedha shilingi bilioni 4, tumezitoa kwa ajili ya watafiti 33 ambaao watafanya shahada ya *Masters* na wengine 12, kufanya shahada ya *Ph.D.*

Lakini tunaendelea kufanya hivi kwa nyakati tofauti ili wataalam wetu hawa waweze kupatikana kujaza pengo la wale ambaao wanastaafu. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa swalii hili

nzuri na sisi tumeshalionna na Mheshimiwa Rais ameshalitolea maekelezo na tunaendelea kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuhusu mbolea ya ruzuku, Mheshimiwa kidogo hili swali liko nje lakini nadhani ni vizuri nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu yanaelekea huko huko kwa sababu wataalam wetu hawa ndiyo wanaofanya hata utafiti wa udongo na kujua mbolea gani itumike kwa wakati.

Kwa hiyo, kwa sasa niseme tu kwamba tutaendelea kuangalia zile wilaya ambazo hazikubahatika kupata mbolea ya ruzuku. Japokuwa kwa mwaka huu kwa msimu huu lazima nikiri kwamba mbolea ya ruzuku hatikuwa kama ile iliyokuwa mwaka jana. Itapungua kidogo kulingana na ufanyu wa Bajeti, lakini tutaangalia yale maeneo ambayo yanahitaji kupata mbolea zaidi, na baada ya kufanyiwa utafiti wa udongo, basi msimu unaofuata pia tutaangalia tuweze kuongeza mbolea yenyeye ruzuku.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, wakulima wengi wakiwemo wakulima wa Jimbo la Kwimba, jimbo ninalotoka ni maskini na hawawezi ku-afford kununua mbolea hata kwa kutumia vocha.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kuwapatia wakulima hao mbolea bure ili tuwakwamue kuwaondoa kwenye umaskini?

NAIBU SPIKA: Mbolea ya bure, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Chakula na Ushirika.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, leo naona ni maswali ya kinamama tu kama ifuatavyo:-

Sio rahisi kwa kweli kusema kwamba sasa tunao uwezo wa kuwapatia wakulima wote mbolea ya bure, hata wale ambao tumetenga mbolea ya ruzuku hatujaweza kuwafikia wote. Tumejitahidi sana tumefikia wakulima milioni mbili (2) na msimu huu tunatarajia kuwafikia wakulima milioni 1.8 kwa mbolea ya ruzuku.

Tunachokifanya sasa ni kujaribu kuwajengea uwezo wakulima hao. Kwanza wajue matumizi sahihi ya fedha, tujue na udongo wao unahitaji mbolea gani, halafu baadaye sasa tujenge utaratibu mzuri utakaowezesha wakulima hawa kuweza kujinunulia mbolea wenyewe kutoka kwenye taasisi mbalimbali.

Lakini kwa sasa tukisema kila mkulima wa Tanzania tutampelekea mbolea au mbolea ya bure, nadhani nitakuwa nasema uwongo hapa kwa sababu nina hakika kwamba hatuna uwezo wa kufikia wakulima wote kuwagawia mbolea ya bure.

NAIBU SPIKA: Tuhamie Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Waheshimiwa Wabunge, muda mkiuangalia umebakia mdogo sana, maswali ni matatu, Mheshimiwa Said Amour Arfi, endelea.

Na. 442

Kuboresha Makazi ya Askari Polisi na Askari Magereza - Mpanda

MHE. SAID A. ARFI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa Kuboresha Makazi ya Askari Polisi na Askari Magereza Mpanda?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali 442. Waheshimiwa Wabunge hilo ni swali la kibunge, kama hilo lilivyo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mpango wa kujenga na kuboresha makazi ya askari polisi na magereza nchi nzima. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti zoezi hilo linatekelezwa kwa awamu kadri tunavyopata fedha.

Aidha, tunao mkakati wa kutumia vifaa vya ujenzi vinapopatikana katika maeneo husika kwa nia ya kupunguza gharama za ujenzi. Kupitia mkakati huu katika mwaka wa fedha 2010/2011 tumefanikiwa ujenzi wa nyumba mbili za askari magereza Mpanda na ujenzi wa nyumba tatu unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa nyumba za Askari Polisi na Magereza nchi nzima ni zoezi endelevu. (*Makofii*)

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, pamoja na kupatikana kwa vifaa vya ujenzi tena kwa gharama nafuu lakini nyumba zinazojengwa ni chache sana. Nyumba zilizokamilika ni mbili na sasa zinajengwa nyumba tatu kwa askari wa magereza. Unadhani kwamba hatua hiyo itamaliza tatizo la makazi kwa askari polisi na askari magereza Mpanda?

La pili, inachukua muda gani ili Serikali iweze kutekeleza hasa pale inapopewa taarifa kama vile kwa zaidi ya takribani miaka minne nimekuwa nikisemea Gereza la Mahabusu Mpanda liko katika hali mbaya, hata ukarabati wake haujafanyika.

Naomba tu niambiwe inachukua miaka mingapi, ili ukarabati wa Gereza hilo uweze kufanyika?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Arfi, Mheshimiwa Mbunge, haya masuala na matatizo tumekuwa tunayazungumza mimi na wewe. Tatizo siyo kwamba Serikali ama Wizara haina nia kabisa tunapenda askari wetu wa polisi, wa magereza wapate makaaozi mazuri na pia tunapenda magereza yetu yaboreke. Tatizo kubwa tulilokuwa nalo na ambalo linatukabili na ndiyo maana nakuwa na tatizo ama kigugumizi kidogo kukwambia kwamba tunaweza tukakamilisha wakati fulani.

Tatizo kubwa tulilonalo ni tatizo la uhaba wa rasilimali fedha, na kwa kweli Bajeti ingekuwa inaruhusu tungefanya kama tunavyofanya. Kwa sababu changamoto tuliyonayo siyo ya Mpanda peke yake, Mheshimiwa Mbunge anaewela ni suala la kitaifa, tunazungumzia taifa zima. Kwa hiyo, naomba tu awe na imani, tutakavyozidi kuwa tunapata fedha tutazidi kuboresha.

Lakini nichukue nafasi hii niwashukuru sana wananchi, katika maeneo mbalimbali ya Tanzania ambao wamekuwa wakishiriki katika michango yao mbalimbali ya kuboresha majengo, ofisi na kadhalika.

MHE. PETER SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niulize swalii la nyongeza. Ni kweli tuna rasilimali chache, kupanga ni kuchagua ningewomba Mheshimiwa Naibu Waziri, katika kuchagua machache ya kuanzia kwanini asianzie na nyumba za askari wa pale Kigoma na magereza ambao kwa kweli hali yao ni mbaya sana. (*Makofii*)

Lakini pia Askari wa Kigoma wanaishi maisha magumu, maisha wanayoishi pale kwa sababu ule mpaka wetu ni mpaka ambaa una majambazi wana *take risk* kubwa. Kwa hiyo, nilitarajia Serikali na hilo nalo walione watupe *priority* ili tuwasaidie Polisi na Askari Magereza waliopo Mjini Kigoma. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Peter J. Serukamba, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kwamba kupanga ni kuchagua na nimwambie tu kwamba ni tatizo la kitaifa kuhusu makazi na kuhusu majengo ya Askari Polisi, Askari Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na kadhalika. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba kwa kuwa tumetamka hapa na Waziri alitamka katika Bajeti yetu ambayo tunashukuru mlipitisha kwamba ni mpango wetu ambaa ni mpango endelevu kuona kwamba ifikapo mwaka 2015 tutakuwa tumejitahidi maeneo mbalimbali na Kigoma ikiwemo kuona kwamba tumeboresha makazi ya Askari wetu wote.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, Mamlaka ya Mji mdogo wa Mombo unakuwa kwa haraka na kwa kuwa kituo cha Polisi cha Mombo ni nyumba ya Mamlaka ya Mkonge.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo cha Polici Mombo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngonyani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani kama nilivyo sema hapa na kila mara ninapokuja hapa hili ni tatizo ambalo linatupa changamoto ambayo tunayo kitaifa lakini kweli kama anavyosema kwamba kituo cha Mombo na kukua kwa mji Mdogo wa Mombo na ile hadhi ya nyumba iliyokuwepo pale ambayo tunaifahamu, nimhakikishie tu kwamba katika program yetu ambayo tunaifanya kwenda kufika mpaka mwaka 2015 hilo jambo lipo ndani ya program yetu lakini kikubwa ni kutafuta raslimali fedha ili kuhakikisha kwamba hiyo program yetu inatekelezeka. (*Makofii*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa mpango wa kuboresha makazi ya Askari Polisi na Askari Magereza yanatakiwa yaendane na kuboresha mazingira ya kazi. Je, sasa Serikali imeshaanza kufikiria mpango wa kiwango gani muafaka Askari Polisi na Askaari Magereza wanatakiwa walipwe ili kiweze kuendana na hali ya maisha ikiwemo kupanga ama kujenga makazi mapya?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David E. Silinde, kama ifuatavyo:-

Kwa kweli nafarijika sana kuona kwamba Wabunge wengi hapa wanachukulia haki ama tusema maslahi ya Askari Polisi na Askari Magereza kwa nguvu sana. Suala la kuwasaidia kuhusu mambo ya makazi wale Askari ambaa wanakaa makambini utaratibu tuliokuwa nao ni kwamba wanazo nyumba ingawaje si nyumba nzuri lakini ni nyumba. Kwa hiyo, hakuna kinachofanyika kusema kwamba tunawapa posho ya kuweza kuwasaidia katika hilo. Lakini wale ambaa wanakaa nje ya kambi tuna utaratibu ambaa wanapata stahiki ya kuweza kuwasaidia katika nyumba ambazo wanapangisha.

Lakini naomba kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba Tume ya Maslahi ama Tume ambayo inashughulikia haki na stahiki za Jeshi la Polisi, Askari Magereza na sasa itakuwepo pia Uhamiaji itakuwa na kikao kulitazama hili suala tena upya na kuona kwamba Askari wetu wanawenza kupata stahiki inayofaa kuendana na mazingira tuliyokuwa nayo, wakati tulio nao lakini pia kutazama na hali halisi ya raslimali fedha tuliyokuwa nayo. (*Makofii*)

Hitaji la Gari la Magereza Mbeya

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA aliuliza:-

Jeshi la Magereza Wilayani Mbeya halina gari kwa ajili ya kulihudumia Gereza na Mahabusu kwenda nakurudi Mahakamani.

Je, ni lini sasa Serikali italipatia Gereza hilo gari kwa mahitaji ya kulihudumia Gereza hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:- Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi, napenda kaujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali katika kuboresha miundombinu vikiwemo vyombo vya usafiri (Magari) katika magereza yote nchini ni endelevu kulingana na mahitaji yake.

Kuhusu usafirishaji wa Mahabusu kwenda Mahakanani na kurudi Gerezani, jukumu hilo linatekelezwa kwa awamu ambapo zoezi hilo lillianzia Mkoa wa Dar es Salaam na baaadhi ya Wilaya za Mkoa wa Pwani na sasa litaendelea kutekelezwa katika Wilaya zilizosalia katika Mkoa wa Pwani na kuanza Mkoa wa Arusha. Lengo ni kupanua utekelezaji wa zoezi hilo katika Mikoa mingine ukiwemo Mkoa wa Mbeya kadri hali ya Bajeti Wizara itakavyoruhusu.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Mahabusu wengi wanaolundikana katika Gereza la Ruanda kwenye Jiji la Mbeya ambalo lina Mahabusu wengi sana na Mahabusu wengine wanatokea Wilaya ya Chunya ambapo pia hakuna Gereza na Mahabusu wengine wanatokea Wilaya ya Kyela ambapo hakuna Gereza wenyewe wanarundikana kwenye Gereza la Tukuyu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anatuambia nini katika mkakati wake wa kuhakikisha kwamba jambo hili linatiliwa mkazo?

Askari Magereza wa Gereza la Ruanda Mbeya wako 221, nyumba zipo 70, Wilaya ya Mbozi nako Askari Magereza wanakaa makambini hawana nyumba. Naibu Waziri anatuambia nini katika kuhakikisha kwamba jambo hili linatiliwa mkazo pamoja na kwamba kipato cha Serikali ni kidogo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, kama ifuatavyo:-

Kuhusu swalii lake la kwanza nataka kumwambia kwamba uhaba wa vyombo vya usafiri kama magari upo lakini katika Gereza Kuu la Ruanda tunayo magari matatu hivi sasa ambayo yanafanya huduma hiyo na yapo sawasawa yanafanya huduma hiyo.

Hoja imekuwa ni kuongeza tu magari na kuanzisha utaratibu rasmi wa kuweza kuwatoa Mahabusu kutoka Magerezani na kuwapeleka Mahakamani. Niseme huu ni mpango ambao tunao na niombe nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jinsi tutakavyokuwa tunajipanga lakini kikubwa ni fedha tutahakikisha kwamba hili linatekezeza kwa sababu ni mpango ambao tayari tumeuanza tangu mwaka 2008 na kama nilivyojibu katika jibu langu hapa tumeanzia Dar es Salaam lakini mwaka huu tunakwenda Arusha na kadhalika.

Kuhusu swalii la pili ambalo linahusu makazi, hii kwa kweli nimwambie Mheshimiwa Mbunge Dkt. Mwanjelwa kwamba hili ni *challenge* kubwa ambayo tunayo na kama jana mmeona pale Dar es Salaam Makamu wa Rais amezindua nyumba za Askari na bado tunaendelea lakini pia tunaendelea katika Mikoa mingine ya Tanzania.

Kwa hiyo, nimwambie kwamba *program* yetu ambayo tunaitazamia katika kipindi hiki mpaka kufikia mwaka 2015 tutajitahidi kadri tuwezavyo kwa sababu hili si tatizo niseme kwa ukweli ambalo limeanza mwaka huu au mwaka jana, ni tatizo ambalo limekuwepo kwa muda mrefu sana.

Kwa hiyo, awamu hii ya Serikali inajitahidi kulitatua na ndio maana tunapata matatizo yaliyokuwa makubwa kwa sababu ingekuwa maeneo fulani yamekuwa sawa. Kwa hiyo tunashughulikia maeneo fulani ya nchi ingekuwa barabara, lakini sasa ni tatizo ambalo tunalitazama katika Tanzania nzima. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira na wananchi pamoja na Askari wetu wawe na subira. Lakini azma na nia ya kutekeleza hili tunayo sana.

Na. 444

Ubinafsishaji wa Mgodi wa Nyanza Salt Mines Limited

MHE. DAVID Z. KAFULILA aliuliza:-

Kwa sababu mchakato mzima wa ubinafsishwaji wa Mgodi wa *Nyanza Salt Mines Ltd.* uligubikwa na utata mkubwa.

- (a) Je, Serikali inaweza kueleza thamani ya Mgodi kabla ya kubinafsishwa na thamani ya Mgodi baada ya kubinafsishwa?
- (b) Kabla ya ubinafsishaji huo, *PSRC* ilitoa tangazo pamoja na mambo mengine kulipa mkono wa kwaheri lakini ni muongo mmoja umepita. Je, ni lini mkono huo wa kwaheri utatolewa?
- (c) Je, ni kwa kiasi gani mwekezaji huyo anazingatia Sheria za kazi kwa watumishi wake?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Thamani ya Mgodi kabla ya kubinafsishwa ilikuwa ni kati ya shilingi billioni 1.16 na shilingi billioni 1.91 (mwaka 1996) na thamani ya mgodi ulipobinafsishwa mwaka 1999 ilikuwa ni shilingi 1,168,080,000/= (Serikali ilikuwa na hisa 81.33% sawa na shilingi 950,000,000/= na *M/S Bridge Balgie Ltd.* ilibaki na hisa 18.67% sawa na shilingi 218,080,000/=).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu zinaonyesha kuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma yaani *PSRC* haikuwahi kutoa tangazo kabla, wakati au baada ya ubinasishaji kuwa itawalipa mkono wa kwaheri kwa wafanyakazi wa *Nyanza Salt Mines Limited* kwa kuwa hali ya kifedha na uendeshaji wa kampuni hiyo ilikuwa mbaya sana.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria za Tanzania, kila mwajiri ana jkumu la kuzingatia sheria za kazi kwa watumishi wake. Serikali inaanmini kuwa, mwekezaji katika kampuni hii anazingatia Sheria za kazi kwa watumishi wake kwa mujibu wa Sheria.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwa majibu yasiyo na matumaini kabisa ya Wizara hii ya Fedha lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Moja, wakati wa mchakato wa ubinafsishaji moja ya sababu kubwa ya wafanyakazi hawa kulinwa kidogo ni kiasi kidogo cha fedha ambazo *Nyanza Salt Mine* ilikuwa ikiipeleka kwenye mfuko wa hifadhi na kwa mujibu wa taratibu *CHC* ilikuwa na wajibu na ina wajibu wa *ku-compensate* kiasi ambacho kilikuwa hakipelekwi kwenye mifuko ya hifadhi kwa ajili ya kuhakikisha

kwamba wafanyakazi wale wanapata kiasi chao ambacho ni stahiki na kwa taarifa ni kwamba kuna wafanyakazi ambao wamefanya kazi takribani miaka 10, 20 au 30 wamepata mafao ya shilingi 100,000/=, 200,000/= au 400,000/= kiasi ambacho kinatokana na tathmini mbovu kabisa iliyofanywa na Wizara wakati wa ubinafsishaji. Napenda kujua, ni lini Serikali itafanya tathmni upya ya mafao halali ya wafanyakazi hawa?

Pili, Mgodi ule wa *Nyanza Salt Mine* ni mgodi ambao ulikuwa unategemewa katika eneo lote la Afrika Mashariki na Kati kwa kuzalisha Chumvi bora, soko la Zambia, Kongo, Rwanda, Burundi na Tanzania yenyewe.

Lakini mgodi ule ulibinafsishwa kwa malipo ya awali ya shilingi milioni 95. Mgodi ule baada ya kubinafsishwa mwekezaji yule ameanza kung'oa, siyo leo, ameng'oa mitambo ya mgodi ule iliyojengwa na Waitaliano miaka ya 1990 na mwekezaji yule anauza nyumba za mgodi ule. Naijuliza hii Serikali ilibinafsisha mgodi ili uendelezwe au ilibinafsisha kwa maana ya kugawa tu?

Naomba Serikali iniambie ni lini uchunguzi utafanya kuhusu sakata hili ili kusudi thamani halisi ya Watanzani ipatikane.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa David Kafulila, kama ifuatavyo:-

Hili la pili la uchunguzi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kuitia shirika la *CHC* itafanya uchunguzi na kuangalia halafu tutawasialiana na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kujua hatma baada ya uchunguzi wa *CHC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kwanza kuhusu malipo naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba taarifa ambazo zipo mpaka sasa ni kwamba wafanyakazi wote ambao waliachishwa kazi walishalipwa malipo ya mafao yao kisheria na endapo kutakuwa bado kuna wengine ambao hawajalipwa madai yao basi *CHC* yaani *Consolidated Holding Cooperation* itachunguza na itahudumia ipasavyo hawa wengine ambao watakuwa bado hawajalipwa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, nazidi kusitiza katika maswali ambayo mnazidi kuyatunga basi myatunge maswali ambayo ni mafupi ambayo yanajielekeza moja kwa moja kwenye eneo ambalo unataka kuliuliza. Ukiangalia swali la Mheshimiwa David Z. Kafulila leo, amechomeka maswali manne ndani ya swali moja, sasa kwa vyovypote vile muda wetu wa saa moja hauwezi kutosha ambao unatarajiwu kwa kipindi hiki cha maswali. Nazidi kusitiza kwa Waheshimiwa Wabunge wote kutunga maswali ambayo ni mafupi yanayojielekeza kwenye eneo ambalo una nia ya kuihoji Serikali.

Matangazo ni kama ifuatavyo: Kwanza naanza na wageni walipo kwenye jukwaa la Spika. Naomba kuwatambua wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige. Kwanza ni familia yake yupo mke wake Reberata Maige, karibu sana Mama Maige, kazi inayofanywa na Mzee ni kazi nzuri. Pia yupo mtoto wake Geoffrey na Kabula. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ni pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara Bi. Maimuna Tarishi, Naibu Katibu Mkuu Bi. Nuru Milao, Mshauri wa Wizara katika masuala ya Operesheni na Intelijensia na Kamishna Msaidizi wa Polisi Mstaafu Venance Tosi. Hii ni kuwaambia majangili wote nchini kwamba Kamanda Tosi sasa anashughulika nao kwenye Hifadhi zote na mapori ya akiba nchini, kama mshauri wa Wizara katika oparesheni ya mambo hayo. Karibuni sana. (*Makofii*)

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Waziri Dr. Ladislaus Komba ambaye ameambatana na mke wake ambaye alikuwa ni Katibu Mkuu aliyejita wa Wizara hii.

Pia wapo Wakurugenzi wa Wizara pamoja na Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo ndani ya Wizara na watumishi wa Wizara karibuni sana na kwa siku hizi mbili mtapata

ushauri mwangi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, tutawaomba sana muuzingatie katika kazi zenu za kila siku za utumishi wenu. Karibuni sana. (*Makof*)

Wapo pia wageni wa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Aggrey D. Mwanri, ambao ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Siha Ndugu Jonathan Nasari, Ndugu Rashid Kitambulilo - Mkurugenzi Mtendaji Siha na Katibu wa Mbunge Ndugu Justice Mkita, karibuni sana. Katibu wa Mheshimiwa Mwanri, matunda ya kazi yako ni kwamba Mheshimiwa Mbunge yuko humu ndani analitumikia Taifa. (*Makof*)

Pia yupo Ndugu Michael Brashi, *Project Manager* wa mradi wa maji, Siha. Karibuni sana hapa Bungeni Dodoma. (*Makof*)

Wageni wa Mheshimiwa James Daud Lembeli, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira inayowasilisha *report* yake leo baada ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ni mdogo wake Mheshimiwa James Daud Lemeli ambaye ni Mhandisi Reginald Daud Lembeli, mtoto wake Wizilia James Lembeli na Mpwa wake Wilfred Ndembu Lunda. Karibuni sana. (*Makof*)

Mgeni wa Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, ni Ndugu Jamal Kazinja, ni matumaini yangu kuwa yupo hapa Bungeni lakini eneo la *Basement* kutokana na kukosa nafasi kwenye *Gallery* zetu. Karibuni sana Bungeni. (*Makof*)

Pia wako wageni wa Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji ambao ni Makatibu 18 wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Kata kutoka kule Mtwara wakiongozwa na Ndugu Hawa Mangasala, Mwenyekiti na Katibu wa UWT wa Wilaya ya Mtwara. Karibuni sana wageni wetu kutoka kule Mtwara, mmesafiri kutoka mbali kabisa, karibuni na niwahakikishieni Mbunge wenu Mheshimiwa Hasnain anafanya kazi nzuri hapa Bungeni. (*Makof*)

Pia naomba kuwatambulisha wageni ambao ni Madiwani 27 kutoka Jimbo la Bumbuli, wageni wa Mheshimiwa January Makamba. Waheshimiwa Madiwani kutoka Bumbuli karibuni sana, niwahakikishieni pia kwamba January Makamba, Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Nishati na Madini, anawawakilisha ipasavyo ndani ya ukumbi huu. Karibuni sana. (*Makof*)

Wageni wa Mheshimiwa Susan Kiwanga, ni Coretha Mwanjoka kutoka Dar es Salaam, Godi Luena na Jonson Msuya kutoka Kilombero. Ahsanteni sana na karibuni sana. Mheshimiwa Susan hakuweka uhusiano. (*Makof*)

Wageni 40 wa Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki ambao ni watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu pamoja na akinamama kutoka Rah Man *Orphanage Centre* Dodoma. Wageni wa Mama Mfaki tunawakaribisha sana wageni wetu, karibuni sana Bungeni, tunafurahi kuwaona mpo pamoja nasi. (*Makof*)

Sasa matangazo ya vikao, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara, anawaomba Wabunge wa Mikoa ya Mtwara na Lindi na kutoka Tunduru kukutana leo jioni baada ya kuahirisha Bunge kwenye saa 1.30, ukumbi wa Msekwa.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa Wabunge wote wa CCM, anawaomba Wabunge wote wa CCM kukutana baada ya kuahirisha kikao cha Bunge, saa 7.15, ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa January Makamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake ya Nishati na Madini kwamba baadaye leo mchana kwenye saa 7.20, Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane chumba namba 227.

Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, wale Wabunge ambao wanataka Miongozo au Utaratibu, naomba wasimame wote kwa wakati mmoja, ni watatu na Mheshimiwa Naibu Waziri Afya. (*Makof/Kicheko*)

Tuanze na Mheshimiwa Mkosamali halafu Mheshimiwa Mtima.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) juu ya swali alilouliza Mheshimiwa David Kafulila Na.444 kwa sababu wakati Mheshimiwa Waziri anajibu katika kipengele cha (c) alisema tu kwamba Serikali inaamini kwamba wafanyakazi wale kwenye mgodi ule wanalipwa maslahi yao na wanalipwa kwa mujibu wa sheria lakini nchi haiongozwi tu kwa kuamini kwamba mtu anafanya vile, nchi haiongozwi kwa imani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilitaka nipate Mwongozo wako kwamba hili suala ni suala muhimu sana na kwenye mgodi ule kuna wizi mkubwa sana unaendelea kufanyika, kuna mitambo inaendelea kuuzwa, sasa hivi kuna mitambo ya zaidi ya shilingi bilioni nne imeuzwa na huyu mwekezaji. Sasa ningependa kupata Mwongozo wako kama Waziri amesema atafanya uchunguzi, sasa tujue uchunguzi huu utafanyika lini kwa sababu hili ni suala linaloangusha Taifa. Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako kama Waziri anaweza kusimama hapa akatuambia lini uchunguzi huu utafanyika?

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na Mwongozo wangu nataka kurekebisha *Hansard* kwa ajili ya kuweka rekodi sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi kwa ajili ya kuitisha mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, nilipata fursa ya kuomba ufanuzi kutoka kwa Waziri lakini wakati naomba ufanuzi kuna kauli ambayo nilizungumza ambayo binamini haikuwa sahihi. Natambua kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila Mtanzania ana haki ya kuishi mahali popote na natambua kabisa Mkoa wa Morogoro bila wageni tusingewenza kuendelea. Kauli ile mimi mwenyewe ilinumiza, sikuwa na amani toka jana mpaka leo hii ninapoomba Mwongozo wako na niliwaumiza Watanzania wengi wanaoniamini kama Klongozi. Kwa hiyo, naomba kufuta kauli, naomba radhi, naomba *Hansard* irekebishe yale niliyoyazungumza jana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawakaribisha Watanzania wote Mkoani Morogoro mje kuwekeza. Tuko pamoja hata mimi mwenyewe natarajia kuolewa na mtu ambaye sio wa Mkoa wa Morogoro, kwa hiyo, nawakaribisha wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba Mwongozo wako.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa tu taarifa kwa mujibu wa Kanuni hiyo hiyo ya 68(7) juu ya hoja aliyoitoa Mheshimiwa Mkosamali kuhusiana na swali liliolizwa kwa Wizara ya Fedha. Ni kweli kwamba Naibu Waziri yale majibu aliyojibu ni sahihi lakini nilitaka kutoa majibu ya nyongeza kwa Mwongozo aliota kwamba Wizara ya Viwanda kwa kushirikiana na *CHC* wameshafanya mapitio kuangalia viwanda vyote vilivyobinafsishwa ikiwepo Uvinza na hivi sasa wanakamilisha hiyo taarifa, maeneo yote ambayo yamebinafsishwa na kuandaa *status report* kwa sababu walishaagizwa na Serikali kufanya jambo hilo. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia kwamba huo uchunguzi si suala jipya kama aliyosema Mheshimiwa Mbunge, hivi sasa wanakamilisha hiyo ripoti ya uchunguzi walioufanya si kwa Uvinza peke yake kwa viwanda vyote vilivyobinafsishwa ili kuandaa ripoti ambayo inaonyesha tangu walivyobinafsishwa kazi iliyo fanyika na kama wale walibinafsishwa wametimiza malengo yaliyokusudiwa na Serikali na sasa Serikali inataku kuandaa taarifa ya kuonyesha hatua zitakazochukuliwa kwa wale amba walikiuka masharti ya mauzo. Kwa hiyo, nilitaka kutoa taarifa hiyo.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge). Niseme naishukuru Serikali kwa ufanuzi huo na kwa maana hiyo Mheshimiwa Mkosamali na Mheshimiwa Kafulila jambo hili linashughulikiwa, Serikali wanalo, wanalipitia, kwa hiyo, lile swali la kusema ni lini hebu tuwape nafasi waweze kufanya kazi jambo hili.

Nikienda kwa Mwongozo alioutaka Mheshimiwa Regia Mtema, mimi binafsi kwa niaba yenu na Watanzania wote nimshukuru sana kwa uungwana ambao amekuwa nao wa kurekebisha kauli, huu ndio Ubunge jamani. Nyumba hii ni kubwa na mambo ni mengi, unawenza kujikuta umesema jambo ambalo hukulitarajia. Sasa wengine wetu hapa hata akisema jambo ambalo sio basi anang'ang'ana tu. Taratibu zipo unachukua nafasi baadaye tunakupa fursa unaliweka vizuri kama Kiongozi kwa sababu kila tunachokiongea kinaingia katika Kumbukumbu za Bunge inaitwa *Hansard*. Hata wajukuu zako watakuja kusoma na kuona hivi babu au bibi alipokuwa Bungeni alisema hili kweli? Kwa hiyo, ni fursa muhimu ambayo sote tungeitumia vizuri. Nampongeza na kwa jinsi hiyo naagiza Kitengo chetu cha *Hansard* kurekebisha maneno yale aliyozasema Mheshimiwa Regia Mtema jana na kuyaweka haya aliyozasema leo.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Wizara ya Maliasili na Utalii

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka 2010/2011 na Mpango wa Utekelezaji na Malengo kwa mwaka 2011/2012. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuiongoza nchi yetu. Pia niwapongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kuteuliwa kwa mara nyingine kuwa Waziri Mkuu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Anne Semamba Makinda kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa kwanza Mwanamke katika historia ya nchi yetu. Naomba nikupongeze pia wewe mwenyewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Naibu Spika wetu. Vilevile nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mukutano huu ni wa kwanza wa Bajeti tangu Bunge hili liundwe baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Naomba kutumia nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wenzangu wa Jimbo la Msalala kwa kunichagua kwa kura nyingi ikiwa ni kielelezo cha imani yao kwangu. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa na imani kubwa kwangu na kunituea kuiongoza Wizara hii muhimu katika kuchangia ukua wa uchumi wa Taifa letu. Napenda pia kuwashukuru watumishi wote wa Wizara hii kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza na kufanikisha majukumu niliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama na Chifu wa Wasumbwa, kwa kupokea, kuchambua kwa kina na hatimaye kuitisha makadirio ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2011/2012. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imezingatia maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na tuko tayari kupokea mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu saba. Sehemu ya kwanza ni utangulizi na sehemu ya pili inazungumzia mpango wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Sehemu ya tatu inatoa Taarifa ya Utekelezaji wa ahadi

zilizotolewa Bungeni wakati wa Bunge la Bajeti kwa mwaka 2010/2011, pamoja na maelekezo na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Bunge na Vlongozi Wakuu wa Serikali. Sehemu ya nne imezungumzia changamoto ambazo Wizara ilikabiliana nazo pamoja na mikakati. Sehemu ya tano ni Mpango wa utekelezaji na malengo kwa mwaka 2011/2012. Aidha, sehemu ya sita ni shukrani na sehemu ya saba ni hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010-2015, imeielekeza Wizara kutekeleza mambo mbalimbali ili kuziwezesha sekta zinazosimamiwa na Wizara kuchangia ipasavyo katika kukuza uchumi na ajira. Ilani, pamoja na mambo mengine, inaitaka Wizara kuboresha miundombinu ndani ya mapori ya akiba, hifadhi za wanyamapori na misitu; kuvutia wawekezaji katika Sekta ya Utalii; kuendeleza jitihada za kuhifadhi mazingira, upandaji miti na kukuza shughuli za ufugaji nyuki. Aidha, Ilani inaitaka Wizara, kukuza utalii wa ndani na nje; kupanua wigo wa vivutio vya utalii ikiwa ni pamoja na utalii wa kihistoria, utamaduni, michezo na mazingira. Vilevile, Ilani inaitaka Wizara kuelekeza jitihada katika kuboresha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, imeandaa Mpango wa Miaka Mitano ambao umeainisha mikakati mbalimbali ya utekelezaji katika kipindi hicho. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali; kuendelea kushirikisha jamii na wadau mbalimbali katika uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili, malikale na utalii na kuendelea kujenga na kukarabati miundombinu katika hifadhi za maliasili na malikale. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha Halmashauri za Wilaya katika kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili na malikale pamoja na kuendeleza utalii katika maeneo yao. Katika kuongeza kasi ya ukuaji wa Sekta ya Utalii nchini, Wizara itaendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi, kuboresha huduma kwa kupanga hoteli katika daraja na kuanza kutoa mafunzo katika kampasi mpya ya Chuo cha Taifa cha Utalii mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa wataalam, Wizara itaendelea kuboresha mafunzo katika vyuo vyake pamoja na kuongeza udahili. Aidha, ili kukuza Sekta ya Ufugaji Nyuki nchini, Wizara itaongeza maeneo ya ufugaji nyuki kwa kushirikiana na wananchi, kuboresha uzalishaji, uchakataji na vifungashio vya mazao ya nyuki pamoja na kuhakikisha asali inayozalishwa nchini inakuwa ya viwango vinavyokubalika katika soko la kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Ahadi Zilizotolewa Bungeni wakati wa Bunge la Bajeti mwaka 2010/2011. Sekta ya Wanyamapori ina jukumu la kusimamia, kuhifadhi, kuendeleza na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuanza kutumika kwa Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009, Wizara inaendelea na mchakato wa kuanda Kanuni za kuwezesha utekelezaji wake. Mwaka 2010/2011, Kanuni za maeneo matano zimekamilika na kuanza kutumika. Maeneo hayo yanahusu Uwindaji wa Kitalii; Uwindaji wa Wenyeji; Ukamataji Wanyamapori; Leseni ya Biashara ya Nyara na Utaratibu wa kutoa kifuta machozi kwa wananchi walipoteza ndugu zao walioawa na wanyamapori wakali na kifuta jasho kwa wananchi walioathirika kutohana na uharibifu wa mazao uliosababishwa na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni nydingine kwenye maeneo sita zitakamilishwa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Maeneo hayo ni: Uanzishaji na Usimamizi wa Mashamba, Bustani za Wanyamapori; Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori; Matumizi ya Wanyamapori yasiyo ya uvunaji; Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo katika hatari ya kutoweza (*CITES*); Uchimbaji wa Madini katika Mapori ya Akiba na Maeneo Tengefu na Utendaji kazi wa Kikosi Dhidi Ujangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ulinzi wa Rasilimali za Wanyamapori. Katika kutekeleza dhamira ya uhifadhi na matumizi endelevu ya wanyamapori na mazingira yake, Wizara iliimarisha uwezo wake wa kupambana na ujangili kwa kununua silaha za kisasa, magari 14, mahema 36 na sare za

watumishi 2,800. Aidha, watumishi 50 walipatiwa mafunzo maalum ya intellijensia. Hadi kufikia Mei, 2011 siku za doria 75,779 zilifanyika ndani na nje ya Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu. Jumla ya watuhumiwa 1,370 walikamatwa wakiwa na silaha 171 za aina mbalimbali (bunduki za kivita 44, *shotgun* 72, magobore 55). Kesi 466 zilifunguliwa na kati ya hizo, kesi 239 zilimalizika na watuhumiwa 145 walihukumiwa vifungo kati ya miezi sita na miaka 30 na kulipa faini ya Shilingi 79,259,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilijenga vituo vinne kwa ajili ya kupambana na wanyamapori waharibifu katika maeneo ya Terrat (Simanjiro), Kibale (Karagwe), Ngoyoni (Rombo) na Longido Mjini (Longido) na kukarabati kituo kimoja eneo la *West Kilimanjaro*. Vilevile, kwa kushirikiana na Mfuko wa Wanyamapor wa Dunia (WWF), Wizara ilijenga kituo cha doria katika maeneo ya Mtambaswala Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa miundombinu katika Mapori ya Akiba. Katika kuimarisha na kuongeza mtandao wa barabara na viwanja vya ndege katika mapori ya akiba, barabara zenyet urefu wa kilomita 132 zilitengenezwa katika Mapori ya Akiba Moyowosi na Ibanda-Rumanyika. Aidha, barabara zenyet urefu wa kilomita 178 zilikarabatiwa na mipaka yenye urefu wa kilomita 401 iliyekwa katika Mapori ya Akiba Liparamba, Burigi, Ikorongo, Mpanga-Kipengele na Selous. Vilevile, viwanja vya ndege 13 kwenye Mapori ya Akiba Selous, Maswa, Rukwa-Lukwati, Rungwa, Ibanda-Rumanyika na Ugalla vilikarabatiwa kwa kuwekewa alama za kuongoza ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, jithada za kuboresha makazi ya watumishi katika maeneo ya hifadhi ziliendelea ambapo ujenzi wa nyumba za watumishi umeanza katika Mapori ya Akiba Swagaswaga na Kanda ya Kalulu, Selous. Vilevile, Wizara inaendelea kuboresha mtandao wa kusambaza maji katika Pori la Akiba Selous Kanda ya Matambwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea na usimamizi wa ardhi oevu katika maeneo manne yaliyotengwa kama ardhi oevu yenye umuhimu wa Kimataifa (*Ramsar sites*). Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara iliratibu kazi za kiuchumi zinazozingatia matumizi bora ya ardhi kwa kutoa elimu katika Wilaya 14 za Urambo, Kigoma, Ngorongoro, Longido, Manispaa ya Iringa, Iringa Vijiji, Ludewa, Njombe, Kilolo, Mufindi, Mbeya Vijiji, Mbarali, Mbozi na Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ipo katika hatua ya mwisho ya makubaliano na Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi kuhusu kuandaa Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi katika Vijiji sita vinavyozunguka Ziwa Natron katika Wilaya za Longido na Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapor. Wizara iliendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika uhifadhi wa wanyamapor kwa kuendelea na mchakato wa kuanzisha Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapor (*WMAs*). Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wadau ilianza mchakato wa kuanzisha WMA katika Wilaya za Longido, Tunduru na Namtumbo. Jumla ya WMA nne zilianzishwa ambazo ni Ziwa Natron, Wilaya ya Longido; Chingoli Wilaya ya Tunduru na Kimbanda na Kisungule, Wilaya ya Namtumbo. Aidha, Ofisi tatu za Asasi za Kijamii (*CBOs*) zilijengwa katika Wilaya za Tunduru na Namtumbo. Wizara ilitoa Haki ya Matumizi ya Rasilimali za Wanyamapor (*User rights*) kwa Jumuiya mbili zilizoidhinishwa ambazo ni jukumu na Magingo zinazosimamia maeneo ya Jumuiya ya hifadhi ya wanyamapor ya Ukutu na Liwale sawia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi wa mali na maisha ya wananchi. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ina jukumu la kulinda maisha na mali za wananchi dhidi ya wanyamapor kwa kufanya doria za msako wa kudhibiti wanyamapor wakali na waharibifu. Hadi Mei, 2011 jumla ya siku za doria 2,743 zilifanyika katika Wilaya 13 za Rombo, Hai, Siha, Simanjiro, Singida Vijiji, Monduli, Nachingwea, Kondoaa, Biharamulo, Rufiji, Karagwe, Muleba na Serengeti. Katika kukabiliana na tatizo la Tembo waharibifu, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilitoa elimu ya kudhibiti Tembo hao kwa kutumia njia za pilipili kali iliyochanganya na mafuta machafu (*oil*) katika Wilaya za Serengeti, Morogoro, Nanyumbu, Kilosa na Kilwa. Wizara iliendelea na zoezi la kudhibiti Kunguru Weusi katika maeneo ya Kibaha, Morogoro na Dar es Salaam kwa kutumia mitego na sumu aina ya *DRC* 1339. Jumla ya Kunguru 279,158 waliuawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kutekeleza utaratibu wa kutoa kifuta jasho kwa wananchi walioharibiwa mazao yao na wanyamapori na kifuta machozi kwa wananchi waliofiwa na ndugu zao kwa kuuawa na wanyamapori wakali. Jumla ya shilingi 37,100,000.00 zilitolewa kwa wakulima 371 walioharibiwa mashamba yao yenye ukubwa wa ekari 5,390.7 katika Wilaya za Longido, Karagwe, Morogoro, Siha na Iringa Vijiji. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya wananchi 18 waliuawa na wanyamapori katika Wilaya za Chunya, Kondoa, Mbozi na Iringa Vijiji. Wizara illipa jumla ya shilingi 3,600,000.00 kama kifuta machozi kwa familia za marehemu. Nachukua fursa hii kuwapa pole wote walipoteza ndugu zao na walioharibiwa mazao kutokana na matukio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania. Mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (*Tanzania Wildlife Authority*) umeanza kwa kumteua Afisa Mwandamizi atakayeratibu zoezi la kuanzisha mamlaka. Taratibu za kuwapata wataalam elekezi kwa ajili ya kufanya kazi baadhi ya maeneo, ikiwa ni pamoja na kutayarisha Muundo wa Mamlaka, zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa maduhuli. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 30,015,900,000.00 kutokana na rasilimali za wanyamapori. Hadi kufikia Mei, 2011 kiasi cha Shilingi 31,115,093,434.08 kilikusanywa, hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 3.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwindaji wa kitalii. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilikamilisha kuandaa Kanuni za Uwindaji wa Kitalii, kutengeneza miongozo na vigezo vya kuomba vitalu vya uwindaji wa kitalii; kufanya tathmini ya vitalu na kuviweka katika daraja tano kulingana na ubora. Vilevile, Kamati ya Ushauri ya Kugawa Vitalu iliteuliwa. Baada ya maandalizi hayo kukamilika, vitalu 159 vimetangazwa katika awamu mbili tofauti na mchakato wa ugawaji kwa kipindi cha uwindaji 2013-2018 unaendelea. Mchakato huo unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Taaluma ya Wanyamapori. Wizara imeendelea kutoa mafunzo katika taaluma ya wanyamapori kuitia vyuo vya Mweka, Pasiansi na Likuyu Sekamaganga. Katika kipindi cha 2010/2011, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka kilidahili wanafunzi 453 wa kozi ndefu. Chuo kiliwawezesha pia wakufunzi sita kusomea Shahada ya Uzamivu (*PhD*) na mmoja ngazi ya Shahada ya Uzamili (*MSc*). Vilevile, mitaala ya Shahada za Usimamizi wa Wanyamapori (*Wildlife Management*) na Utalii wa Wanyamapori (*Wildlife Tourism*) imepata ithibati ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundji (*NACTE*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka 2010/2011, jumla ya Wakurufunzi 224 walihitimu mafunzo ya Usimamizi wa Wanyamapori ngazi ya Cheti cha Awali katika Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi. Aidha, Chuo kimeboresha miundombinu ya kufundishia kwa kujenga madarasa mawili yenye uwezo wa kuchukua Wakurufunzi 50 hadi 60 na bweni lenye uwezo wa kuchukua Wakurufunzi 50. Vilevile, Chuo kimekarabati madarasa mawili na mabweni manne. Chuo cha Likuyu Sekamaganga kimeendesha mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji 137. Chuo pia kimekarabati ofisi na kujenga eneo la kuegesha magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori (*TWPF*). Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori uliendelea kugharimia shughuli za kulinda wanyamapori, utafiti, mafunzo, kutoa elimu kwa umma na kuimarisha miundombinu. Hadi Mei, 2011, Mfuko ulipata shilingi 14,152,188,603.31 kutokana na makusanyo ya Wizara kuitia Idara ya Wanyamapori ikilinganishwa na makadirio ya shilingi 12,994,051,019.50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (*TAWIRI*). Mwaka 2010/2011, Taasisi ilifanya mapitio ya Mwongozo wa kufanya utafiti wa wanyamapori nchini kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Zoezi hili lilianza kwa kukusanya michango na maoni kutoka kwa watafiti wa ndani na nje ya nchi, likifiatiwa na warsha ya wadau wakuu wa utafiti wa wanyamapori nchini iliyofanyika Arusha Februari, 2011. Katika warsha hiyo, wadau walioshiriki ni pamoja na Idara za Wanyamapori, Misitu na Nyuki, Shirika la Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, Chuo Kikuu

cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma. Wadau hao walipitia Mwongozo wa Kufanya Utafiti wa Wanyamapori wa mwaka 2001 na kuandaa rasimu ya Mwongozo mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ilifanya mapitio ya maeneo ya kipaumbele ya utafiti wa wanyamapori Tanzania ya mwaka 1999 na kuainisha maeneo 15 ikiwa ni nyongeza ya maeneo matano ikilinganishwa na maeneo 10 ya awali. Maeneo hayo mapya ni mabadiliko ya tabia nchi, ufugaji wa nyuki, usimamizi wa ardhiœvu, usimamizi wa rasilimali maji, uhifadhi shirkishi jamii wa maliasili na utawala bora katika maliasili. Vipaumbele hivi vitaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Vilevile, Taasisi iliendelea na mchakato wa kukamilisha Mpango wa Kitaifa wa Kuhifadhi Tembo nchini (*Tanzania Elephant Management Plan*). Mpango huo umeainisha vipaumbele vinavyohitaji kutiliwa maanani katika kuhifadhi na kudhibiti Tembo katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Taasisi imeendelea tafiti nane kuhusu: matumizi ya pilipili katika kudhibiti uharibifu wa mazao unaofanywa na tembo; kurejea kwa Mbwa Mwitu katika Hifadhi ya Taifa Serengeti; homa ya bonde la ufa; kupe wa nyuki (*Varroa spp.*); ufuutiliaji wa mwenendo wa magonjwa ya wanyamapori; utafiti wa Sheshe (*Kobus vardonii*) katika maeneo ya Kilombero; utafiti wa Twiga Kusini na Kaskazini mwa Mto Rufiji na utafiti wa bioanuwai katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi. Aidha, Taasisi iliratibu na kusimamia utafiti wa miradi 118 ya watafiti wa ndani na nje ya nchi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ilifanya utafiti wa njia muafaka za ufugaji kwa lengo la kuungeza uzalishaji na ubora wa mazao yatokanayo na nyuki. Utafiti huo ulihusu: aina na tabia za nyuki; vifaa vya ufugaji makundi ya nyuki; mazao na masoko yake; maadui na magonjwa pamoja na uhusiano wa nyuki na mimea. Taasisi pia ilitoa mafunzo ya ufugaji wa nyuki kwa wafugaji 118 katika Vijiji vitano vya: Mamire, Gichameda, Matufa, Mapea na Sangaiwe Wilayani Babati; 92 katika Vijiji 15 vya Jimbo la Busega Wilayani Magu; 330 katika Kata za Ngarenanyuki na Oldonyo Sambu wilayani Arumeru na 10 katika kijiji cha Ololosokwan wilayani Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (*NCAA*). Katika mwaka 2010/2011, Mamlaka iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia eneo la Hifadhi ya Ngorongoro linalojumuisha hifadhi ya wanyamapori, makazi ya watu na mifugo. Mamlaka ilitumia shilingi 1,793,049,733.00 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na ununuzi wa mtambo ya kutengenezea barabara. Aidha, Kiasi cha shilingi 592,968,042.00 zilitumika kwa ajili ya kununua malori mawili kwa ajili ya kazi za ujenzi na ukarabati wa barabara ndani ya Hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka iliendelea kutekeleza miradi ya ujirani mwema kwa kujenga mabweni mawili ya Shule ya Sekondari Embarway ambapo kiasi cha shilingi 150,000,000.00 zilitumika. Vilevile, kiasi cha shilingi 200,000,000.00 zilitumika katika Ujenzi wa Bwalo, Jiko na mtambo wa Biogas katika shule ya Msingi Olbalbal. Michoro kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa katika maeneo ya Kaitakiteng, Iltulele (Naiyobi) na Ngairishi umekamilika. Aidha, kiasi cha shilingi 120,000,000.00 zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa majosho ya Alailelai, Embulbul, Nainokanoka, Meshili na Ndiani. Pia, Mamlaka ilitumia shilingi 451,000,000.00 kwa ajili ya madarasa na nyumba za waalimu katika eneo la Jema-Oldonyo Sambu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Makumbusho ya muda katika eneo la Laetoli katika Hifadhi ya Ngorongoro umekamilika, ambapo taarifa za tafiti zilizofanyika zimehifadhiwa. Aidha, katika makumbusho hiyo zimebekwa nyayo za mfano wa zile za Laetoli (*replica footprints*). Hata hivyo, upembuzi unaendelea ili kupata michoro stahiki kwa ajili ya jengo la kudumu la makumbusho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Hifadhi la Taifa (*TANAPA*). Katika mwaka 2010/2011, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania iliendelea na wajibu wake wa kusimamia uhifadhi wa maliasili na mazingira na kutangaza vivutio vya utalii. Shirika liliimarisha shughuli za doria kwa kushirkiana na Kikosi cha Doria cha Idara ya Wanyamapori pamoja na "Village Game Scouts" kwenye hifadhi

mbalimbali. Mafunzo yaliendelea kutolewa kwa Askari wa Shirika kwenye Chuo cha Wanyamapori Pasiansi. Aidha, Shirika lilihudhuria mikutano ya pamoja kuhusu uimarishaji wa ulinzi wa rasilimali za maliasili kati ya Taasisi za Kenya na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utoaji huduma za utalii kwenye hifadhi, Shirika liliendelea na jitihada zake za kuimarisha miundombinu ndani na nje ya hifadhi. Katika mwaka 2010/2011, Shirika lilijenga madaraja manne, nyumba tisa za watumishi, kukarabati mabanda ya kufikia watalii na hosteli kwa ajili ya wanafunzi, vyoo katika hifadhi mbalimbali na ujenzi wa gati katika Hifadhi ya Gombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai 2010 hadi Mei 2011, hifadhi zilitembelewa na watalii 938,737 na mapato yaliyopatikana yalifkia shilingi 94,014,769,950. Aidha, ukilinganisha na takwimu za mwaka jana kwa kipindi husika, idadi ya mwaka huu ni zaidi kwa jumla ya watalii 191,421 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 36. Ongezeko hili ni kiashiria cha kupungua kwa makali ya m dororo wa uchumi duniani na kuongezeka kwa juhudi za utangazaji utalii nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika liliendelea kutoa mchango wake kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wanaozunguka hifadhi kupitia mpango wa ujirani mwema. Miradi iliyotekelizwa ni ya kujenga na kuimarisha miundombinu ikiwemo madarasa na mabweni, zahanati, ununuzi wa samani, uchimbaji visima na kuanzisha vitalu vya miche ya miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika liliendeleza mikakati mbalimbali ya kuboresha utalii kwenye Hifadhi kwa kufanya maandalizi ya awali ya kuziwezesha kampuni binafsi kujenga kambi na hoteli za kulala wageni kwenye Hifadhi za Katavi, Ruaha, Serengeti, Mkomazi, Saadani na Kitulo kulingana na mipango kabambe ya kusimamia hifadhi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kufanya mapitio ya Mipango ya Jumla ya Usimamizi wa Hifadhi za Taifa za Arusha na Ziwa Manyara inatarajiwa kukamilika mwaka 2011/2012. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukusanya na kuchambua taarifa za awali za uandaaji wa Mipango hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, shughuli za ufuatililaji wa mabadiliko ya mazingira zilifanyika na kubaini kuwa kwa ujumla hali ya mazingira ndani ya hifadhi ni ya kuridhisha ingawa kuna changamoto ya ukame kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya mipango ya jumla ya usimamizi ya Hifadhi za Ruaha, Saadani, Mkomazi na Serengeti yalikamilika na kubaini maeneo mapya ya uwekezaji wa hoteli na kambi za utalii. Zoezi la kuandaa mipango kabambe ya kusimamia Hifadhi za Manyara, Udzungwa na Arusha lilianza. Aidha, wigo wa shughuli za utalii umeongezwa kwa kuanzisha utalii wa puto (*balloon safaris*) katika Hifadhi ya Tarangire na utalii wa kutembea kwa miguu (*walking safaris*) katika Hifadhi za Taifa Serengeti na Tarangire.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhamasisha utalii wa ndani, Shirika limekuwa likishiriki katika maonesho ya Sabasaba na Nanenane, kutoa elimu kwa umma na kutoa unaifuu wa usafiri kwenda kutembelea Hifadhi za Mikumi, Arusha na Tarangire. Kupitia programu ya Ujirani Mwema, Shirika lilitoa ushauri na kuchangia katika uhifadhi wa maeneo yenye thamani ya kikolojia katika vijiji vinavyozunguka Hifadhi, pamoja na kuhamasisha vikundi vya wajasiriamali vya kuboresha utalii wa maeneo nje ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika liliendelea kutoa elimu ya uhifadhi katika shule na vijiji, kwa kuonesha video/sinema, kuanzisha vitalu vya miche, kugawa miche shulen, kutoa elimu ya matumizi ya majiko banifu na sanifu; kuwezesha ziara za wanafunzi, viongozi wa vijiji na makundi maalum kutembelea Hifadhi. Aidha, mabango yenye ujumbe wa uhifadhi yalisambazwa kwenye Hifadhi ili yatumike katika kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha maeneo ya hifadhi yanalindwa dhidi ya uvamizi, kazi ya kuhakiki mipaka ilifanyika katika Hifadhi ya Serengeti. Kazi hiyo ilifanyika kwa kushirikiana na wataalam wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na TAMISEMI kwa maeneo yanayopakana na Pori la Akiba Maswa na Loliondo. Kazi ya uhakiki wa mpaka kat

ya Hifadhi ya Taifa Mikumi na kijiji cha Maharaka Wilaya ya Mvomero imekamilika na kuridhiwa na pande zote mbili. Zoezi la uhakiki kwa vijiji vya Ruhembe, Kihelezo na Msindazi linaendelea na linatarajiwaa kukamilika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa Gombe na vijiji vya Mpanga na Mwamgongo umemalizika kwa pande zote kufikia makubaliano. Kwa upande wa Hifadhi ya Taifa Mkomazi, uhakiki wa mipaka ulifanyika katika eneo la Igire lillio na mgogoro kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Same. Uhakiki huo ulibaini kuwa eneo hilo ni sehemu ya lillolikuwa Pori la Akiba Mkomazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro kati ya mpaka wa Hifadhi ya Taifa Tarangire na vijiji vitatu vya Gijedabom, Gedamar na Ayamango vinavyopakana na Hifadhi hiyo umekwisha kwa kufikia makubaliano na wananchi kulipwa fidia. Aidha, kwa sasa uongozi wa Wilaya una jukumu la kuwapatia wananchi maeneo mengine watakayohamia. Vilevile, mgogoro wa mpaka kati ya kijiji cha Kikondo A na Hifadhi ya Taifa Kitulo unaendelea kushughulikiwa kwa kushirikisha uongozi wa kijiji. Hata hivyo, uhakiki wa mipaka ya kiutawala kati ya Wilaya ya Makete na Mbeya uliofanyika umebaini kuwa Kikondo A iko Wilaya ya Makete na siyo Mbeya. Shirika limeanza mchakato wa kufanya marejeo ya Tangazo la Serikali (*GN*) iliyoanzisha Hifadhi kwa lengo la kufanya marekebisho muhimu yatakayosaidia kumaliza migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Misitu na Nyuki. Katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya mwaka 2010/2011, Sekta ya Misitu na Nyuki iliendelea na jukumu la kusimamia, kuhifadhi na kutunza rasilimali za Misitu na Nyuki. Rasilimali hizo zinategemewa katika kuhakikisha upatikanaji endelevu wa huduma na mazao ya misitu na nyuki kwa matumizi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera za Taifa za Misitu na Ufugaji Nyuki. Mchakato wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998 ambaa ulianza mwaka 2006 umekamilika baada ya kuingiza maoni ya Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Misitu. Mchakato wa kupitia Sera ya Ufugaji Nyuki umeanza na hadidu za rejea za kumpata mshauri mwelekezi zimekamilika. Mapitio ya sheria na programu ambavyo ni vyombo vya kutekeleza sera hizi yatafanyika mara baada ya mapitio ya kila sera.

Mheshimiwa Naibu Spika, utunzaji na usimamizi wa mashamba ya miti. Katika mwaka 2010/2011, Mashamba 16 ya miti ya Serikali yaliendelea kuhudumiwa ambapo jumla ya miche 12,926,852 ya miti aina mbalimbali ilikuzwa na jumla ya hekta 6,040 zilipandwa. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 21 ya lengo la mwaka 2009/2010. Pia hekta 4,055.6 zilipogolewa, kilomita 754.9 za barabara zilikarabatiwa na barabara za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 2,485.7 zilitengenezwa. Katika kipindi cha 2010/2011, miti yenye mita za ujazo 1,154,373 ilifikia muda wa kuvunwa. Hata hivyo kiasi kilichovunwa hadi mwezi Mei 2011 kilikuwa mita za ujazo 939,831 ambazo ni sawa na asilimia 81.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanya jitihada za kushirikisha sekta binafsi katika zoezi la upandaji miti kibashara. Uhamasishaji ulifanyika katika Wilaya tano za Njombe, Makete, Mufindi, Kilolo na Rungwe na kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya kutengeneza katiba na usajili wa vyama vya umoja wa wapanda miti. Aidha, Vijiji vinne vya Wilaya ya Makete viliwezesha kuanzisha ushirika wa wakulima wa miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi wa rasilimali za Misitu na Nyuki. Wizara iliendelea kudhibiti na kukagua mazao ya misitu katika kanda nane kwa kufanya doria 1,457 zikiwemo kanda tatu za mikoko katika ukanda wa bahari. Katika doria hizo, majahazi 39, vipande 31,736 vya mbao, vilingu 784; nguzo 6,115; mkaa magunia 14,150; magogo 998; Kilogramu 250 za vinyago; vitanda 45; slipa 280; milango 138; kuni zenye ujazo wa mita 238, misumeno saba; pampu nne za maji na baiskeli 66 vilikamatwa na kutaifishwa. Aidha, wahalifu 504 walikamatwa na kutozwa faini ya jumla ya shilingi 218,640,000.00 kwa kumiliki mazao ya misitu kinyume cha sheria na kesi 39 zilifikishwa Mahakamani. Kati ya hizo, kesi 25 zimekwisha na Serikali ilishinda, kesi tatu watuhumiwa wallachiwa huru na kesi 11 zinaendelea Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, operesheni za kuondoa wavamizi katika misitu iliyohifadhiwa zilifanyika kwenye misitu 16 ya hifadhi ya Goweko, Nyahua, Ipembampazi na Inyonga East Wilaya ya Sikonge; Mpanda-Line na Ulyankulu Wilaya ya Urambo; Ilomero Hill, Wilaya ya Nzega; Kigwa Rubuga Wilaya ya Uyui na msitu wa Mto Igombe uliopo Wilaya tatu za Uyui, Nzega na Urambo Mkoani Tabora. Aidha, wavamizi waliondolewa katika misitu ya Ruvu Kusini, Ruvu Kaskazini, Kazimzumbwi, Pugu, Masanganya na Mtita katika Mkao wa Pwani. Vilevile, katika Mkao wa Kilimanjaro operesheni ilifanyika katika Msitu wa Hifadhi Asilia wa Chome. Katika operesheni kwenye Msitu wa Chome, mbao 919, milango 350, madirisha 16, pampu saba za wachimbaji wa dhahabu, magunia ya mkaa 231, magari manne, kondoo 585 na ng'ombe 52 walikamatwa. Pia, matanuru 157 ya mkaa yaliyojengwa ndani ya hifadhi yaliharibiwa. Watuhumiwa 56 walihukumiwa kifungo cha kati ya miezi sita mpaka saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la uvamizi kwenye maeneo ya hifadhi ya mikoko, semina na mikutano mbalimbali zilifanyika kwa kuhusisha Wakuu wa taasisi zinazosimamia matumizi ya ardhi ya ukanda wa Pwani. Vilevile, mafunzo ya usimamizi wa Sheria na utunzaji wa kumbukumbu yalitolewa kwa washiriki 225 wa Kamati za Mazingira na Misitu. Pia, kiasi cha hekta 152 za mikoko zilipandwa kwenye Delta ya Rufiji na katika Mikoa ya Tanga na Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupima na kutathmini rasilimali za Misitu, jumla ya kilometra 221 za mipaka ya misitu ya hifadhi na mashamba ya miti ilifanyiwa soroveya. Misitu hiyo ni: Ruvu Kaskazini (km 0.4), Misitu wa Hifadhi wa Minziro (km 127), Misitu wa Marende (km 7.1), Misitu wa Hifadhi Loliondo (km 62.5) na Misitu wa Makerezange (km 9.1) na Shamba la Miti Mtibwa (km 11.9). Pia ramani ya Shamba la Miti Mtibwa ilichorwa. Aidha, Wizara iliendelea kuhudumia hifadhi nane za misitu ya Hifadhi Asilia ya Chome, Kilombero, Mkinga, Magamba, Nilo, Amani, Rungwe na Uluguru. Pia, ofisi tatu za Kilombero, Nilo na Uluguru zimejengwa. Vilevile, ujenzi wa nyumba mbili za watumishi na vituo viwili vya ulinzi wa misitu (*Rangers posts*) umefanyika katika Hifadhi Asilia ya Nilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunaji na udhibiti wa mazao ya misitu. Katika kuhakikisha uvunaji endelevu na udhibiti wa rasilimali za misitu, Wizara iliwezesha Wilaya 12 zenye Mpango wa Usimamizi wa Misitu kuendesha vikao vya uvunaji wa mazao ya misitu pamoja na kufanya doria kwenye misitu. Wilaya hizo ni Sikonge, Mpanda, Biharamulo, Kigoma, Chunya, Liwale, Sumbawanga, Nanyumbu, Rufiji, Kisarawe, Karagwe na Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuungeza nguvu ya kudhibiti uvunaji na usafirishaji haramu wa mazao ya misitu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Wizara iliendesha warsha moja iliyowahusisha Maafisa 51 wa Polisi katika Kanda ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kwa umma na uhamasishaji. Kanda za Uenezi zilifanya uhamasishaji jamii katika Wilaya 80 kuhusu upandaji miti wa biashara, ufugaji nyuki, kampeni ya moto, usimamizi shirikishi wa misitu na uanzishaji wa mashamba ya miti ya watu binafsi. Uhamasishaji ulifanyika kwa njia ya mikutano, maonesho na sinema. Aidha, uanzishwaji wa jumuiya ya vyama vya waoteshaji miti ulifanyika katika vijiji 17 vya Wilaya za Mbanga, Namtumbo, Songea na Liwale. Vilevile, kanda ziliandaa na kurusha vipindi 52 vya redio kuptitia redio za kanda na kuandaa makala 10 zilizochapishwa kwenye magazeti na majorida mbalimbali likiwamo 'MISITU NI MALI'. Aidha, jumla ya mikanda 76 ya video iliandaliwa kwa shughuli za ugani na jumla ya vipeperushi na vijarida 17,990 vyenye ujumbe mbalimbali vilisambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamasishaji wa ufugaji nyuki ulifanyika katika katika Wilaya nane (8) kama ifuatavyo: Geita - vijiji vitano (5); Kahama vijiji sita (6); Chunya vijiji vitano (5); Njombe vijiji vitano (5), Namtumbo vijiji 12, Rungwe vijiji 10, Ileje vijiji tisa (9) na Mpanda vijiji tisa (9). Vilevile, kanda ziliandaa mafunzo ya matumizi ya majiko banifu na jinsi ya kuyatengeneza kwa wananchi wa vijiji 17 vya Wilaya za Ksimba, Ukerewe na Moshi vijijini. Jumla ya kaya 2,790 zimejengewa majiko banifu 5,223, wananchi 53 na wataalam wa Wilaya 18 wamefundishwa kujenga majiko banifu ili kuifanya shughuli hii kuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni za kudhibiti moto zilifanyika katika Wilaya tano za Kilolo, Mufindi, Makete, Njombe na Ludewa na katika vijiji 21 vinavyozunguka Hifadhi Asilia Magamba.

Aidha, barabara za kuzuia moto na njia za watalii zenyenye urefu wa kilomita 102 kwenye Hifadhi Asilia za Magamba, Uluguru, Chome na Kilombero zilisafishwa. Elimu ya udhibiti wa moto kwa njia za sinema, video na machapisho ilitolewa. Pia, miche 5,000 ya miti ya aina mbalimbali ilipandwa katika Hifadhi Asilia Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki. Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya misitu na ufugaji nyuki katika vyuo vyake vitatu: Chuo cha Misitu Olmotonyi - Arusha, Chuo cha Viwanda vya Misitu – Moshi na Chuo cha Ufugaji Nyuki – Tabora. Mafunzo haya ni jitihada za kuhakikisha soko la ajira linakuwa na wataalam wa kutosha kuhudumia Sekta ya Misitu na Nyuki. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya Wakurufunzi 202 walidahiliwa kwa mwaka wa kwanza wa masomo kama ifuatavyo: Chuo cha Misitu Olmotonyi 147, Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi 21 na Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora 34. Hili ni ongezeko la asilimia 40 ukilinganisha na idadi ya wakurufunzi 112 walidahiliwa kwa mwaka 2009/2010. Pia, katika kipindi hicho jumla ya wakurufunzi 130 walihitimu katika taaluma ya misitu na ufugaji nyuki. Katika kipindi hicho mitaala ya Misitu na ya Ufugaji Nyuki ilipitiwa na kupatiwa ithibati na *NACTE*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Chuo cha Ufugaji Nyuki, Tabora kilianza rasmi kutoa mafunzo ya Ufugaji Nyuki kwa kozi ya Astashahada. Aidha, ukarabati wa majengo ya Chuo unaendelea ambapo hadi sasa mabweni mawili, nyumba tatu za wakufunzi zimefanyiwa ukarabati. Ujenzi wa jiko na bwalo unaendelea na utakamilika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Rasilimali za Misitu. Wizara inaendelea na zoezi la kuhesabu na kutathmini rasilimali za misitu kupitia mradi wa “*National Forest Resources Monitoring and Assessment- (NAFORMA)*” chini ya uhisani wa Serikali ya Finland na ushauri wa kitaalamu kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO). Tathmini imefanyika katika Mikoa ya Morogoro, Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Pwani, Mtwara na Ruvuma. Kazi ya kuhesabu na kutathmini miti inatekelezwa kwa muda wa miaka mitatu na itamalizika mwaka 2012. Tathmini hiyo itawezesha upatikanaji wa takwimu ambazo zitatumwiwa kuboresha Mipango ya Usimamizi wa Misitu na kutoa mchango ipasavyo katika masuala ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendeleza ufugaji nyuki. Wizara iliendelea kutunza na kuhudumia Hifadhi sita za Ufugaji Nyuki zenyenye hekta 5,225. Hifadhi hizo zina jumla ya makundi 400 ya nyuki katika Wilaya za Handeni 244, Manyoni 37, Kibondo 83 na Kondoa makundi 36. Aidha, katika kuongeza wingi na ubora wa mazao ya nyuki, Wizara imeendelea kutekeleza mpango wa kuboresha ufugaji nyuki katika Wilaya tisa kwa kuhamasisha ufugaji nyuki kwa wananchi 1,592. Uhamasishaji huo umefanyika katika Wilaya za Kahama wananchi 646, Geita 155, Bukombe 106, Kilombero 115, Ulanga 117, Longido 111, Monduli 174 na Lindi 168. Vilevile, jumla ya vikundi 39 vya ufugaji nyuki vimeanzishwa kwenye Wilaya za Bukombe, Geita na Kahama. Vikundi hivyo vilipewa mizinga 138 kama ifuatavyo; Bukombe 40, Geita 50 na Kahama 48. Pia, mizinga 477 imetengenezwa na inatarajwa kusambazwa katika Wilaya za Same, Kahama, Nachingwea, Tunduru, Mpanda, Sumbawanga na Lindi. Aidha, vifaa vya kinga viligawanywa katika Wilaya za Longido, Monduli na Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa maduhuli. Sekta ya Misitu na Nyuki pia inalo jukumu la kukusanya maduhuli ambapo hadi Mei, 2011 Wizara kupitia Sekta hii ilikusanya kiasi cha Shilingi 24,700,928,733.77 sawa na asilimia 63.4 ya lengo la Shilingi 38,958,900,000.00 zilizotarajiwaa kukusanya kwa mwaka 2010/2011. Pamoja na mambo mengine upungufu huo ulitokana na kupunguzwa kwa asilimia 30 ya ushuru wa mazao ya misitu yanayotokana na mashamba ya miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (*TFS*). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mchakato wa kuanzisha Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (*Tanzania Forest Service Agency*) umekamilika. Wakala huo umeanza kufanya kazi rasmi tangu tarehe 1 Julai, 2011. Madhumuni ya kuanzisha Wakala huu ni kuongeza ufanisi katika shughuli za uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki, kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya misitu na nyuki na ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Misitu Tanzania. Kama ilivyoahidiwa katika Bunge la mwaka jana, Wizara imeanzisha Mfuko wa Misitu (*Tanzania Forest Fund*) ambaa ulianza rasmi Julai,

2010. Makusanyo ya Mfuko yalianza Oktoba, 2010 na hadi kufikia Mei, 2011 jumla ya Shilingi 1,997,066,851.00 zilikusanya. Chanzo cha mapato ya Mfuko huu ni kutokana na asilimia tatu ya mapato yatokanayo na mrabaha (*royalty*), asilimia mbili ya tozo ya ushuru mbalimbali wa bidhaa za misitu na asilimia 100 ya faini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Misitu (TAFORI). Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) inalo jukumu la kutafiti na kusimamia tafiti mbalimbali katika sekta ya misitu na kuishauri Serikali. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Taasisi ilifanya na kusimamia utafiti wa mpango shirikishi wa kuendeleza misitu na utafiti kuhusu upatikanaji na mwenendo wa soko la mbaao nchini katika Mikoa ya Iringa, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAFORI kwa kushirikiana na taasisi za utafiti za Afrika Mashariki chini ya Jumuia ya Kimataifa ya Kuhifadhi na Kuongeza Ubora wa Miti (*Central American and Mexico Coniferous Resources – CAMCORE*) illendelea kufanya majoribio 81 ya mkaratusi aina ya *Eucalyptus pellita* kutoka nchi mbalimbali duniani. Ustawishaji wa miti hii utasaidia kuongeza miti bora ya kupandwa kwa ajili ya matumizi ya nguzo na mbaao ili kupunguza ukataji ovyo wa miti ya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi illendelea na utafiti juu ya bioteknolojia ya aina mbalimbali za kloni za miti ya mkaratusi (*Eucalyptus clones*). Majoribio 15 yamefanywa katika maeneo mbalimbali nchini. Miti hiyo inayokuwa haraka imeendelea kutunzwa katika bustani ya Kwamarukanga – Korogwe na kusambazwa kwa jamii. Aidha, taasisi imeanzisha bustani nyngine ndogo huko Mufindi na Kibaha kwa ajili ya kusogeza huduma ya upatikanaji wa miche na teknolojia karibu na wananchi katika maeneo na ukanda huo. Taasisi illendelea na ujenzi wa Ofisi na maabara kwa gharama ya shilingi bilioni 2.9 na ujenzi umekamilika kwa asilimia 96.

Mheshimiwa Naibu Spika, Akaunti Maalum ya Kuendeleza Mashamba ya Miti (*LMDA*). Akaunti ya *LMDA* (*Logging and Miscellaneous Deposit Account*) ilianzishwa kwa madhumuni ya kuimarisha usimamizi na kuhudumia mashamba ya miti. Hadi Mei 2011, mapato ya Akaunti yalifikia Shilingi 8,394,394,568.00 sawa na asilimia 109.9 ya makadirio ya mapato ya shilingi 7,638,127,658. Mapato hayo yalitokana na mauzo ya miti katika mashamba 13 kati ya 15 yenye miti iliyofikia umri wa kuvunwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala za Mbegu za Miti (*TTSA*). Madhumuni ya Wakala wa Mbegu nchini ni kuwezesha upatikanaji endelevu wa mazao ya misitu na utunzaji wa mazingira nchini kwa kuzalisha na kusambaza mbegu bora za miti pamoja na vipandikizi vingine. Wakala wa Mbegu za Miti uliendelea kuzalisha na kuuza mbegu na miche bora ya miti. Hadi kufikia Mei, 2011 kiasi cha mbegu za miti kilo 8,625 zenye thamani ya Shilingi 96,396,784.00 na miche 42,000 yenye thamani ya Shilingi 19,089,450.00 ilizwua nchini. Miche iliyouzwa kwa wingi ni mitiki, miembe, michungwa, mikangazi na mwalambe. Aidha, kiasi cha mbegu kilichokuwa katika maghala ya Wakala kilikuwa kilo 14,250 ambazo ni kwa ajili ya wateja wanaoagiza mbegu kwa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, aina za mbegu za miti zilizouzwa ni 83 na kati ya hizo, aina za miti ya asili ni 33 sawa na asilimia 40 ya mbegu zote na iliyosalia ni mbegu za miti ya kigeni. Mbegu zinazonunuliwa kwa wingi ni za Msindano, Mkangazi, Mtiki, Mwerezzi, Mkenge, Mgunga na Mkongo. Hadi Mei 2011, Wakala umesambaza nchini tani 12.2 za mbegu za miti pamoja na miche 45,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii. Utalii ni Sekta inayokua kwa kasi na mchangwo wake kwenye Pato la Taifa umekuwa ukiongezekwa kila mwaka. Sekta ya Utalii huchangia pia kuleta mapato ya fedha za kigeni nchini, kutoa ajira kwa Watanzania na kuhamasisha sekta nyngine kama kilimo na hivyo kukuza uchumi. Sekta hii inachangia asilimia 25 ya mapato ya fedha za Kigeni. Takwimu zinaonyesha kuwa shughuli za hoteli ambazo ni sehemu ya Sekta ya Utalii nchini zilikua kwa asilimia 6.1 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Sheria. Wizara imeanza mchakato wa kupitia upya Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 kwa lengo la kuboresha ili iendane na maendeleo ya utandawazi katika ngazi mbalimbali. Aidha, Kanuni za utalii zinaendelea kuboreshwa ili ziendane na mazingira ya sasa. Wizara ilitoa elimu kuhusu Sheria ya Utalii kwa wakala wa biashara za utalii

katika Mikoa ya Mara, Dar es Salaam, Pwani, Mtwara na Lindi. Wakala 167 walielimishwa kuhusu Sheria, Kanuni na taratibu za kuanzisha na kuendesha biashara za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mazao ya Utalii. Katika kuendeleza mazao ya utalii, Wizara imeelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu utalii wa kiutamaduni unaohusisha jamii. Elimu imetolewa kwa wanajamii kuhusu kuanzisha na kuendeleza utalii wa kiutamaduni katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Mbeya, Iringa, Pwani na Kilimanjaro. Aidha, idadi ya miradi ya Utalii wa kitamaduni imeongezeka kutoka 24 mwaka 2008 hadi kufikia miradi 34 mwaka 2010/2011. Vilevile, Wizara ilioa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo 51 katika Wilaya ya Bagamoyo ili kusaidia kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika biashara ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha ushirikiano kati ya Wizara na Sekta binafsi Mkataba wa Ushirikiano kati ya Wizara na Shirikisho la Vyama vya Utalii Tanzania ulisainiwa. Mkataba huu umeweka utaratibu wa mazungumzo kati ya Serikali na Sekta Binafsi kuhusu maendeleo ya sekta ya utalii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukuza utalii wa ndani, Wizara imeendelea kushiriki katika maonesho mbalimbali yanayofanyika nchini kama vile Saba Saba, Nane Nane na *Karibu Travel & Tourism Fair* ili kuelimisha na kuhamasisha Watanzania kutembelea vivutio vya utalii. Takriban wananchi 1,352,500 walielimishwa kuhusu Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya utalii. Wizara ilisambaza jumla ya nakala 6,000 za Sera ya Utalii, vipeperushi na vijarida mbali mbali vya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa huduma katika Sekta ya Utalii. Katika kuboresha huduma zinazotolewa na sekta ya utalii, Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa utoaji huduma za utalii katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mwanza, Mara, Lindi, Mtwara na Arusha. Pia, Mitaala mipy ya huduma na malaziimeandaliwa na kusambazwa katika Vyuo vya Utalii ambavyo vimesajiliwa na *NACTE*.

Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano ya ushirikiano ya kuwezesha mafunzo ya wataalam wa kuweka hoteli katika daraja yalisainiwa kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kupitia mradi wa *Capacity Building for Trade Development and Integration in Tanzania*. Katika makubaliano hayo, Wizara ilipewa shilingi milioni 133 kutoka mradi huo ambazo ziligharimia mafunzo ya wiki nane kwa wataalam 17 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa Maduhuli. Katika mwaka 2010/2011, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi 2,793,200,000 kutokana na leseni za wakala wa biashara za Utalii nchini. Hadi kufikia Mei, 2011 kiasi cha shilingi 2,981,449,641.40 sawa na asilimia 106.7 ya lengo kilikuwa kimekusanywa. Mafanikio haya katika ukusanyaji yametokana na kuimarika kwa usimamizi, kuongezeka kwa uwekezaji na uboreshaji wa huduma za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Utalii (TTB). Jukumu la Bodi ya Utalii ni kutangaza utalii ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2010/2011, Bodi iliendelea na jukumu lake kwa kushiriki katika maonesho, kuandaa na kusambaza vipeperushi, majarida na kutumia tovuti na televisheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu hilo mwaka 2010/2011, Bodi ya Utalii iliandaa na kusambaza nakala 36,000 za vipeperushi mbalimbali vya utalii katika lugha tisa za kimataifa ambazo ni Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa, Kijeruman, Kihispaniola, Kijapani, Kiitaliano, Kichina, na Kiarabu. Aidha, Bodi iliandaa na kusambaza ramani 25,000 zinazoonyesha vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo nchini, CD 24,000, DVD 1,600, nakala 18,000 za jarida la Selling Tanzania, nakala 2,800 za *Tanzania Conference Directory* na nakala 3,000 za *Tanzania Tourism and Travel Directory*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi pia imefanikiwa kuweka matangazo ya utalii kwenye viwanja sita vya Ligi Kuu ya Uingereza (*English Premier League*) na matangazo hayo yamerushwa rasmi kuanzia Agosti, 2010 na kufikia tamati Mei, 2011. Matangazo hayo yalionesha utalii wa fukwe, Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na mzunguko wa kuhama kwa nyumbu katika Hifadhi ya Taifa

Serengeti. Aidha, Takwimu za utafiti zinaonesha kuwa takriban watu bilioni mbili duniani waliweza kuona matangazo hayo kuititia ligi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi imeendelea kutangaza mazao na huduma za utalii katika maonesho ya utalii 14 ambayo yaliifanyika nchini Urosi, Kanada, Uingereza, Marekani, Italia, Ujerumani, Hispania, Ufaransa, Uhlanzi, Uturuki, Japani, Falme za Kiarabu na Ubelgiji. Katika maonesho hayo vipeperushi mbalimbali vya vivutio vya utalii vilisambazwa. Vilevile, Bodi iliwezesha misafara ya Waandishi wa Habari, Wakala 10 wa utalii kuja Tanzania kutembelea vivutio vya utalii kwa lengo la kuvitangaza. Kati ya hao, Wakala saba wa utalii walitoka kwenye masoko mapya ya Japani na India na watatu walitoka soko la Marekani. Vilevile, Bodi iliratibu msafara wa waendesha pikipiki maarufu ya *Harley Davidson Rally* uliohusisha washiriki 70 kutoka Ufaransa, Ubelgiji, Kanada na Israeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutangaza utalii wa ndani, Bodi ya Utalii imeendelea kudhamini matukio mbalimbali yaliyofanyika hapa nchini kama vile mbio za Kilimanjaro Marathon na Mlimbwende wa Utalii (*Miss Domestic Tourism*). Udhamini huo umesaidia kuhamasisha Watanzania kutembelea vivutio vya utalii. Aidha, Bodi inatumia wasanii wa muziki kuhamasisha utalii wa ndani kwa kutoa burudani inayoambatana na uulizaji maswali yanayohusu utalii pamoja na utoaji zawadi mbali mbali kwa washindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudzi za uendelezaji, utangazaji na uboreshaji wa huduma katika sekta ya utalii, mapato yatokanayo na sekta hii yameongezeka hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni 1.25 zilizopatikana kutoka kwa watalii 782,699 kuanzia Januari hadi Desemba mwaka 2010 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani bilioni 1.16 mwaka 2009 kutoka kwa watalii 714,367.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii (*NCT*). Katika mwaka 2010/2011, Chuo kiliendelea kutekeleza majukumu ya kutoa mafunzo katika fani ya ukarimu na utalii ili kuongeza ubora wa utoaji wa huduma katika Sekta ya Utalii. Jumla ya Wakurufunzi 321 walipatiwa mafunzo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Katika kuwajengea uwezo watumishi, Chuo kiliwezesha watumishi wanne kupata mafunzo ya Shahada ya Uzamili, wawili Stashahada na 26 mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala uliendelea kusimamia ujenzi wa kampasi mpya ya Chuo cha Taifa cha Utalii ambapo kazi za kufunga vifaa vya jikoni na kuagiza transfoma ili kuongeza kiwango cha umeme pamoja na jenereta zilifanyika. Kampasi hiyo inatarajiwa kuanza mafunzo Septemba, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Malikale. Sekta ya Malikale ina jukumu la kuhifadhi, kulinda, kutunza na kuendeleza Urithi wa Utamaduni wa Taifa. Aidha, Sekta hii inachangia katika kukuza utalii nchini kwa kuongeza idadi ya vivutio vikihusisha utalii wa kihistoria, makumbusho na malikale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Sheria. Katika kipindi cha 2010/2011, Wizara ilikamilisha kutafsiri Sera ya Malikale katika lugha ya Kiingereza ambapo nakala 1,000 za Sera hiyo zilichapishwa. Aidha, Wizara ilianda rasimu ya mkakati wa kutekeleza Sera hiyo kwa kuainisha maeneo muhimu ya utekelezaji. Wizara ilianza mchakato wa kuandaa Sheria ya Malikale kwa kuainisha upungufu katika Sheria Na. 10 ya mwaka 1964 na marekebisho yake Na. 22 ya mwaka 1979.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhifadhi wa Malikale. Katika kutambua na kuweka kumbukumbu za wapigania uhuru, Wizara iliendelea kuandaa orodha ya maeneo yaliyotumiwa na wapigania uhuru hapa nchini. Katika mwaka 2010/2011, Wizara ilikamilisha taarifa za maeneo 11 ya wapigania uhuru katika Mikoa ya Iringa na Mbeya. Katika Mkoo wa Iringa maeneo yaliyohusika ni Khesa, Mgagao (Wilaya ya Kilolo), nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa zilizotumiwa na FRELIMO, Mnara wa FRELIMO na jengo la Kikosi Maalum cha Wapigania Uhuru (*SDU-Special Duty Unit-Manispaa ya Iringa*). Katika Mkoo wa Mbeya maeneo yaliyohusika ni mabweni ya Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) katika Wilaya ya Mbalizi, Nyumba ya Samora

Machel, Shule ya Sekondari ya Samora Machel, Bwalo la Maafisa wa Jeshi Jiji la Mbeya na Kambi ya Mafunzo ya Itumbi Wilaya ya Chunya. Maeneo hayo yatajumuishwa katika Orodha ya Urithi wa Utamaduni wa Taifa na yanatambuliwa kuwa maeneo muhimu yalijotumiwa na wapigania uhuru Kusini mwa Afrika. Vilevile, Wizara imeandaa kanzi kwa ajili ya kuweka na kutunza kumbukumbu za malikale kwa njia ya kisasa ya elektroniki ili kuhakikisha kuwa rasilimali za malikale zinafahamika na kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika kuimarisha uhifadhi na matumizi endelevu ya vituo vya Malikale kwa mwaka 2010/2011, ilikamilisha michoro ya majengo ya kutolea taarifa yatakayojengwa kwenye vituo vya Mapango ya Amboni, Kimondo cha Mbozi, Makumbusho ya Kumbukizi ya Chifu Mkwawa, Kalenga, Engaruka na magofu ya Kilwa Kisiwani. Wizara inaendelea na ujenzi wa uzio katika Kituo cha Kumbukizi ya Dkt. Livingstone, Kigoma. Vilevile, Wizara iliendelea kutoa ushauri wa kitaalamu katika ukarabati wa Boma la Kijerumani Wilayani Bagamoyo pamoja na kuainisha gharama za huduma muhimu za maji na miundombinu katika Kituo cha Kwihiara, Tabora ambapo utekelezaji wake utaanza mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilianza kazi ya kufukua nyayo za zamadamu katika eneo la Laetoli liliopo katika hifadhi ya Ngorongoro-Arusha kwa kufukua eneo la mita 3.5 kati ya mita 27 za eneo lenye nyayo. Katika eneo liliofukuliwa zilipatikana nyayo nane zote zikiwa katika hali nzuri. Kufukuliwa kwa nyayo hizo kulikuwa na lengo la kuweka mikakati ya kuzihifadhi zikiwa wazi, kutoa fursa kwa wananchi kuona nyayo hizo na wanasayansi kuona aina ya mwamba wenye nyayo hizo na kutathmini masuala ya uhifadhi kabla ya kuzifukua nyayo zote kwa ujumla. Kwa kuzingatia kuwa nyayo hizi za Zamadamu zenye umri wa miaka milioni 3.6 ni za kipekee duniani katika historia ya mabadiliko ya mwanadamu; kufukuliwa kwake kunataraja kuongeza idadi ya watalii na mapato kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti na ugunduzi wa nyayo katika maeneo mbalimbali umeendelea na katika kipindi cha 2009/2010, nyayo nyingine zinazokadirwa kuwa na umri wa miaka 120,000 ziligungduliwa huko Engaresero karibu na Ziwa Natron, Wilayani Ngorongoro. Mwaka 2010/2011, nyayo nyingine ziligungduliwa katika eneo la Naiyobi, Ngorongoro mkoani Arusha. Kuendelea kugunduliwa nyayo zaidi, siyo tu kunaonyesha umuhimu wa eneo la Ngorongoro kihistoria bali pia umuhimu wa eneo hili kiutalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kwa umma. Wizara iliendelea kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa uhifadhi wa malikale kupitia vipindi vya radio na televisheni. Wizara iliandaa na kuendeleza kipindi cha Zamadamu kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC). Kupitia kipindi hicho, Wizara iliandaa vipindi 10 kuhusu urithi wa utamaduni kutoka Mkoa wa Iringa. Maeneo yaliyohusika ni Kituo cha Kalenga kwa ajili ya historia ya Chifu Mkwawa na Utawala wake; Kaburi la Nyundo, Mnara wa Kumbukumbu ya Askari wa Kijerumani waliokufa wakati wa vita kati ya Wajerumani na Wahehe wakiongozwa na Chifu Mkwawa eneo la Lugalo, Iringa; Mapango ya Magubike na Bonde la Isimila kuhusiana na chimbuko la mwanadamu na matumizi ya zana za mawe.

Aidha, nakala 2,000 za kitabu cha Urithi wa Utamaduni kwenye Njia ya Kati ya Biashara ya Utumwa na Vipusa (*Tanzania Cultural Heritage Along the Central Slave Route*) zilichapishwa kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusu malikale zilizopo kwenye njia ya kati ya Biashara ya watumwa na vipusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilishiriki katika uzinduzi wa mnara wa mashujaa wa vita vya majimaji uliofanyika tarehe 16 Agosti, 2010, katika Kijiji cha Nandete, Kilwa Kipatimu, Mkoa wa Lindi. Kupitia uzinduzi huo, Mnara wa Kumbukumbu wa Mashujaa wa vita ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, tarehe 25 hadi 27 Februari, 2011, Maadhimisho ya Mashujaa wa Vita vya Majimaji yalifanyika katika Mkoa wa Ruvuma ambapo Mnara wa Kumbukumbu za Mashujaa wa Vita vya Majimaji mjini Songea ulizunduliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa maeneo ya urithi wa Dunia. Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa UNESCO wa mwaka 1972 unaohusu Uhifadhi na Ulinzi wa Urithi wa

Dunia wa Asili na wa Utamaduni. Mkataba huo uliidihiishwa na Mkutano Mkuu wa UNESCO uliofanyika Paris Ufaransa mwaka 1972. Tanzania iliridhia Mkataba huo mwaka 1977. Kutokana na mwongozo wa utekelezaji wa Mkataba huo, Tanzania imefanikiwa kupewa heshima ya kuwa na maeneo saba kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo hayo ni Hifadhi ya Taifa Serengeti, Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro, Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara, Pori la Akiba Selous, Michoro ya Miambani Kondoa na Hifadhi ya Mji Mkongwe Zanzibar. Maeneo hayo yanazo sifa za pekee duniani na hayafanani na maeneo mengine kwa umuhimu na ubora wake hapa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka Tanzania imekuwa ikihudhuria mikutano ya Kamati ya Urithi wa Dunia ili kushiriki katika kuelezea hali ya uhifadhi wa maeneo ya urithi wa dunia, changamoto za kiuhifadhi na kuwasilisha maombi ya kuongeza au kupunguza idadi, wigo au ukubwa wa maeneo kwenye orodha hiyo kwa mujibu wa vigezo. Mwaka 2010/2011, Wizara imeshiriki kwenye mkutano huo mara mbili, mikutano hiyo ilifanyika Brasilia, Brazil Julai hadi Agosti, 2010 na Paris, Ufaransa Juni, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa 34 wa Kamati ya Urithi wa Dunia uliofanyika Brasilia, Brazil, Wizara iliwasilisha ombi na kukubaliwa kwa Hifadhi ya Urithi wa Dunia ya Ngorongoro kuwa hifadhi ya urithi mchanganyiko (*natural and cultural mixed site*). Hatua hii inalifanya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kuwa hifadhi ya urithi asilia na wa utamaduni, hivyo kuvutia watalii wengi zaidi. Wizara inaandaa utaratibu wa kuwezesha maeneo ya malikale yaliyopo kwenye eneo la hifadhi kuwa katika usimamizi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa 35 wa Kamati ya Urithi wa Dunia uliofanyika Paris, Ufaransa pamoja na mambo mengine, Tanzania ilikwenda kutoa maelezo ya kina kuhusu hoja ya ujenzi wa barabara ya kukatisha Hifadhi ya Taifa Serengeti. Aidha, wajumbe walikwenda kutetea ombi la Tanzania la kufanya mabadiliko madogo ya mpaka wa eneo la Urithi wa dunia katika Pori la Akiba Selous. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa maelezo ya Tanzania kwa maeneo yote mawili yameeleweka vizuri na Kamati ya Urithi wa Dunia imeahidi kuwa itaendelea kushirikiana na Tanzania ili kuhakikisha kuwa mipango yetu ya maendeleo inayotekeliza kwenye maeneo yaliyoko kwenye urithi wa dunia inatekelezwa kwa uangalifu mkubwa bila kuathiri sifa za upekee za maeneo hayo (*outstanding universal value*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia utafiti wa muda mrefu na kugundulika kwa madini ya Urani katika eneo la Mto Mkulu katika Pori la Akiba Selous, Serikali ilianza mchakato wa kuruhusu wawekezaji walikuwa wakifanya utafiti huo kuchimba madini hayo. Pamoja na Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 kuruhusu uchimbaji wa madini ya urani, gesi na mafuta (Kifungu Na. 20(3)) katika Mapori ya Akiba, uchimbaji madini hauruhusiwi katika maeneo ya urithi wa dunia. Hivyo, Serikali ilipeleka ombi UNESCO la kufanya mabadiliko ya mpaka kwa kuondoa eneo la km² 345 katika ya km² 50,000 sawa na asilimia 0.69 ya Pori zima la Selous ili kuruhusu uchimbaji ufanyike nje ya eneo la urithi wa dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida za maeneo yetu kuorodheshwa kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia ni pamoja na urahisi wa kuyatangaza na hivyo kuwavutia watalii. Aidha, kuititia UNESCO na Mashirika mengine ya uhifadhi duniani, maeneo hayo hopata misaada ya kifedha na utaalamu katika kuyahifadhi na kuyaendeleza. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na UNESCO ilitoa mafunzo kwa Wakuu wa Vituo 10 vilivypo kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia hapa nchini; mafunzo kwa wananchi wa Kilwa kuhusu manufaa ya maeneo ya urithi wa dunia na ukarabati wa magofu ya Kasri ya Makutani, Kilwa Kisiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii wa ndani na ukusanyaji maduhuli. Kwa kutambua umuhimu wa kukuza utalii katika kuinua Pato la Taifa, Wizara iliendelea kuhamasisha Watanzania kutembelea maeneo yenye vivutio vya malikale. Hadi kufikia Mei 2011, idadi ya watalii ilifikia 104,362 ikilinganishwa na Mei, 2010 ambapo watalii 103,777 walitembelea maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliweka lengo la kukusanya shilingi 327,400,000.00 kutoka Sekta ya Malikale. Hadi Mei, 2011 shilingi 221,402,267.18 zilikusanya ikiwa ni asilimia 67.6 ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa (*NMT*). Shirika la Makumbusho ya Taifa limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutafiti, kuhifadhi, kutunza na kuelimisha Umma kuhusu urithi wa Taifa. Shirika limeanza mchakato wa kupanua Makumbusho ya Azimio la Arusha ili yawe endelevu na kuonyesha historia pana ya mageuzi ya kisiasa na kiuchumi nchini. Katika mwaka 2010/2011, Shirika limeandaa andiko la mradi wa kujenga jengo pembedi mwa jengo la kihistoria liliopo sasa Jijini Dar es Salaam bila kuathiri mandhari yake. Sambamba na ujenzi huo unaofanyika Dar es Salaam, Shirika pia limepata kiwanja katika Jiji la Arusha kwa ajili ya ujenzi wa Makumbusho ya Elimu Viumbe Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano na Serikali ya Sweden imekamilisha ujenzi wa Nyumba ya Utamaduni Jijini Dar es Salaam. Nyumba hiyo itazinduliwa wakati wa kilele cha Maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara Desemba, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika katika kuhakikisha kuwa Watanzania wanafahamu historia ya Tanzania, limeanzisha programu maalum ya kuelimisha na kuhamasisha wanafunzi na watu wazima kutembelea Makumbusho ya Taifa. Hadi Mei, 2011 ziara za kuhamasisha wanafunzi zilifanyika kwenye shule 74 katika Mikoa ya Arusha, Ruvuma, Mara na Dar es Salaam. Aidha, watalii waliendelea kuhamasika na kutembelea Makumbusho ya Taifa ili kuju historia ya Tanzania. Hadi Mei, 2011 idadi ya watalii walitembelea Makumbusho ya Taifa ilikuwa ni 83,918 ikilanganishwa na watalii 69,711 kwa kipindi kama hicho mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha kularifu Bunge lako Tukufu kuwa juhudzi za kurejesha urithi wa nchi yetu uliokuwa katika Makumbusho ya Taifa la Kenya ziliendelea. Urithi huo unahuishisa masalia ya wanyama wa kale na zana za muhula wa mawe. Hadi kuflikia Juni, 2011 Serikali imerejesha asilimia 90 ya urithi huo. Sehemu iliyobaki itarejeshwa mwaka 2011/2012. Aidha, Shirika limepokea Sarafu 1,446 kutoka *British Institute of Archaeology in East Africa* (Nairobi - Kenya), zilizotumika kuanzia karne ya 10. Sarafu hizi zikiwemo sarafu maarufu za Kilwa, zimesaidia kueleza historia ya maendeleo ya Miji ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala na rasilimali watu. Wizara katika kipindi cha mwaka 2010/2011, imeendelea kusimamia masuala ya watumishi katika maeneo ya ajira, utendaji kazi, nidhamu, mafunzo, maslahi ya watumishi, utawala bora, ustawi wa afya kwa watumishi wote pamoja na kusimamia masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya Watumishi. Wizara ilitarajia kuajiri watumishi wapya 260 na kujaza nafasi zilizoachwa wazi pamoja na kupandisha vyeo watumishi 265 wa kada mbalimbali. Katika kipindi hicho, jumla ya watumishi 265 walipandishwa vyeo na 84 walithibitishwa kazini. Aidha, nafasi za ajira mpya na zilizoachwa wazi hazikujazwa kwa kuwa Serikali ilisitisha zoezi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilikamilisha uandaaji wa Mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia majalada (*file tracking system*) ikiwa ni hatua ya kuboresha masjala ya Wizara. Aidha, watumishi 24 waliwezeshwa kushiriki mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuona umuhimu wa kuwajengea watumishi uwezo wa kielimu na kuboresha utendaji kazi, kwa mwaka 2010/2011, Wizara iliwezesha watumishi 189 kuhudhuria mafunzo ambapo watumishi 44 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na 145 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu. Aidha, Wizara ilifanya zoezi la uhakiki kwa watumishi wote 3,415 kwa lengo la kuboresha mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za kiutumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2010/2011, watumishi 55 walishiriki michezo ya Mei Mosi iliyofanyika Mkoani Morogoro ikiwa na lengo la kuboresha afya na kuimarisha uhusiano na watumishi wengine. Vilevile, Wizara iliendelea kutoa huduma kwa watumishi walioathirika na Virusi

vya Ukimwi na kuhamasisha watumishi kupima kwa hiari ili kujua afya zao. Hadi sasa, watumishi 41 wamejitokeza kuwa wanaishi na Virusi vya Ukimwi na wanawezeshwa kupata lishe bora na virutubisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha utendaji kazi, mwaka 2010/2011, Wizara ilifanya mukutano wa Baraza la Wafanyakazi uliohudhuriwa na wajumbe 70 ambapo hoja mbalimbali za watumishi zilijadiliwa na maazimio ya utekelezaji kufikiwa. Wizara ilifanya Mkutano wa Watendaji wake Wakuu ulioshirikisha wajumbe 100 ambapo maazimio ya kuongeza tija na ufanisi yalipitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto katika utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2010/2011. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kukosekana kwa watumishi wa kutosha kushughulikia utekelezaji wa programu zake hususan katika Idara za Wanyamapori na Misitu na Nyuki.
- (ii) Uvunaji haramu na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za maliasili na malikale na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa.
- (iii) Ushiriki usioridhisha wa wadau katika kuhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili, malikale na vivutio vya utalii.
- (iv) Ufinyu wa bajeti ya Wizara, hivyo kutokidhi utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa na dharura za uhifadhi.
- (v) Fedha za Miradi ya Maendeleo kutopatikana kwa wakati.
- (vi) Kuwepo kwa mwamko mdogo wa Watanzania kutembelea vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyininge kubwa ni kuwepo kwa matukio ya uvunjaji wa Sheria ya Wanyamapori Na.5 ya 2009 kuhusu ukamataji na biashara ya kusafirisha wanyama hai. Katika kipindi hiki, tukio mojawapo kubwa lilihusisha utoroshaji wa wanyama hai wa aina mbalimbali wapatao 120 na ndege hai 16 usiku wa tarehe 26 Novemba, 2010 kutokea Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. Kufuatia tukio hilo watuhumiwa sita wamekamatwa na kufunguliwa mashtaka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia tukio hilo, pamoja na kukamatwa kwa watuhumiwa na kufunguliwa mashtaka, Wizara imechukua hatua nyininge za haraka zifuatazo:-

- (i) Kusitisha leseni kwa wafanyabiashara wanaotuhumiwa;
- (ii) Kuimarisha ukaguzi katika uwanja wa ndege wa *KIA* kwa kuweka Askari Wanyamapori muda wote;
- (iii) Kuweka kituo cha kudumu cha Askari Wanyamapori kwenye uwanja wa *KIA*;
- (iv) Kuimarisha ushirikiano na Askari Polisi, Uhamaaji na Forodha kwenye vituo vyote vya kutokea nchini vya mipakani, bandarini na viwanja vya ndege;
- (v) Kuimarisha Kitengo cha Intelijensia; na
- (vi) Kuimarisha Kikosi Dhidi Ujangili Kanda ya Kaskazini, Arusha kwa kuongeza vitendea kazi, watumishi na kufanya mabadiliko kwa baadhi ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na upelelezi wa Kipolisi kwa ajili ya kesi iliyoko Mahakmani, vyombo vya ulinzi na usalama vinafanya uchunguzi ndani na nje ya nchi ikihusisha pia vyombo vya ushirikiano wa ulinzi wa maliasili vya *CITES* na *LATF* (*Lusaka Agreement Task Force*).

Uchunguzi huo unakusudia pia kujiridhisha kama kuna ushiriki wa watumishi wa Wizara. Aidha, Wizara imeunda 'Task Force' ya kukagua mazizi yote ya kuhifadhi wanyamapori na ndege wanaosubiri kusafirishwa yanayomilikiwa na wafanyabiashara wote 180 wenye leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za kukabiliana na changamoto nyingine katika Wizara zimechukuliwa zikiwemo:-

- (i) Kuboresha ukusanyaaji wa maduhuli, kupitia viwango vya sasa veya tozo na vyanzo vipyta;
- (ii) Kuongeza ushirikishaji wa wadau mbalimbali katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili, malikale na shughuli za utalii;
- (iii) Kuendelea kuongeza ajira kwa watumishi wapya kulingana na bajeti na upatikanaji wa nafasi za ajira;
- (iv) Kuongeza bajeti ya ulinzi, uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za maliasili na malikale;
- (v) Kuhamasisha jamii kutembelea vivutio veya utalii ili kukuza utalii wa ndani; na
- (vi) Kuanzisha Wakala wa Huduma za Misitu na Mfuko wa Misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa utekelezaji na malengo kwa mwaka 2011/2012. Sekta ya Wanyamapori. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kukamilisha Kanuni sita za kutekeleza Sheria Na.5 ya mwaka 2009 ya Kuhifadhi Wanyamapori. Kanuni zitakazohusika ni: Uanzishaji na Usimamizi wa Mashamba na Bustani za wanyamapori; Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori; Matumizi ya Wanyamapori yasiyo ya Uvunaji na utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyoko katika hatari ya kutoweka-CITES. Aidha, Kanuni za Uchimbaji wa Madini katika Mapori ya Akiba na Tengefu na Utendaji kazi wa Kikosi Dhidi Ujangili zitakamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori kwa kuendesha siku za doria 100,000 dhidi ya majangili na siku 3,000 za msako wa wanyamapori wakali na waharibifu, kununua vitendea kazi hususan helikopta moja, kuweka mfumo wa *satellite* wa kufuatilia mienendo ya wahalifu katika hifadhi, magari 10, mahema 50, *GPS* 200 na sare za watumishi 3,000. Vilevile, Wizara itajenga vituo veya doria Nangurukuru na Pori la Akiba Mkungunero. Sanjari na kazi hizo, Wizara itakamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Kanda katika Pori la Akiba Kigosi, Kanda ya Kalulu katika Pori la Akiba Selous na kujenga nyumba mbili za watumishi katika Mapori ya Akiba Rungwa na Liparamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza miundombinu ndani ya Mapori ya Akiba, Wizara itatengeneza barabara zenye urefu wa kilomita 300, kukarabati kilomita 320 na kusafisha kilomita 200 za mipaka katika Mapori ya Akiba. Vilevile, itaendelea na ukarabati wa viwanja veya ndege 15 ndani ya Mapori ya Akiba; kukamilisha maboresho ya mtandao wa kusambaza maji katika Pori la Akiba Selous Kanda ya Matambwe na kujenga bwawa la maji katika Pori la Akiba Rungwa. Aidha, Wizara itaandaa Mpango ya Jumla ya Usimamizi wa Mapori ya Akiba Ugalla, Moyowosi-Kigosi na Mpanga-Kipengele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia maeneo manne yaliyotengwa kuwa Ardhioevu zenye hadhi ya Kimataifa. Vilevile, Wizara itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI kukamilisha Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika vijiji sita vinavyozunguka Ziwa Natron Wilayani Longido na Ngorongoro. Aidha, Wizara itajenga nyumba moja katika eneo la Ramsar la Ziwa Natron.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanwanufaika na rasilimali za wanyamapori, Wizara itaendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika kuhifadhi wanyamapori kwa kupanua wigo wa faida zitokanazo na rasilimali hizo. Wizara itawezesha uanzishaji wa WMA mbili katika maeneo ya Yaeda Chini Wilayani Mbulu na Kilindi. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa

asilimia 25 ya fedha zitokanazo na uwindaji wa kitalii katika Halmashauri za Wilaya zenyе vitalu vya uwindaji na Jumuiya za Jamii zilizoidhinishwa (*Authorized Association – AA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011/2012, Vyuo vya Taaluma ya Wanyamapori vitadahili Wakurufunzi 784 na Askari Wanyamapori wa Vijiji 200 kama ifuatavyo: Mweka 500, Pasiansi 284 na Likuyu Sekamaganga 200. Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi kitaendelea kuboresha miundombinu kwa kujenga darasa moja, maabara moja na mabweni mawili pamoja na kukarabati nyumba za watumishi. Kituo cha Likuyu Sekamaganga, kitaimarisha mafunzo kwa kuongeza idadi ya Askari Wanyamapori wa Vijiji watakaopatiwa mafunzo kutoka 137 mwaka 2010/2011, hadi 200 na kuanza kozi mpya ya uongozaji watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, baada ya kupata ithibati ya mitaala kutoka NACTE, kinatarajia kuanza mafunzo ya Shahada ya Usimamizi wa Wanyamapori (*Wildlife Management*) na Shahada ya Utalii wa Wanyamapori (*Wildlife Tourism*) ifikapo Oktoba 2011. Aidha, Chuo kitaendelea kuboresha maabara, “*taxidermy*” na “*herbarium*” na kununua vifaa vya mafunzo ikiwa ni pamoja na magari matatu ili kuboresha mafunzo kwa vitendo. Katika kipindi hicho, Chuo kitawezesha wakufunzi sita kuhudhuria mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*) na Wakufunzi wawili mafunzo ya Shahada ya Uzamili (*MSc*). Vilevile, Chuo kitawawezesha watumishi wanne wasio Wakufunzi kushiriki mafunzo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*). Katika mwaka 2011/2012, Shirika litaendelea kuimarisha uwezo wa Idara ya Himasheria kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa na nyenzo muhimu ikiwemo utumiaji wa helikopta na mbwa maalum. Katika kutekeleza azma hii, Shirika litajenga vituo 26 vya Askari, kuajiri Askari 120 pamoja na kununua magari 34. Aidha, Shirika litaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Maaskari na Maafisa pamoja na kushiriki warsha na semina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za ufuatiliaji wa mabadiliko ya mazingira ndani na nje ya hifadhi na kuchimba mabwawa kwa ajili ya wanyamapori. Vilevile, Shirika litaendelea kuidadi wanyamaporii katika Hifadhi zake ambapo kwa mwaka 2011/2012, kazi hiyo itafanya katika Hifadhi za Tarangire, Manyara na Mikumi. Pia, Shirika litaendelea kufuatilia afya za wanyama na kudhibiti milipuko ya magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza utalii, Shirika litaendelea kupanua wigo wa shughuli za utalii hasa katika eneo la Hifadhi za Kusini kama vile utalii wa safari za puto, utalii wa usiku katika Hifadhi za Mikumi, Ruaha na baadaye Katavi ili kuvutia wageni wengi zaidi. Aidha, Shirika litaendelea kuratibu shughuli za wawekezaji kwenye hifadhi pamoja na kuelekeza jitihada katika kuendeleza utalii wa ndani, utalii wa kiikoloja na kiutamaduni kwa kushirikiana na jamii zinazozunguka hifadhi pamoja na utangazaji wa vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi. Aidha, Shirika litashiriki katika maonesho 25 nje ya nchi na matatu ndani ya nchi ambayo ni Sabasaba, Nanenane na Karibu Fair. Matarajio kwa mwaka 2011/2012, ni kutembelewa na watalii 889,920 na kuingiza mapato ya shilingi 141,062,553,040.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika litaendelea kutoa elimu ya uhifadhi kwa kutumia njia mbalimbali kama vile majarida, mikutano ya hadhara na wanavijiji, kutoa elimu katika shule za msingi, ziara za waandishi wa habari na vipindi vya radio na televisheni. Aidha, Shirika litaendelea na utaratibu wa kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kuongeza bajeti ya kugharimia miradi ya ujirani mwema kutoka shilingi 550,046,559.00 mwaka 2010/2011 hadi shilingi 744,244,212.00. Vilevile, Shirika litahuisha taratibu na vigezo vya uchangiaji na uibuaji wa miradi ya ujirani mwema ili kuondoa upungufu uliojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika litaendelea kuimarisha miundombinu katika Hifadhi zake kwa kufanya matengenezo ya kawaida ya jumla ya Kilometra 3,200 za barabara na kujenga madaraja manne katika Hifadhi za Ruaha, Tarangire na Serengeti. Katika kuboresha makazi ya watumishi, Shirika limepanga kujenga nyumba 30. Aidha, Shirika litakamilisha mapitio ya Mipango Kabambe ya Hifadhi za Ziwa Manyara, Arusha na Tarangire. Kwa kutambua migogoro ya mipaka, Shirika limeunda Kitengo Maalum cha kushughulikia migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA). Katika kuimarisha na kuboresha miundombinu na makazi ya watumishi, mwaka 2011/2012, mamlaka itaendelea na matengenezo ya barabara ndani ya eneo la Hifadhi zenyet urefu wa jumla ya kilometra 420, kununua tingatinga (*bulldozer*) moja kwa ajili ya ujenzi wa barabara na kujenga nyumba mbili za ghorofa kwa ajili ya familia 12 za watumishi. Vilevile, katika kuongeza vyanzo vya mapato Mamlaka itaandaa michoro kwa ajili ya kujenga kitega uchumi Mjini Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka itaendelea kutekeleza miradi ya ujirani mwema kwa kukamilisha ujenzi wa madarasa matatu katika Shule ya Msingi Jema Ilyoko Oldonyo Sambu. Aidha, mamlaka itafanya ukarabati wa majosho, itatekeleza mradi wa kuboresha mifugo na ujenzi wa mabwawa matatu kwa ajili ya mifugo katika eneo la Ngairishi. Miradi mingine mikubwa itakayotekelawa ni mradi wa uboreshaji wa mifugo ya wenyeji katika vijiji vyote 17 ndani ya Hifadhi. Hii itajumuisha ujenzi wa majosho 17, usambazaji wa madume bora na uhamilishaji, kutoa chanjo, kuchimba mabwawa na kuboresha malisho. Aidha, mamlaka itaendelea kusimamia mfuko wa kutoa chakula kwa wenyeji kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI). Katika mwaka 2011/2012, Taasisi itafanya sensa ya wanyamapori katika Mapori ya Akiba hususan Tembo kwenye Pori la Akiba Selous na mamba kwa nchi nzima. Taasisi pia itaendelea na utafiti wa mwenendo wa magonjwa ya wanyamapori hasa ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa pamoja na kuendelea na utafiti wa mbwa mwitu katika Hifadhi za Serengeti na Wilaya ya Ngorongoro (Loliondo). Aidha, Taasisi itakamilisha na kuanza kutekeleza Mpango wa Utekelezaji wa Kuhifadhi Wanyama Wanyonyeshao nchini (*Conservation Action Plan for Mammals in Tanzania*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi kupitia Kituo cha Utafiti wa Nyuki Njiro itafanya tafiti juu ya nyuki wasiouma katika maeneo muhimu ya ufugaji nyuki; kuendelea na utafiti kuhusu Kupe aina ya *Varroa destructor* amba walipatikana kwenye Wilaya 25 katika Mikoa 12 ya Tanzania Bara. Utafiti itaendelea kufanya katika Mikoa mingine Ilyobaki. Vilevile, Taasisi itaendelea na utafiti kuhusu mahusiano kati ya nyuki na mimea katika kanda zote za Tanzania Bara ili kuwezesha uchoraji wa ramani kulingana na aina za mimea, nyuki, asali na chavua katika maeneo husika. Aidha, Taasisi itaandaa michoro ya jengo la maabara ya utafiti wa nyuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Misitu na Nyuk. Katika kutekeleza majukumu na mpango kazi wa mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kupitia na kuboresha Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu pamoja na Programu za Misitu na Nyuki ili ziendane na wakati. Wizara itafanya tafsiri ya Kanuni za Misitu na Nyuki kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili na kusambaza nakala 4,500 kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza wingi na ubora wa mazao ya nyuki, Wizara itaendeleza ufugaji nyuki kwenye Wilaya 30. Katika kuhakiki na kudhibiti viwango vya ubora wa mazao ya nyuki katika Soko la nchi za Ulaya, Wizara itakusanya sampuli 55 za asali ikiwa ndio idadi ya chini inayokubalika kulingana na kiwango cha uzalishaji nchini kwa ajili ya uchambuzi wa kemikali. Pia, itaendelea kuzipatia kaya 1,500 teknolojia sahihi ya ufugaji nyuki na matumizi bora ya nishati itokanayo na miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itaongeza uhamasishaji wa jamii kushiriki katika masuala ya misitu na ufugaji nyuki ambapo itatao elimu ya utunzaji na matumizi bora ya rasilimali za misitu na nyuki kwa kufanya huduma za ugani na kusambaza majarida na vipeperushi. Jumla ya nakala 6,000 za majarida, vipeperushi, Sera na Kanuni zitachapishwa na kusambazwa kwa wadau. Aidha, vipindi 39 vya redio vinavyotoa elimu ya uhifadhi wa misitu, upandaji miti, kupambana na moto na ufugaji nyuki vitarushwa hewani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Misitu na Ufugaji Nyuki vinatarajia kudahili jumla ya Wakurufunzi 244 katika mwaka 2011/2012 kama ifuatavyo: Chuo cha Misitu Olmotonyi 164; Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi 25 na Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora 55. Aidha, Wizara itaendelea

kuwezesha Vyuo vya Misitu na Ufugaji Nyuki vilivyopo chini yake kutekeleza majukumu yao. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuwezesha ujenzi wa maktaba katika Chuo cha Viwanda vya Misitu – Moshi na kuendelea kukamilisha ujenzi wa bwalo la chakula na ukarabati wa baadhi ya majengo ya Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Huduma za Misitu (*TFS*). Katika mwaka 2011/2012, Wakala wa Misitu Tanzania utaandaa mipango ya usimamizi wa hekta milioni 1.36 za misitu ya hifadhi ya uzalishaji (Misitu ya Asili na Mashamba 16 ya miti ya kupanda) kufuatana na mipango kazi iliyopitishwa. Aidha, miche 10,051,000 ya aina mbalimbali za miti itakuzwa na kupandwa katika hekta 7,900 za mashamba. Vilevile, katika kuongeza wingi na ubora wa mazao ya nyuki, Wakala utaimarisha vituo vinne vya mashamba ya mfano kwa kuviongezea mizinga 5,000, kuanzisha manzuki 12 zenye jumla ya mizinga 200 kwenye maeneo mbalimbali na kutoa elimu ya ufugaji nyuki kwa vijiji 60 vinavyozunguka Hifadhi za Taifa za Misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka na barabara za kuzuia moto zenye urefu wa kilometa 4,700.8 pamoja na barabara zinazotumika ndani ya misitu zenye urefu wa kilometa 2,311.5 zitakarabatiwa. Aidha, Wakala utajenga majengo 14 kwenye mashamba ya miti ya Sao Hill (tisa), Rubare (moja), Buhindi (moja), Matogoro (moja), Mtibwa (moja) na Rondo (moja). Vilevile, Wakala utakarabati jumla ya majengo 165, ikiwa ni nyumba 154 za watumishi katika mashamba 15 ya miti na vituo vinne vya nyuki pamoja na ofisi saba za kanda. Wakala pia utaimarisha mifumo ya kukusanya maduhuli yatokanayo na mazao ya Misitu na Nyuki ili kufikia lengo la shilingi bilioni 38.9 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha usimamizi wa misitu ya hifadhi nchini yenye hekta milioni 1.8, Wakala utafanya tathmini kwenye Mikoa 10 ili kuhakiki mipaka, kuchora ramani na kutayarisha mipango ya usimamizi. Aidha, kwa kuanzia hifadhi zitakazohakikiwa zitapangiwa mameneja ili kuimarisha usimamizi. Vilevile, Wakala umepanga kuondoa wavamizi wa misitu ya hifadhi katika Mikoa tisa na kanda tatu za mikoko. Wakala pia, utaimarisha usimamizi na udhibiti wa biashara ya mazao ya misitu na nyuki kwa kuanzisha vikosi vidogo katika Mikoa miwili na Wilaya nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza ufanisi na tija katika utendaji kazi, Wakala utanunua vitendea kazi muhimu ambavyo vitatumika katika kukusanya maduhuli, kufanya doria na kutoa elimu kwa wafugaji nyuki vijijini. Vifaa vitakavyonunuliwa ni magari manne, pikipiki 48, kompyuta 50, vifaa vya kupima ubora wa asali, mavazi ya kinga, sare, mahema na magodoro. Aidha, Wakala utaainisha mahitaji ya watumishi na kuwasilisha maombi ya ajira mpya ili kuboresha utendaji. Katika kuhakikisha kuwa jamii na wadau mbalimbali wa misitu wanaoshiriki kusimamia misitu ya hifadhi ya Serikali Kuu wananaufaika, Wizara itapitia upya "Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu wa Pamoja". Aidha, Wizara itaweka utaratibu mzuri wa jinsi watakavyonufaika kwa kubainisha kiwango cha mgawanyo wa kazi na mapato yatokanayo na ushiriki wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Misitu Tanzania. Katika Mpango Kazi wa mwaka 2011/2012, Mfuko wa Misitu Tanzania umetenga takribani Shilingi 500,000,000.00 kuwezesha jamii katika Wilaya 10 kuanzisha na kusimamia misitu ya hifadhi ya vijiji; kuanzisha na kuendesha miradi midogo ya jamii ambayo ni rafiki wa mazingira pamoja na uanzishaji wa vitalu vya miti na upandaji miti katika mashamba ya vikundi na watu binafsi. Miongoni mwa watakaonufaika na Mfuko huu ni Jamii katika ngazi za Wilaya na vijiji, watu binafsi, vikundi vya jamii na Asasi za uhifadhi na utafiti wa misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, misitu ina mchango mkubwa katika kuondoa gesiukaa (*carbon dioxide*) katika hewa. Ili kupunguza kasi ya kutoweka na kuharibika kwa misitu ambayo ndio chanzo cha kuongezeka gesiukaa, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) inaandaa Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji Gesiukaa kutokana na kutoweka na kuharibika Misitu (MKUGUMI). Utekelezaji wa Mkakati huo utaimarisha utunzaji wa misitu kutokana na biashara ya gesiukaa. Biashara hii pia itawezesha wananchi kufaidika na mapato yatakayopatikana hivyo kuimarisha utunzaji wa misitu ya asili pamoja na kupanda miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Mbegu za Miti (TTSA). Katika mwaka 2011/2012, Wizara kuititia Wakala wa Mbegu za miti inatarajia kuuza kilo 12,500 za za mbegu za miti na miche 56,000 ya miti aina mbalimbali. Vilevile, Wakala utaanzisha vyanzo vinne vya mbegu bora za miti ambapo viwili ni kwa ajili ya miti ya Mkangazi (*African Mahogany*), Mfudufudu (*white teak*) na Michungwa na vingine viwili kwa ajili ya miti ya asili aina ya Mvule na Mninga. Wakala pia itaendelea kutunza vyanzo 27 vya mbegu za miti katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Wakala itaendesha mafunzo ya muda mfupi kuhusu kuanzisha bustani na kutunza miche ya miti kwa wadau mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Misitu (TAFORI). Mwaka 2011/2012, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania itaendelea na utafiti wa sampuli za udongo zilizochukuliwa katika maeneo ya majoribio ya mikaratusi. Aidha, Taasisi itaendelea kupima matumizi ya maji kwa aina mbalimbali za miti kwa mfano mikaratusi, misindano (*pine*) na miti ya asili ili kutoa ushauri wa kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAFORI kwa kushirikiana na Taasisi za Utafiti za Afrika Mashariki chini ya Jumuiya ya Kimataifa ya Kuhifadhi na Kuongeza Ubora wa Miti (*Central American and Mexico Coniferous Resources - CAMCORE*) itaendelea na majoribio ya kuotesha jamii ya miti iliyoboreshwa kutoka nchi mbalimbali ikiwemo familia 72 za Mitiki (*Tectona grandis*) huko Longuza – Muheza. Aidha, Taasisi itafanya majoribio ya kuotesha aina mbalimbali za msandarusi ili kusaidia jamii kuanzisha mashamba. Vilevile, Taasisi itawaelimisha watumiaji njia bora za uvunaji wa msandarusi na pia kusaidia kutafuta masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi pia itaendelea kusimamia na kuangalia ukuaji wa miti ya dawa iliyopewa kipaumbele cha kwanza Kanda ya Ziwa. Pia, Taasisi itaendelea kusimamia majoribio ya kilimo mseto pamoja na kusambaza teknolojia hiyo katika sehemu mbalimbali nchini kutokana na uhitaji. Taasisi itaendelea kutunza na kukusanya takwimu za mashamba ya miti mbalimbali ya majoribio katika kanda zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAFORI imekuwa ikifanya tafiti na kutunza sampuli za miti-vichaka (*shrubs*) na mimea mingine yenye matumizi mbalimbali katika Hebaria yake. Kichaka aina ya *Carissa spinarum* ambayo hapo awali ikiujulikana kama *Carissa edulis* kiko katika familia ya *Apocynaceae*. Kichaka hiki hutumika katika kutengeneza tiba ya asili huko Samunge maarufu kama "Kikombe cha Babu". Hifadhi ya sampuli za kichaka hiki, imefanyika toka mwaka 1925 na kuna makusanyo 22 kutoka maeneo mbalimbali ya nchi ikiwemo Samunge. Katika maeneo haya kichaka hiki hufahamika kwa majina mbalimbali kama ifuatavyo Mugamuryok (Sonjo), Mchofwe (Pare), Qach (Barabaig), Machame, Manka (Chagga), Msuuku (Fipa), Titiwi (Gorowa), Umuyonza (Waha), Muyonzaki, Muyanza, Muyonza (Haya), Mfumbwe, Mvambandusi (Hehe), Quach, Titiyo (Iraqw), Mkanga onza, Mkangayonza (Kerewe), Munyore, Rinyore (Kuria), Olamuriaki, Olyamliyak (Maasai), Mkumbaku (Nguu), Mfumbeli (Nyamwezi), Mkabaku (Rangi), Mfumba, Mkumbaku (Sambaa), na Mukambaku (Zaramo).

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuzaji wa mti-kichaka huo hufanyika kwa njia ya mbegu, maotea na vilevile kwa njia ya vipande kutoka kwenye mti wenywewe yaani matawi au mizizi. Kwa vile mti huu umeonekana kutumika kwa wingi, katika mwaka 2011/2012, Taasisi itasaidia katika kuuzalisha na vilevile kuweza kukusanya takwimu za kiwango cha upatikanaji wake ili kusaidia katika uhifadhi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi itaendelea na utafiti juu ya bioteknolojia ya aina mbalimbali za kloni za miti ya mikaratusi (*Eucalyptus clone*) inayofaa iliyopandwa katika maeneo 15 ya majoribio nchini. Miti hiyo inayokua haraka itaendelea kutunza na kuboreshwa katika bustani za Kwamarukanga – Korogwe, Mufindi na Kibaha na teknolojia hiyo kusambazwa kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii. Katika jitihada za kuboresha huduma na kuongeza mapato yatokanayo na sekta ya utalii, mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kupanga hoteli katika daraja za ubora wa nyota kwa Mikoa ya Arusha na Manyara kufuatia kukamilika kwa zoezi la uhakiki wa hoteli katika Mikoa hiyo. Aidha, Wizara itaendelea kutoa ushauri kwa

wawekezaji wapya katika ujenzi wa hoteli za kitalii ili zijengwe kwa kuzingatia ubora wa madaraja. Hatua hii itachukuliwa kufuatia kukamilika kwa mafunzo ya wataalam watakaohusika katika zoezi la upangaji hoteli katika daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kufanya doria, ukaguzi na kutoa elimu juu ya Sera, Sheria na Kanuni za Utalii kwa wakala wa biashara ya utalii hapa nchini. Wizara itafungua Ofisi za utalii katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa ili kuwawezesha wafanyabiashara ya utalii kupata huduma kwa karibu na urahisi. Ofisi hizo zitatumika kukuza na kuendeleza utalii, kuongeza kasi ya utangazaji wa vivutio na huduma za utalii. Katika jitihada za kukuza na kuendeleza utalii, Wizara itaendeleza mazao ya utalii wa fukwe, kihistoria na kiutamaduni, michezo na ikolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Utalii Tanzania (*TTB*). Katika mwaka 2011/2012, Bodi itaendelea kuboresha tovuti kwa kuongeza lugha za kimataifa za Kijerumani, Kifaransa, Kihispaniola na Kiitaliano. Bodi itaendelea kutangaza mazao na huduma za utalii katika maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuvutia watalii. Aidha, Bodi itaendelea kuchapisha majarida mbalimbali yanayoeleza vivutio vya utalii kwa lugha mbalimbali na kualika na kudhamini safari za wakala wa utalii na waandishi wa habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudzi za kupanua wigo wa mazao ya utalii, Bodi itaendelea kutangaza vivutio vya utalii wa utamaduni na utalii ikolojia wa Tao la Mashariki ikiwemo milima ya Udzungwa, Usambara na Upare. Aidha, itatangaza vivutio vya kihistoria vya miji mikongwe ya Pangani, Bagamoyo, Kilwa na Ujji na Michoro ya Miambani-Kondoa. Vilevile, Bodi itaandaa jarida litakalotangaza maeneo ya vivutio vya kipekee (*hard tourism*) kama vile Jiwe la Ukerewe linalocheza, viboko wa Lindi wanaotii amri, Maporomoko ya Kalambo na Kimondo cha Mbozi kwa ajili ya watalii wanaoweza kufika maeneo yasiyo na huduma za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi itaendelea kutangaza vivutio vya utalii kupitia vipindi vya redio na televisheni ili kukuza na kuendeleza utalii wa ndani. Vilevile, Bodi itaandaa kaulimbiu maalum ya kuhamasisha utalii wa ndani, kuendesha semina za uhamasishaji kwa vikundi mbalimbali kama vile watumishi wa umma na binafsi pamoja na wakurufunzi. Katika kuadhimisha miaka 50 ya uhuru wa Tanzania Bara, Bodi kwa kushirikiana na mwakilishi wake wa Marekani imeandaa shindano la kuorodhesha sababu 50 za kutembelea Tanzania. Shindano hilo litafanyika kwa kutumia mitandao ya kijamii ya *twitter* na *facebook*. Mshindi atazawadiwa kutembelea vivutio vyetu katika kipindi hiki cha maadhimisho. Aidha, utaratibu wa kujitangaza kupitia Ligi ya Mpira wa Miguu ya Uingereza utaendelea ikiwemo kutumia magazeti (*inflight magazines*) ya Shirika la Ndege la Hispania na Uingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii (*NCT*). Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wakala utaendelea kutoa mafunzo katika tasnia ya ukarimu na utalii kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada katika Kampasi zake tatu. Kampasi ya Temeke itatoa mafunzo ya Utalii kwa wakurufunzi 140 wakati Kampasi ya Arusha itaendelea kutoa mafunzo ya Ukarimu kwa wakurufunzi 165. Aidha, Kampasi mpya ya Dar es Salaam itanza kutoa mafunzo ya ukarimu kwa kudahili wakurufunzi wapya 156 na kuendelea kutoa mafunzo kwa wakurufunzi 144 wanaoendelea na mafunzo. Kuanzishwa kwa Kampasi hii mpya kutaongeza udahili kutoka 321 katika mwaka 2010/2011 hadi kufikia 605 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kukamilika kwa Kampasi mpya yenye vifaa vya kisasa vya kufundishia, Wakala utaandaa mitaala ya mafunzo ya usimamizi katika tasnia ya ukarimu ili kuongeza idadi ya Watanzania wenye taaluma hiyo. Aidha, Chuo kina mpango wa kutoa mafunzo ya wakufunzi wa masomo ya ukarimu na utalii ili kuboresha utoaji mafunzo katika tasnia ya ukarimu na utalii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Malikale. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kukamilisha mkakati wa utekelezaji wa Sera na kuandaa Sheria ya Malikale. Pia, Wizara itaendelea kuandaa orodha ya maeneo yenye urithi wa utamaduni, katika maeneo ya wapigania uhuru ya Mikoa ya Lindi na Mtwara. Vilevile, Wizara itafanya utafiti wa mila na desturi za wenyeji kwenye Njia ya kati ya Biashara ya Watumwa na Vipusa. Hii ni pamoja na kuandaa mpango wa kuhifadhi

na kuendeleza eneo hilo. Aidha, utafiti utaendelea katika eneo la nyayo za zamadamu katika eneo la Engaresero Wilayani Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuandaa mpango wa kufukua na kuhifadhi nyayo za Laetoli; kumtafuta mtaalam atakayebuni michoro ya Makumbusho ya nyayo hizo; kutembelea maeneo yenye kuhifadhi nyayo ili kupata ujizi na uzoefu na kushirikiana na wataalam wa ndani na nje ya nchi ili kutafiti mazingira stahili ya kuhifadhi nyayo hizo. Aidha, Wizara itaandaa na kurusha vipindi nya televisheni nya malikale ya Mikoa ya Tanga na Lindi; kujenga kituo cha kumbukumbu na taarifa katika Mapango ya Amboni; kukarabati jengo la Kwihsara-Tabora na kushiriki katika mikutano ya kimataifa kama vile *ICCROM*, *WHC*, *UNESCO* pamoja na kulipia ada za uanachama katika mashirika hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa (*NMT*). Mwaka 2011/2012, Shirika litafanya tafiti 10 zinazoambatana na ukusanyaji wa kumbukumbu za urithi wa kihistoria na maliasili. Aidha, Shirika litahamasisha utalii wa ndani kwa kusambaza vipeperushi 5,000 kwa wadau; kushiriki katika maonesho na matamasha; kutembelea shule na kuandaa vipindi nya elimu kwa umma nya radio na televisheni. Shirika pia litaratibu mikutano miwili ya wadau wa Makumbusho kwa ajili ya majadiliano ya namna ya kuboresha huduma zinazotolewa na makumbusho; mikutano 12 ya kamati za ushauri pamoja na kuwezesha na kuandaa Programu za Siku ya Utamaduni wa Tanzania - Kijiji cha Makumbusho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika litaandaa michoro ya majengo mawili ya makumbusho za Chamwino na Dar es Salaam; kujenga uzio wa Makumbusho ya Mwalimu J.K.Nyerere-Butiama; kupanua Makumbusho ya Azimio la Arusha, Makumbusho ya Elimu Viumbe-Arusha, Makumbusho ya Majimaji - Songea na kuongeza vitendea kazi. Aidha, Shirika linatoa ushauri kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuanzisha Makumbusho ya jeshi. Vilevile, katika juhudi za kuboresha makumbusho hapa nchini, kwa nia ya kuvutia watalii wa ndani na wa nje, Makumbusho ya Taifa itaaniszha bustani ya wanyama (*Zoo*) katika Kijiji cha Makumbusho kuanzia Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala na maendeleo ya Rasilimaliwateru. Ili kukuza ufanisi wa watendaji, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kazi na inatarajia kuajiri watumishi 408 na kuwapandishwa vyeo watumishi 299 wa kada mbalimbali. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa watumishi 163 katika nyanja mbalimbali kulingana na majukumu yao. Vilevile, itaandaa mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi na kutoa mafunzo kwa Kamati ya Maadili ya Wizara. Aidha, Wizara itaandaa mafunzo ya maadili na kupambana na rushwa kwa watumishi 60 na kugawa nyaraka na miongozo ya kiutumishi kwa Idara na Vitengo nya Wizara. Pia, Wizara itaweka nyumba zote za Wizara wanazoishi watumishi katika daraja kwa lengo la kuboresha makazi yao. Wizara pia itaaniszha mfumo wa kieletroniki wa kushughulikia malalamiko ya wateja na kuendelea kuimarisha mfumo wa kieletroniki katika masjala ya wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha watumishi namna ya kujiepusha na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI na kuwawezesha kupata lishe bora watumishi walioathirika na wanaoishi na virusi nya UKIMWI. Wizara itawezesha wafanyakazi kushiriki katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Siku ya Wanawake Duniani na Siku ya Wafanyakazi Duniani. Wizara pia itawezesha watumishi kushiriki katika michezo ya Mei Mosi na SHIMIWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaongeza ufanisi katika ukusanyaji maduhuli. Ili kufanikisha zoezi hili, mafunzo kwa watumishi wanaohusika kukusanya maduhuli yatafanyika na vitendea kazi vitaongezwa. Vilevile, Wizara itaendelea kufuatilia na kufanya ukaguzi wa maeneo yenye vyanzo nya mapato pamoja na kuweka mifumo mipywa ya kukusanya maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukurani. Napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru wadau na washirika wetu wa maendeleo ambao kwa nafasi zao waliiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kama nilivyoeleza awali. Naomba kutumia fursa hii kuwataja baadhi yao kama ifuatavyo: Denmark, Finland, Norway, Ujeruman, Sweden, Ufaransa, Ubelgiji, Japan, Marekani,

Uingereza, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Benki ya Dunia, UNDP, UNESCO, FAO, IUCN, ICCROM, KfW, GIZ, GEF, AWHF, FZS na WWF.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu yote niliyoyaeleza yametekelezwa kwa ushirikiano mzuri baina ya viongozi na watumishi wote wa Wizara ambao wengi walikuwa hapa asubuhi na wengine bado wapo *Speakers Gallery*. Shukrani za pekee nazielekeza kwa Katibu Mkuu, Bibi Maimuna K. Tarishi na Naibu Katibu Mkuu Bibi Nuru H.M. Millao, kwa ushirikiano wao walioutoa kwangu. Aidha, naomba kumshukuru Katibu Mkuu aliyetangulia Dkt. Ladislaus Komba ambaye alishiriki katika kufanya kazi mbalimbali za mwaka wa fedha uliopita. Pia napenda kuwashukuru kwa dhati Wakuu wa Idara na Vtengo pamoja na Watendaji Wakuu wa Asasi zilizo chini ya Wizara hii. Mwisho, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru watumishi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa juhudhi zao kubwa walizoonyesha katika kutekeleza majukumu tuliopewa na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Ili Wizara iweze kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Bunge lako Tukufu wote kwa umoja wetu, upande huu na upande huu, likubali kuidhinisha jumla ya Shilingi 57,826,303,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 21,373,697,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi 36,344,986,000.00 kwa matumizi mengineyo na Shilingi 107,620,000.00 kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Bunge lako Tukufu, nawashukuru kwa kunisikiliza, kwa heshima kabisa, naomba kuwasilisha hotuba hii na ninaomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige, kwa hotuba yako nzuri. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tutajadili Wizara hii leo na kesho na kwamba maombi ambayo nimeshapata mpaka sasa kwa kweli yamejaa kabisa kwa hiyo siombi tena kupata ombi jipyaa hata moja ambaye hajaomba mpaka sasa naomba tu akubali ya ishe. Naomba sasa nimkaribishe moja kwa moja Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli.

MHE. JAMES D. LEMBELI-MWENYEKITI KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99 (7) na Kanuni ya 114(11), naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima, afya na kuniwezesha kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako. Kabla sjawasilisha Maoni ya Kamati, naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mkosefu wa fadhila kama sitawashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Kahama kwa kunichagua kwa kishindo kuwa Mbunge wao kwa awamu ya pili na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge. Nawaahidi kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu wote kuwatumikia kwa uaminifu na uadilifu mkubwa na kamwe sitawaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wanakamati kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati yetu. Nawashukuru kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa, ushirikiano ambao tumeujenga katika misingi ya umoja wetu kama wazalendo wa Tanzania. Aidha, namshukuru Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah Mbunge wa Mafia, kwa ushirikiano anaonipa na kwa namna ya kipekee, namshukuru sana Waziri Kivuli wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mchungaji Peter S. Msigwa, Mbunge kwa ushirikiano wake mkubwa katika Kamati yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa Taarifa kuwa Kamati ilipata muda wa siku mbili kuanzia tarehe 30 Mei hadi 1 Juni, 2011, Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara, Malengo yaliyowekwa katika Mwaka wa Fedha 2010/2011 na kupitia Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vikao hivyo, Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge aliwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2010/2011. Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi Julai, 2010 hadi Aprili 2011 na changamoto zilizojiteza wakati wa utekelezaji wa Bajeti hiyo. Aidha, Kamati pia ilipitia Mpango wa Maendeleo wa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. Sehemu hii ilijumuisha Makadirio ya Bajeti, vipaumbele na kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, Kamati ilitoa maoni na maagizo kwa Serikali katika maeneo mbalimbali ambayo Wizara imezingatia ushauri wa Kamati na kutekeleza kama ifuatavyo:-

(i) Wizara imefanya marekebisho ya kodi na tozo mbalimbali katika mashamba ya miti ya Serikali katika Mwaka 2010/2011. Katika marekebisho haya, kiasi cha ujazo wa Mti unaolipiwa ushuru wa Serikali umepunguzwa kutoka asilimia mia moja 100 hadi asilimia sabini (70). Hatua hii itasaidia wananchi wengi kuweza kumudu gharama za mbaao na kujenga nyumba bora.

(ii) Wizara imezijengea uwezo Taasisi zake za utafiti ambazo ni TAWIRI na TAFORI na kuwezesha TAFORI kufanya utafiti wa magonjwa na wadudu waharibifu wa misitu ya *Sao Hill*, tatizo la miti kukauka huko *West Kilimanjaro* na wadudu walioshambulia miti aina ya Misindano katika misitu ya Meru.

(iii) Utafiti kuhusu matunda ya asili kwenye misitu umefanyika katika maeneo ya Tabora na Iringa. Matokeo yameonyesha kuwa bado kuna miti mingi itoayo matunda ya asili ambayo inaweza kuongeza kipato kwa jamii zinazozunguka hiyo misitu.

(iv) TAFORI wamewezeshwa na Wizara kufanya tafiti kuhusu misitu na miti. Villevile TAWIRI imewezeshwa kufanya utafiti kuhusu namna ya kupunguza migongano ya tembo na wananchi wanaoishi magharibi mwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, kutathimini uharibifu wa mazao unaofanywa na tembo, kugundua mienendo na mizunguko ya tembo katika Vijiji na utafiti kuhusu majoribio ya utumiaji wa fensi ya pilipili ili kuzuia tembo waharibifu wa mazao umefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizoikabili Wizara wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2010/2011. Ukusanyaji wa Mapato. Katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, Wizara ilikadiria kukusanya Shilingi 72,151,100.00 kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Aprili, 2011, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi 65, 465,014,242.94 sawa na asilimia 90.7 ya makisio. Hadi ilipofika Juni 30, 2011 Wizara ilikadiria kuvuka lengo la Makusanyo kwa kukusanya jumla ya Shilingi 73,319,927,685.92 sawa na asilimia 101.6. Pamoja na kuweka lengo hilo, Kamati inaamini Wizara bado ina uwezo wa kukusanya makusanyo zaidi ya hayo iwapo Wizara itasimamia vyema vyanzo vyake vyaa mapato hasa viingilio kwenye mbuga za wanyama, vitalu vyaa uwindaji wa kitalii, uvunaji wa mashamba ya miti, mauzo ya nyara za Serikali ikiwa ni pamoja na uwindaji wa wanyama na uvunaji wa asali.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kawaida. Katika mwaka wa Fedha 2010/2011, Bunge lako liliidhinisha jumla ya Shilingi 65, 506,240,000.00 kwa Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za Miradi ya Maendeleo ni Shilingi 10,107,260,000.00. Hadi kufikia Aprili, 2011, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi 35, 064,177,687.00 kati ya Shilingi 65,506,240,000.00 zilizoidhinishwa. Changamoto kubwa iliyokabili Wizara katika kukamilisha malengo yake ni pesa pungu zinazotolewa na Wizara ya Fedha (Hazina) ikilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya Fedha kwa Matumizi ya Wizara na Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa 2011/2012. Wizara ya Maliasili na Utalii Fungu 69, inaomba kuidhinishiwa Shilingi 57,825,943,000.00. Kwa ajili ya matumizi ya Wizara, kati ya fedha hizo Shilingi 107,260,000.00 ni fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika kitabu cha fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Fungu 69, kinaonyesha Wizara hii haikutengewa fedha yoyote ya Bajeti ya Maendeleo kutoka ndani au nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina wasiwasi ikiwa hakuna kiasi chochote cha fedha ya Maendeleo kilichotengwa Wizara itawezaje kutekeleza miradi ya Maendeleo? Kamati haikuridhishwa na Serikali kutotenga fedha hizi ambazo ni muhimu kwa shughuli za kupanda miti, kulinda vyanzo vya maji, kuhifadhi maeneo ya wanyamapori, kuzuia ujangili na kukuza utalii ambayo ndio majukumu ya msingi ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Ikiwa Wizara hii itatumika vizuri ina uwezo mkubwa wa kutoa ajira, kupunguza umaskini wa kipato mionganoni mwa wananchi na kuchangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa pato la Taifa. Kutowana na umuhimu wa sekta hii, Kamati ina maoni na ushauri ufuataao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa ugawaji vitalu. Mwaka 2009 Bunge lako lilipitisha Sheria Namba 5 ya Uhifadhi wa Wanyamapori. Katika Sheria hiyo pamoja na mambo mengine inaelekeza kuwa, Mwekezaji yeote wa kigeni analazimika kutenga hisa zake kwa asilimia ishirini na tano (25) kwa Watanzania. Aidha, Sheria hiyo pia ina kipengele kinachoelekeza kuwa ni asilimia kumi na tano (15) ya makampuni ya kigeni ndio yanaruhusiwa kupata vitalu vya uwindaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sheria ilikusudia kuwasaidia Watanzania, wazawa/wazalendo kuendesha biashara hiyo na kwa kuwa suala la ugawaji wa vitalu vya uwindaji ni suala linalolalamikiwa muda mrefu kuwa lina mianya ya rushwa na kwa kuwa tayari mchakato wa kugawa vitalu unaendelea. Kamati inapendekeza yafuatayo:-

- (i) Watanzania watakaopewa vitalu hivyo ni vyema wakawa watu wenye uwezo wa kifedha na wenye weledi katika uendeshaji biashara. Wizara ihakikishe asilimia ishirini na tano (25) ya hisa za kampuni za kigeni zinamiliwi na wazawa (Watanzania) kwa mujibu wa Sheria badala ya hisa zote kumiliwi na wawekezaji ambao ni wageni.
- (ii) Watakaopewa vitalu wawe wamefanyiwa tathimini ya kina kubaini uwezo wao kabla ya kugawa vitalu hasa katika maeneo ya uhalali wa dhamana za benki walizotoa, taarifa sahihi za waombaji kuhusu ulipaji wa kodi, uraia wa baadhi ya wenye kampuni na wanahisa wake na uhalali wa kampuni zilizoomba vitalu.
- (iii) Pamoja na baadhi ya watu kudai kwamba Sheria Mpya ya Wanyamapori ina upungufu hata kabla ya kuanza utekelezaji wake. Kamati inaishauri Serikali kuwa, Sheria hii ipewe nafasi ya kutekelezwa na Serikali ifuatilie kwa karibu utekelezaji wake na ikiwa kuna changamoto zitakazojitokeza, hatua muafaka zichukuliwe kukabiliana na changamoto hizo pamoja na kuleta marekebisho ya Sheria hiyo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na mapendekezo haya, zipo taarifa kwamba mchakato unaoendelea wa kugawa vitalu umegubikwa na mambo yanayoashiria kutokuwapo kwa uadilifu katika mchakato mzima. Mambo hayo yanayolalamikiwa ni pamoja na jinsi matangazo ya maombi yalivyoshughulikiwa, ufunguaji wa maombi kufanywa na kikundi kidogo cha Maafisa na baadhi ya Maafisa kubinafsisha mchakato mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lisemwalo lipo kama halipo linakuja. Kamati inaishauri Serikali kuchunguza kwa kina malalamiko haya na ikithibitika mchakato huo haukufanywa kwa uwazi na

shirikishi basi mchakato huo uanze upya ili kuwatendea haki wote walioomba ili kujenga mazingira ya utawala bora katika tasnia ya uwindaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya mipaka/misitu na Hifadhi za Taifa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga kiasi cha asilimia 20 ya ardhi ya nchi yetu kama hifadhi ya maliasili. Pamoja na jitihada hizo za Serikali kumekuwa na migogoro mingi ya mipaka kati ya jamii na hifadhi. Migogoro hii imesababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi hivyo kuathiri maisha na ustawi wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kukabiliana na migogoro hiyo, Kamati inapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe:-

Wizara itumie vifaa vya kisasa kama GPS katika kuhakiki mipaka na kisha kuweka eneo maalum *Buffer zones*. Zoezi hili lifanyike kwa kushirikisha wananchi wa maeneo husika. Aidha, Kamati inashauri kwenye maeneo ya misitu ambayo huduma za jamii kama shule, zahanati na kadhalika vimeshawekezwa ndani ya misitu ni vyema maeneo hayo yakaondolewa ndani ya misitu. (*Makof*)

Kwenye maeneo ambayo ni ya muhimu kuhifadhiwa na hayajavamiwa na wananchi au Wanaviji ni vema hatua za makusudi zichukuliwe ili kuyahifadhi maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utoroshwaji wa Wanyama Novemba, 2010 Kupitia Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KA), nchi yetu ilipopata uhuru ilionesha azma kubwa ya kuhifadhi Wanyamapor wakati ule Waziri Mkuu wa Tanganyika Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere alipotoa lile tamko maarufu la Arusha alisema: "Uhai wa Wanyamapor ni jambo linalotuhusu sana sote katika Afrika. Viumbe hawa wa porini, wakiwa katika mapori wanamoishi, sio muhimu tu kwa ajili ya kuajabiwa na kuvutia lakini pia ni sehemu ya maliasili yetu na pia ndio mustakabali wa maisha yetu ya baadaye". Kwa kukubali dhamana ya Wanyamapor wetu tunatamka kwa dhati kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba wajukuu wa watoto wetu wataweza kufurahia urithi huu mkubwa na wa thamani adimu". (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tamko la Arusha liliweka misingi na kutoa mwongozo wa kuhifadhi Wanyamapor katika Tanzania hadi hivi leo, kuna Watanzania wachache waliokosa uzalendo na nchi hii wakishirkiana na raia wa nchi za nje na kwa kutumia Ndege ya mizigo ya Jeshi la *Qatar* tarehe 24 Novemba 2010 walitorosha nchini Wanyamapor hai 116 wenye thamani ya Sh. 163,732,500.00 na ndege hai 16 wenye thamani ya Sh. 6,838,000.00 jumla kuu ikiwa Sh. 170,570,500.00.

Mheshimiwa Spika, uhalifu huu ulifanyika kupitia uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. Mpaka Kamati yetu inatoa Taarifa hii ndani ya Bunge lako Tukufu hajulikani wanyama wale baada ya kupakiwa pale Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro walipelekwa wapi na kama bado wako hai. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Serikali kupitia Sheria ya Wanyamapor Namba 5 ya Mwaka 2009 ikisomwa pamoja na Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 ya Mwaka 2002 imeshawakamata baadhi ya watuhumiwa. Kamati imesikitishwa na uharamia huo uliofanywa na Watanzania wale bila kuzingatia kwamba viumbe hao pia wana haki ya kuishi. Lakini pia imesikitishwa na jinsi Serikali inavyopata kigugumizi katika kushughulikia suala hili hasa katika kuhakikisha rasilimali hiyo muhimu na adimu ilioibwa inajulikana iko wapi na inarudishwa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imesikitishwa na hatua ya Serikali kupuuza mapendekezo ya Kamati kuhusu suala hili. Mapendekezo hayo ya kitaalam yailenga kuisaidia Serikali kuhakikisha upatikanaji wa wanyama hao. Ni jambo la kufedhehesha kuona kwamba tangu utoroshwaji wa wanyama hao ufanyike Novemba 24, 2010 hadi leo bado Serikali ilikuwa hajui wanyama hao wako wapi hali inayotia mashaka na kuhoji kulikoni? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maswali mengi ya kujiuliza kuhusu suala hili la utoroshwaji wa wanyama hao. Katika wanyama 116 walitoroshwa wenye thamani ya Sh. 163,732,500.00, ni pamoja na twiga wanne (4), Kama ndivyo, Kamati inauliza kwa nini Sheria ya Wanyamapori inayozuia raia wa Kigeni kupewa leseni ya kukamata wanyama wakiwemo twiga amba ni Nembo ya Taifa haikuzingatiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika kuna dalili kubwa ya uzembe na kulindana ndani ya Wizara hii na ndio maana kumekuwa na kigugumizi katika kushughulikia ushauri wa Kamati. Ukweli wa mashaka haya unajidhihirisha katika zoezi zima liliofanyika hivi karibuni ndani ya Idara husika la kuhamisha Maafisa. Zoezi ambalo halikuwagusa kabisa Maafisa wa Kitengo cha Uwindaji na *CITES* wakiwemo wa Arusha, licha ya kadhia hiyo ya kutorosha Wanyama, badala yake baadhi ya Maafisa hao wamepandishwa vyeo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwabaini wote waliohusika na sakata hili na kuwafikisha kwenye vyombo nya dola mara moja. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha anakuwepo Afisa Wanyamapori wa kudumu katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ambapo nyara nyangi zinazosafirishwa nije hupitia. Kuwepo kwa Afisa kama huyo katika Uwanja huo wa Ndege kutapunguza mianya ya watu kutorosha rasilimali za nchi hii kama ilivyofanyika tarehe 24 Novemba 2010. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ujangili nchini, ni jambo la kusikitisha kuwa, kiwango cha ujangili nchini kimefikia hatua ya juu katika mapori yote ya akiba yaliyopo nchini. Pamoja na nia njema ya Raís Jakaya Mrisho Kikwete kutaka kuisaidia Wizara katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imekaa kimya wakati wanyama na misitu ikiendelea kuteketea. Kamati inashangazwa na hatua ya Wizara ya kutotaka kuitumia vizuri fursa hii ya msaada wa Rais wa kuiongezea nguvu ili iweze kutokomeza tatizo hili la ujangili katika mapori ya akiba. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa Urani katika Pori la Akiba la Selous, kimsingi chimbuko la uchimbaji wa madini ya urani lilitokana na Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kutaka kufanya utafiti ili kubainisha madini ya urani yaliyopo nchini. Wizara ya Nishati na Madini ilikwishatoa kibali kwa kampuni ya *Mantra Tanzania Limited* kufanya utafiti huo. Utafiti uliofanywa tayari umeonesha kuwa katika pori la Akiba la Selous lenye ukubwa wa kilomita za mraba 50,000 kuna madini ya urani katika hifadhi hiyo yanayokadiriwa kuwa tani milioni 82.3 ambayo ikiwa yataanza kuchimbwa yatamalizika baada ya miaka ya takriban kumi na tano (15). Eneo ambalo linategemewa kuchimbwa urani lina ukubwa wa kilomita za mraba 197.94 na litazungukwa na eneo maalum *Buffer Zone* za kilomita za mraba 147.06 na kufanya jumla ya eneo ambalo litakuwa chini ya mradi huu kuwa kilomita za mraba 345 ambalo ni sawa na asilimia 0.69 ya Pori la Akiba la Selous. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009, inaruhusu uchimbaji wa madini muhimu (*strategic minerals*) ndani ya hifadhi. Kamati inapendekeza kushirikishwa kwa Kamati za Bunge za Ardhi, Maliasili na Mazingira na Kamati ya Nishati na Madini katika hatua zote tena kwa uwazi usio na usiri wowote ikiwa ni pamoja na kuziwezesha Kamati hizi mbili kutembelea eneo la mgodi na kuona hali halsi ya eneo na kujelimisha ili Kamati hizi ziweze kushauri ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali katika kubaini maeneo yenyé madini kwa ajili ya uchimbaji mkubwa kwa manufaa ya nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali kuacha kuandaa michakato hiyo kwa usiri bali michakato iwe shirkishi kwa kushirikisha wadau wote zikiwemo Kamati za Kudumu za Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato mzima wa mradi wa Urani katika hifadhi ya *Selous*, Kamati yetu haikushirikishwa kabisa, jambo ambalo linazua maswali mengi. Hadi tunaposoma Taarifa hii Kamati yetu haijapata nafasi ya kutembelea eneo hili wala si Kamati ya Nishati na Madini kutembelea hili kuliona na kupata fursa ya kuzungumza na wananchi wa eneo hilo kwa lengo la kupata maoni yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya Serengeti. Kamati imeridhishwa na uamuza uliofikiwa na Serikali baada ya kuzingatia ushauri na maoni ya wadau ndani na nije ya

nchi kuruhusu ujenzi wa barabara ya Serengeti kwamba kipande cha barabara chenyе urefu wa kilomita hamsini na tatu (53) kinachopita ndani ya Hifadhi ya Serengeti kitabaki kuwa chini ya usimamizi wa Hifadhi za Taifa (*TANAPA*). Kamati inatambua kuwa, maamuzi haya yamefikiwa kutokana na Serikali kutambua mchango wa sekta ya uhifadhi na utalii katika nchi yetu na nia ya dhati ya Serikali kuhimiza uhifadhi endelevu unaofanywa na Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mambo mengine yaliyojiteze. Yapo mambo kadhaa ambayo Kamati inaona ni muhimu kuyazungumzia ambayo kama yatazingatiwa yatasaidia kuimarika kwa Sekta ya Maliasili na Utalii, mambo hayo ni pamoja na:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgomo wa wenge Hoteli za Kitalii zilizoko Ndani ya Hifadhi ya Hifadhi Kanda ya Kaskazini kukataa kulipa tozo (*Concession Fee*). Kwa muda mrefu wamiliki wa hoteli za kitalii ndani ya Hifadhi wameendelea kulipa kiwango kidogo cha *concession fee* ambacho ni chini ya dola kumi (10) kwa kila mtalii anayelala katika hoteli. Kiasi hicho cha malipo ni kiwango ambacho kimekuwepo tangu miaka ya tisini (1990) ambapo gharama ya chumba kimoja ilikuwa katika dola mia moja mpaka mia hamsini (100- 150) kwa siku.

Kufuatia kupanda kwa gharama za kiundeshaji kiwango cha malipo cha sasa kwa chumba kimepanda hadi kufikia katika dola mia tano mpaka elfu moja (500- 1000) na zingine 1500 kwa chumba. Baada ya kuliona hilo Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) waliweka kiwango maalum (*fixed*) cha dola sitini (60) kwa kila mgeni anayelala ndani ya hoteli zilizoko hifadhini. Licha ya kiwango hicho cha dola sitini (60) kuwa bado ni cha chini ukilinganisha na bei halisi wanayotoza. Wamiliki wa hoteli hizo za kitalii wakiongozwa na *Sopa Lodges* na *Serena Lodges* na *Elewana* kwa makusudi wameendelea kulipa tozo (*Concession Fee*) ya chini ya dola kumi (10) iliyopeleke kulikosesha Taifa zaidi ya shilingi bilioni 20 kwa mwaka jana pekee. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa wafanyabiashara ambao wamekuwa hawataki kwa makusudi kufuata Sheria na taratibu zilizowekwa wanachukuliwa hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuwanyang'anya leseni za kuendesha biashara wanazomiliki. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kutoa onyo kwa kampuni zinazofanya biashara ya Utalii (*Tour Operation Companies*) kama *Leopard* na *Ranger Safari's* kutojihusisha na mgomo huo kwa kuwa hauwahuusu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya uhifadhi inahitaji fedha nyngi na kwa kuwa mapato ya Hifadhi za Taifa yanategemea tozo hizo zenyе viwango stahiki ni dhahiri kuwa wanachokifanya wenge mahotelii hayo ni wao kuvuna pesa nyngi huku wenge eneo la hifadhi (*TANAPA*) wakiendelea kuhanganya kuboresha maeneo ya hifadhi katika mazingira magumu. Kamati inaitaka Serikali kutoruhusu wawekezaji wa aina hii na kutowavumilia wote wanaoendesha kampeni ya kuhujumu mapato ya Shirika na Serikali kwa kuwapa onyo au ikibidi kuwafutia kabisa leseni za biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro. Kuna taarifa kuwa, ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro tena kwenye njia ambayo faru wanaitumia mara kwa mara, kuna mpango wa ujenzi wa hoteli yenye hadhi ya Nyota Tano. Kamati inapinga mpango huu haramu na inaitaka Serikali kusimamisha mara moja maandalizi yoyote yanayoendelea kama yapo, ili nchi yetu iendelee kuhifadhi hali nzuri ya uoto wa asili uliopo kwa ajili ya vizazi vijavyo. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuacha kuingilia katika maamuzi ya kitaalam hasa yale ya kisayansi yanayofanywa na menejimenti kwa lengo la kudumisha uhifadhi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANAPA* na Ngorongoro kulipa gawio kwa hazina, Hifadhi za Taifa Tanzania (*TANAPA*) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (*NCAA*) ni mashirika ya umma yanayomilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja 100. Mashirika haya kwa muda mrefu yamekuwa ni mfano wa kuigwa sio tu hapa nchini bali Afrika na duniani kote kwa Utendaji wake mzuri wa kazi za uhifadhi ambazo zimepeleke maeneo saba ya nchi yetu kuingizwa kwenye hifadhi za urithi wa dunia (*World Heritage sites*). Hatua hii ni ya kujivunia hasa ikizingatiwa kuwa tangu uhuru wa Taifa letu, mashirika haya yamekuwa yakiongozwa na kuendeshwa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni, Serikali imetoa maelekezo kwa Mashirika hayo kulipa gawio la asilimia kumi kutoka katika mapato yake, wakati huo Serikali ikiyataka kutekeleza majukumu yao ya msingi ya kuhifadhi maeneo yaliyotangazwa na Serikali kuwa hifadhi. Kwa mfano, wakati Serikali ilipoamua kuongeza eneo la ukubwa wa hifadhi ya Ruaha, *TANAPA* kwa niaba ya Serikali illazimika kulipa fidia kwa wananchi waliohamishwa kupisha hifadhi kiasi cha takriban shilingi bilioni sita. Mbali ya kugharamia uhifadhi mashirika haya yamekuwa yakilipa ushuru kama kampuni binafsi zinavyolipa na wamekuwa wakifanya hivyo kwa uaminifu mkubwa na bila kukwepa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii ya Serikali ya kudai gawio inahatarisha ustawi wa mashirika haya hali ambayo itaweza kuzorotesha utendaji wake wa kazi. Mwaka huu pekee *TANAPA* wanatakiwa kulipa gawio la shilingi bilioni saba, pesa ambayo ingeweza kufanya mambo mengine muhimu katika sekta ya uhifadhi. Kamati inaishauri Serikali kusitisha utaratibu huo kwani utaathiri kwa kiwango kikubwa kazi nzuri inayofanywa na mashirika haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANAPA* Ngorongoro kutangaza vivutio vyake, hivi karibuni Wizara ya Maliasili na Utalii imeiagiza Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongo (*NCCA*) na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (*TANAPA*) kusitisha utaratibu wake wa kutangaza duniani vivutio vilivyoko ndani ya hifadhi hizo na kuacha kazi hiyo ifanywe na Bodi ya Utalii Tanzania (*TTB*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii kwa hakika itarudisha nyuma jithada za Tanzania kuvutia watalii wengi kuja nchini kwa kuwa Bodi ya Utalii Tanzania (*TTB*) yenewe haina uwezo wa kifedha na watumishi wa kutosha wenye uelewa wa kina wa maeneo yenye vivutio. Aidha, Bodi ya Utalii Tanzania (*TTB*) haina mtandao madhubuti ndani na nje ya nchi. Ni ukweli usiopingika kwamba, kabla ya taasisi hizo mbili hazijajingiza katika kazi ya kutangaza vivutio vyake zenewe sambamba na Bodi ya Utalii Tanzania (*TTB*) na mawakala wa utalii nchini idadi ya watalii waliokuwa wanakuja nchini na mapato ya taasisi hizo yalikuwa duni.

Kamati inaishauri Serikali kuacha kuingilia mambo mema na mazuri yanayofanywa na mashirika haya, badala yake iendelee kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Utangazaji unaofanywa na taasisi hizo kwa mujibu wa taratibu na sio kupunguza kasi ya kazi nzuri inayofanywa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (*NCCA*) na Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*). (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kwa niaba ya Kamati namshukuru Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala, Waziri wa Maliasili na Utalii, akisaidiwa na Watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Maimuna K. Tarishi na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Nuru M. Milao, kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati kutoa majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu mkubwa napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa ushirikiano wao, maoni yao, busara na ushauri wao katika kuchambua Bajeti ya Wizara hii hadi kufanikisha kukamilishwa kwa Taarifa hii ambayo leo naiwasilisha mbele ya Bunge lako. Kwa heshima kubwa naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Abdulkarim E.H. Shah, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mjumbe; Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mjumbe; Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Abdallah Haji, Mjumbe; Mheshimiwa Suzan A. Jerome Lyimo, Mjumbe; Mheshimiwa Dokta Mary Machuche Mwanjelwa, Mjumbe; Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mjumbe; Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mjumbe; Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mjumbe; Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mjumbe; Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mjumbe; Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mjumbe; Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, Mjumbe; Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mjumbe; Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mjumbe; Mheshimiwa Al-Shymaa J. Kwegyir, Mjumbe; Mheshimiwa Philemon K. Ndesamburo, Mjumbe; Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mjumbe; Mheshimiwa Benadetha K. Mshashu, Mjumbe; Mheshimiwa Saleh A. Pamba,

Mjumbe; Mheshimiwa Dokta Charles J. Tizeba, Mjumbe; Mheshimiwa Engineer Hamad Y. Masauni, Mjumbe; Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mjumbe; Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mjumbe na mwisho Mheshimiwa Mchungaji Peter S. Msigwa, Mjumbe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge na hususan Katibu wa Bunge Dokta Thomas Kashilillah na Katibu wa Kamati Ndugu Rachel Nyega kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati mpaka kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Fungu 69 kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa James Lembeli, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambaye ametusomea taarifa ya Kamati kwa niaba ya Kamati nzima. Tunakushukuru sana. Kabla sijamwita Msemaji anayefuata ninukuu tu mahali pamoja katika ripoti ya Kamati ukurasa wa tisa ambapo panasema panahusu utoroshwaji wa wanyama kupitia Uwanja wa Ndege wa *KIA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Kamati wametwambia Bungeni hapa kwamba Kamati imesikitishwa na hatua ya Serikali kupuuza mapendekezo ya Kamati kuhusu suala hili, nina hakika kabisa hili jambo sio rahisi sana, naomba Serikali ijpange vizuri kulieleza jambo hili. (*Makofii*)

Katika hatua yoyote ile kama Kamati mnaona mmepuuza basi tushirikishane ili tuone namna ya kuhakikisha kwamba maslahi ya Taifa yanalindwa. Naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Msigwa samahani kidogo, niwaandae watakaochangia kwa kusema hapa, baada ya Mheshimiwa Msigwa atafuata Mheshimiwa Freeman Mbewe, atafuatiwa na Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae. Mheshimiwa Mchungaji endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA- MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, nakushukuru kwa kunipa nafasi hili ya kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi yetu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 99(3) na (7) Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumsifu, kumtukuza na kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye nguvu na hekima tele kwa kunipa afya njema na kuendelea kunipigania kwenye kila jambo. Kama alivyomwezesha Daudi kuibuka mshindi dhidi ya Goliath, jitu kubwa na lenye nguvu nyingi, ndivyo alivyoniwezesha mimi kushinda uchaguzi na kuwa Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini. Kwa makusudi yake maalum, ambayo sina budi kuyatekeleza nikifuata uongozi wake, namshukuru kwa Kunifanya sehemu ya Bunge hili la Kumi, ambalo binafsi naamini ni Bunge la Kimapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa, namshukuru mke wangu mpenzi, Mama Kisa Msigwa, watoto wetu Jimmy, Peter Junior, Semione, Karren na mapacha wetu, Jacqueline na Jocelyn, kwa upendo na sala zao kwangu. Huko waliko nawaomba wakumbuke kuwa: "*The value of our dignity in this World will never be determined by what we have accumulated, but rather for what we have contributed*". Thamani ya utu wetu hapa duniani haitatokana na kile tunachokichuma katika jamii, bali itatokana na kile tunachojitolea kwa jamii. Naisihi familia yangu iendelee kuniunga mkono wakati wote ninapokuwa mbali, nikishughulikia kero na matatizo ya wananchi wa Iringa Mjini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati na kwa unyenyekevu mkubwa, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Iringa Mjini kwa kunielewa, kuniamini na hatimaye kunipa heshima hii kubwa ya kuwa Mbunge wao. Wazee wa Iringa Mjini, Vijana wa Iringa Mjini na akinamama wa Iringa Mjini, kwa hiyari yao wenyewe waliamua kuchagua uadilifu dhidi ya ufisadi, umakini dhidi ya usanii na walichagua haki dhidi ya dhuluma. Nawasifu, nawapongeza na nawashukuru kwa ujasiri na ushujaa wao mkubwa waliouonesha katika kipindi chote cha kampeni zetu na hasa wakati wa kulinda kura zao. Nawapenda na Mungu awabariki sana. Sitawaangusha. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani na pongezi zangu za dhati pia nazielekeza kwa viongozi wakuu wa CHADEMA, kwa kuklongoza vema chetu na kuwa tumaini pekee na la uhakika la Watanzania wengi. Mwanafalsafa mmoja maarufu wa karne ya 16, katika moja ya maandiko yake aliwahi kusema, *"Weak leaders inspire their followers to have confidence in them. But Great leaders inspire citizens to have confidence in themselves"*. (Makof)

Viongozi dhaifu huhamasisha kuaminiwa na wafuasi wao, lakini Viongozi makini huhamasisha wananchi wajiamini, mwisho wa kunukuu. Leo Watanzania wamejitambua zaidi, wamejamini zaidi na wamekuwa na ujasiri zaidi, hata kujitokeza kwa wingi kwenye mikutano na maandamano ya kudai haki na maendeleo yao, kwa sababu wameguswa na harakati za kizalendo za CHADEMA, chini ya uongozi makini wa Kamanda Mkuu, Mheshimiwa Freeman Alkaeli Mbwe na Katibu Mkuu wetu Mheshimiwa Dokta Willbrod Peter Slaa. Nawapongeza sana, CHADEMA mwendo mdundo, hakuna kulala mpaka kieleweke. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, dira ya Wizara ya Maliasili na Utalii inalenga kuwa na Maliasili na Malikale zilizohifadhiwa vizuri, kusimamiwa na kutumika kiendelevu na kuwa na utalii unaowajibika. Kwa dira hii na utajiri mkubwa wa maliasili na vivutio vya utalii tulivyo navyo, Wizara hii, ilipaswa kuwa mtaji mkubwa wa kuharakisha maendeleo ya nchi hii. Ilipaswa kuwa chanzo kikubwa cha mapato ya Serikali katika kugharamia na kusukuma miradi mingi ya maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinyume chake, Watanzania wengi, ndani ya nchi hii, yenye utajiri mkubwa wa misitu na mbuga nydingi za wanyama, milima na mabonde ya kuvutia, pamoja na vivutio vingi vya utalii, wameendelea kuwa maskini hata baada ya miaka 50 ya uhuru wetu. Wizara ya Malisili na Utalii, iliyopaswa kuwa mtaji na chachu ya maendeleo yao, imekuwa ndiyo moja ya Wizara dhaifu kabisa kwa ubadhifuru na upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali na maliasili zetu wakiwemo Wanyamapor. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa zamani wa Marekani, Theodere Roosevelt, aliwahi kusema: "Si kweli kwamba tumeachiwa maliasili tulizonazo na mababu na mabibi zetu.... Ukweli ni kwamba tumeazimishwa maliasili hizi na watoto wetu na vizazi vijavyo", mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa bahati mbaya kuwa Viongozi wa Serikali hii wamekuwa wakiishi kama vile wana haki ya kutumia maliasili hizi kadri watakavyo na kwa nguvu zao zote. Kizazi chetu hiki ni waangalizi tu wa mali hizi ambazo ni za watoto wetu na vizazi vijavyo. Kama waangalizi tuna wajibu wa kudai uwajibikaji katika matumizi ya maliasili zilizopo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa niaba ya Watanzania, inachukua wajibu huu kudai uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za nchi hii, kwani, kila mwaka, maliasili zetu zimekuwa zikifujwa kwa makusudi na viongozi na watumishi wa Serikali kwa kisingizio cha udhaifu wa kimfumo. Upembuzi wetu kuhusu ripoti na nyaraka za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, umeonesha kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 pekee, Wizara hii ilifanya ukiukwaji mkubwa wa Sheria na Kanuni za Fedha wa jumla ya shilingi bilioni 9.2 na kusababisha Taifa lipate hasara ya moja kwa moja ya zaidi ya shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya ubadhifuru huo mkubwa ambao nimeufafanua kwa kirefu sana kwenye Kiambatanisho Namba moja cha hotuba hii, Wizara hii kinyume kabisa na Sheria ya Misitu (CAP 323) na Kanuni za Misitu za mwaka 2007, ilipunguza tozo ya mrabaha wa mazao ya misitu tena bila kibali cha mamlaka husika ya misitu na kusababisha Taifa lipate hasara ya shilingi milioni 874.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii illipa posho ya samani kwa watumishi ambao hawakustahili wanaoishi kwenye nyumba zao binafsi, kinyume na Waraka wa Utumishi na kusababisha Taifa lipate hasara ya shilingi milioni 119.3. Wizara hii, illipa mishahara ya watumishi ambao ni wastaa fu, waliokufa na walioacha ajira na kusababisha Taifa lipoteze kiasi cha takriban shilingi milioni kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani viongozi na watendaji Wakuu wa Wizara hii tulio wapa dhamana ya kuhifadhi na kusimamia fedha na maliasili zetu, wavunje sheria na kanuni na kusababisha nchi yetu ipate hasara kubwa kiasi hicho, halafu waachwe bila kuwajibishwa. Kwa mfano, Wizi huu wa fedha za wananchi, uliopachikwa jina la "mishahara hewa" umekuwa ni mchezo unaofanywa karibu kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani tukaendelea hivi, ni lazima Bunge la Kumi lichukue hatua kali zaidi za kuisimamia Serikali kuliko iliyofanyika huko nyuma, vinginevyo fedha nyingi za Taifa hili zitaendelea kufujwa kila mwaka. Watanzania wataendelea kuteseka kwa umaskini kila mwaka na Serikali itaendelea kulalamika haina pesa kila mwaka, ilhalii pesa za maendeleo zipo nydingi, lakini zinaingia kwenye mifuko ya mafisadi. Mtaalam mmoja wa sayansi ya jamii, aliwahi kusema, kwamba: "Uwendawazimu ni kufanya jambo lilelile kwa njia ile ile huku ukitegemea matokeo yawe tofauti", Watanzania hatutaki kuwa wendawazimu hata kidogo. Ni lazima tuchukue hatua tofauti katika Bunge hili la kumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ukiukwaji huu wa sheria na kanuni za fedha, umekuwa ukifanyika ndani ya Wizara hii na Taasisi nyininge za Serikali kwa muda mrefu, hata kusababisha nchi yetu ipate hasara kubwa karibu kila mwaka. Kwa kuwa wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Mhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), wamekuwa wakishauri na kupendekeza hatua mbalimbali kuchukuliwa, lakini bado ufujaji mkubwa wa fedha unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka viongozi na watumishi wote wa Wizara ya Malasili na Utalii, waliohusika katika kukiuka sheria na kanuni za usimamizi wa fedha za umma na kulisababishia Taifa hasara, wachukuliwe hatua za kinidhamu na kushitakiwa haraka iwezekanavyo, kwa mujibu wa Sheria ya Uhujumu Uchumi na kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Vinginevyo Serikali isipochukua hatua, hakutakuwa na njia nydinge sahihi na ya kizalendo, ya kuwanusuru Watanzania na umaskini wao, zaidi ya kutumia nguvu ya umma kushinikiza hatua kuchukuliwa dhidi ya wahusika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ndogo ya wanyamapori, kuhusu vitalu vya uwindaji. Kumekuwepo uelewa mdogo kuhusu nini hasa kinafanyika kwenye sekta nzima ya uwindaji wa kitalii, ikiwemo uwekezaji unaofanywa, sheria pamoja na taratibu mbalimbali zinazotawala sekta hiyo. Matokeo ya uelewa huu mdogo ni Watanzania wengi kutobaini fursa na changamoto zilizopo na kuibuka kwa migogoro ya mara kwa mara ambayo pengine si ya lazima sana kujitokeza. Kambi rasmi ya Upinzani, tunamtaka Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho yake alieleze kwa kina Bunge hili, kile kinachoendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009, Kifungu 38(3) – (e), imempa madaraka makubwa Waziri mwenye dhamana katika mchakato mzima wa ugawaji wa vitalu vya uwindaji, ikiwemo kuteua wajumbe watano wa kuingia kwenye Kamati ya Ushauri ya Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji. Hata hivyo, wakati wa uteuzi wa wajumbe hao, Waziri analazimika kwa mujibu wa sheria kuzingatia vigezo vifuatavyo: Jinsia, ujuzi na uzoefu katika masuala ya utawala, na uhifadhi wa mazingira unaohusiana na uwezeshaji wa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wajumbe walioteuliwa na Mheshimiwa Waziri Ezekiel Maige, kuingia kwenye Kamati hiyo, ni pamoja na Bwana Benno Malisa (ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na Bwana Daniel Nsanzungwako (ambaye pia ni kada wa CCM). Kambi Rasmi ya Upinzani imeshtushwa sana na uteuzi wa wajumbe hawa kuingia kwenye Kamati hiyo ya kumshauri Waziri. Watu hawa hawana vigezo vinavyotakiwa, ikiwemo ujuzi na uzoefu kwenye masuala ya utawala na uhifadhi wa mazingira unaohusiana na uwezeshaji wa kiuchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mmoja wa wataalam wa masuala ya uongozi, Bwana John Maxwel, aliwahi kusema, “*When leaders are incompetent they become destruction to the team, they waste people's energy, they prevent people from keeping the main thing, the main thing*”. Mwisho wa kunukuu.

Haifai watu wasio na vigezo vinavyotakiwa kwa mujibu wa sheria, wakapewa nafasi nyeti kama hiyo. Mathalan, Bwana Benno Malisa, anafahamika kitaaluma kuwa ana elimu ya sheria, lakini hata sheria yenyewe hana uzoefu nayo na wala hana uzoefu wowote katika masuala ya utalii na mazingira zaidi ya kujihusisha tu na shughuli za vijana wa CCM. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa Waziri amekiuka Sheria ya Wanyamaporu na vigezo vyake katika uteuzi huo. Kambi Rasmi ya Upinzani inalitaka Bunge hili Tukufu kuititia Kamati yake husika, ichunguze sababu za Mheshimiwa Waziri wa Maliasili kukiuka sheria katika uteuzi huo ili kujua alifanya hivyo kwa maslahi ya nani. Kwa kuwa uteuzi huo haukuwa wa wazi, haukufta misingi ya utawala bora na ulikiuka vigezo vya kisheria, Kambi rasmi ya Upinzani, inataka Kamati hiyo iliyoundwa na Waziri ivunjwe yote mara moja na kuundwa Kamati nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Wanyamaporu, Kifungu cha 39(3) -(b), inatamka kuwa asilimia ya kampuni za kigeni zinazopewa vitalu vya uwindaji isizidi asilimia 15 ya idadi ya makampuni yote ya uwindaji. Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kuwa kifungu hiki kinapingana na sheria yenyewe. Kwa sheria hii, hakuna kampuni inayomilikiwa na raia wa kigeni kwa asilimia mia moja. Ni lazima kampuni ya utalii imilikiwe angalau kwa asilimia 25 na Watanzania. Waziri atahakikishaje kwamba kampuni ambazo raia wa kigeni wanamiliki hisa nyingi (*majority shareholding*) hazitapewa vitalu vya uwindaji zaidi ya asilimia 15% ya vitalu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Wanyamaporu kifungu cha 12 (e) kinatamka kwamba Waziri anaweza kufuta ugawaji wa kitalu cha uwindaji endapo aliyepewa atakikodisha. Lakini kifungu cha 39(4) cha Sheria hiyo hiyo ya Wanyamaporu kinampa mamlaka Waziri kuandaa Kanuni zitakazoruhusu uhamishajhi wa vitalu vya uwindaji kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine. Hapa Kambi ya Upinzani inahoji, kuna maana gani ya kuzuia kukodisha kitalu cha uwindaji na wakati huo huo iwepo na sheria ya kuhamisha na je Kanuni hizo zimeshapitishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uhakika gani kwamba Kanuni hizo hazitatumika kuruhusu wajanja wachache kuomba na kupewa vitalu kwa lengo la kuvuza kwa bei ya juu mara baada ya kupewa kwa kisingizio cha uzalendo? Kambi rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba mwombaji yeyote atakayepewa kitalu cha uwindaji asiruhusiwe kuhamisha umiliki wake mpaka baada ya kumalizika kwa miaka miwili, tangu kupewa kitalu hicho. Endapo atakuwa ameshindwa kukiendeleza kitalu au kufanya biashara basi kitalu hicho kitangazwe kuwa wazi na uwekwe utaratibu wa mtu yeyote kukiomba upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kambi rasmi ya Upinzani inataka kujua kwa nini Kanuni za ugawaji wa vitalu vya uwindaji imekuwa ni siri ya Wizara husika. Si kwa wananchi tu, bali hata Bunge hili pamoja na Kamati yake ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, halizijui kanuni hizo. Usiri huu unatoa mwanya wa vitalu hivyo kugawiwa kwa upendeleo na pengine rushwa kupenyezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu namba 15 (a) kuhusu “Mgawanyo wa mapato yatokanayo na utalii wa picha katika maeneo yaliyo nje ya hifadhi za Taifa na mapori ya akiba, kinatamka kuwa asilimia 20 ya mapato italipwa kwa Mkurugenzi wa Wanyamaporu, asilimia 15 kwa Halmashauri za Wilaya na asilimia 65 zitarudishwa katika Serikali za Vijiji ambazo uwekezaji unafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vifungu hivyo vizuri, tumbabaini kuwa mgawanyo wa mapato hayo umekuwa haufanyiki kama inavyotakiwa. Matokeo yake mapato ya utalii wa picha kwa Kijiji cha Robanda Wilaya ya Serengeti yameripotiwa kushuka kutoka milioni 300, mwaka 2008/2009 hadi kufikia milioni 200 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na upotevu huu mkubwa wa mapato ya wananchi, Kambi Rasmi ya Upinzani, inapendekeza kuwa, vijiji viliviyotenga maeneo kwa ajili ya

uwekezaji vipewe uwezo wa kuendelea kukusanya mapato ya vitanda (*Bed fee*) na yale yanayohusu matumizi ya ardhi (*concession fee*) kwa kuingia mikataba na kukusanya mapato hayo moja kwa moja kutoka kwa wawekezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujangili. Mnamo mwezi Septemba, mwaka 1961, Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliuhakikisha ulimwengu kwamba Serikali ya Tanganyika (ambayo sasa ni Tanzania) itahakikisha wanyamapori hawataangamia kama ambavyo Serikali itahakikisha kuwa wananchi wa Tanzania wataishi. Leo miaka takriban 50 tangu Baba wa Taifa atangaze dhamira hiyo njema, tunashuhudia wanyamapori wetu wengi tena wenye thamani kubwa kiuchumi wakiuawa na majangili kila kukicha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za mwezi Oktoba 2010 hadi Machi, 2011, zinaonesha kuwa Tembo 55 walieuawa na majangili kwenye mbuga mbalimbali kama, Katavi (tembo 7), Kilimanjaro (3), Lake Manyara (4), Mikumi (4), Mkomazi (1), Ruaha (4), Serengeti (17), Tarangire (10) na Udzungwa(1). Hii ni hali ya hatari sana na hasa ikizingatiwa kuwa wanyama hao wengi, wameuawa ndani ya kipindi cha miezi sita tu na kwa mantiki hiyo hali hii ikiachwa, kwa mwaka wanawenza kuuawa jumla ya Tembo 110 na kwa miaka mitano Tembo 550 watakuwa .

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha kuwa upo uwezekano mkubwa wa kupoteza maliasili yote ya Wanyamapori mikononi mwetu kabla hatujairithisha kwa vizazi vijavyo. Hii ni kwa sababu tu watendaji waliopewa dhamana ya kuhifadhi maliasili zetu, wamekuwa wabinafsi na hawajibiki ipasavyo, huku Serikali iliyopewa jukumu la kuwajibisha, ikiwaacha bila kuwachukulia hatua madhubuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi rasmi ya Upinzani, inahoji, je huku ndiko kuthubutu, kuweza na kusonga mbele kunakohamasishwa? Tunaitaka Serikali ijieleze imechukua hatua gani madhubuti mpaka sasa, kukabiliana na wimbi hili la ujangili? (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi wa Wanyamapori. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu na za kisheria aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, kwa uzembe na au kwa kufanikisha wizi wa wanyamapori hai 130, wakiwemo Twiga, uliofanyika Novemba 26 mwaka jana (2010).

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii, yaliyoainishwa katika ukurasa wa tatu wa randama ya Wizara husika iliyotolewa hivi karibuni, ni "...Kulinda rasilimali za maliasili (ikiwemo Wanyamapori walioibwa) na malikale dhidi ya matumizi haramu na kuhakikisha utoaji bora wa huduma za utalii". Kwa hiyo, Kambi rasmi ya Upinzani, inataka viongozi na watumishi hawa wa umma wawajibishwe kwa sababu ya kuzembea wajibu wao au na kufanikisha wizi huo.

Pia Serikali iwawajibishe wakuu na watendaji wote wa vyombo vya usalama waliopewa dhamana ya moja kwa moja ya kulinda maliasili zetu. Tunaitaka Serikali ilieleze Bunge hili wanyama wetu hao wako wapi mpaka sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya kuchukuliwa hatua, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii, mapema mwaka huu alihamishwa na kuelezwaa kuwa amepelekwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kupangiwa kazi maalum. Pia, aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori wakati wizi huo unafanyika, badala ya kuchukuliwa hatua, Februari mwaka huu alipewa likizo mpaka atakapostaa fu kwa mujibu wa sheria. Kwa namna yoyote ile maamuzi ya kuhamishwa kwa viongozi hao, yanatoa picha mbaya kuwa Serikali yetu inaendeleza utamaduni wa kulindana badala ya kuwajibishana.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani wanyamapori hai 130 wakiwemo Twiga, wanyama wakubwa kabisa, waibwe, wasafirishwe kutoka mbugani hadi uwanja wa ndege wa KIA, wapakiwe kwenye Ndege ya Qatar na hatimaye watoroshwe nje ya nchi, halafu viongozi wakuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Idara zake wasijue, haiwezekani. Watanzania sio wajinga hadi waibiwe hivyo, tutawaongoza kudai utajiri wao ikiwa hatua dhidi ya watuhumiwa hawa wakubwa hazitachukuliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni aibu kubwa kwa Taifa. Tunalitaka Bunge lako Tukufu lihakikishe watuhumiwa hawa wakubwa na wengine wote wanaohusika wanawajibishwa haraka iwezekanavyo. Ni lazima tujenge Taifa la viongozi wanaowajibika na wanaowajibishwa pindi wanapofanya uhalifu na pindi uhalifu unapofanyika chini ya na ndani ya mamlaka yao. Vinginevyo, Watananzania wataendelea kuwa maskini daima, kwani maliasili na kodi zao zitaendelea kuibwa na kufuja kila mwaka

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ndogo ya utalii. Kwa mujibu wa randama ya Wizara hii, iliyotolewa hivi karibuni, mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa umekadiria kuwa ni asilimia 17.2. Serikali imeeleza kuwa mchango huu umetokana na shughuli za utalii katika sekta ndogo za Wanyamapor, Hoteli, Usafirishaji, Mambo ya Kale, Mawasiliano, Blashara, Michezo na kwamba unachangia asilimia 25 ya mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani hairidhishwi na kiwango hiki cha ukuaji wa Sekta ya Utalii wala mchango wake katika Pato la Taifa, kwani mapato mengi ya utalii yanapotea kila mwaka kwa sababu mbalimbali ikiwemo kuwa na miundombinu duni ya usafiri, kutosimamiwa kikamilifu kwa Sheria za Utalii hapa nchini, ujisadi na zaidi ni kutokuwepo kwa mikakati na mipango madhubuti ya kuboresha sekta hii kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafti zinaonesha kuwa nchi zenyé Shirika la Ndege la umma, asilimia 70 ya mapato yanayotokana na utalii hubakia ndani ya nchi husika, ilhalii kwa nchi ambazo hazina *National Carriers*, ni asilimia 30 tu ya mapato yanayotokana na Utalii ndio hubakia katika nchi hizo. Ndio maana nchi kama Kenya inapata watalii zaidi na mapato ya Utalii hubakia nchini humo kwa kiwango kikubwa. Wakati Serikali hii ikijivunia takwimu zake za ukuaji wa sekta ya utalii, tafti mbalimbali zinaonesha kuwa ni theluthi moja tu ya mapato yanayotokana na Utalii ndio hubakia nchini, kwa sababu Shirika letu la Ndege limekufa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza maradufu mapato yatokanayo na utalii na hivyo kuchochaea ukuaji mkubwa na wa haraka wa uchumi, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaendelea kusisitiza ushauri wetu wa kuitaka Serikali ishirikiane na Mashirika ya Umma yenye kuendesha shughuli za uhifadhi, katika kumiliki Shirika la Ndege, kuanzia katika mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu huu tunaoupendekeza, sehemu ya mtaji ishikwe na Serikali na itakapofika Shirika kuanza kupata faida, wananchi wauziwe sehemu ya hisa za Shirika. Uwekezaji kutoka njie sio mwarobaini wa matatizo yetu yote. Tunaweza kutumia mitaji ya ndani kimkakati ili kuimarisha Shirika la Ndege. Jambo la msingi ni Serikali kusafisha vitabu vya Shirika kwa kuchukua madeni yote na kuingiza uwekezaji kutoka mashirika ya umma ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Uchukuzi, iharakishe upanuzi na uboreshaji wa huduma katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (*KIA*) kwa kuufanya kuwa wa kisasa na wa Kimataifa zaidi ili kukabiliana na changamoto ya ushindani wa kitalii, baina yetu na Kenya, ambayo taarifa zisizo rasmi zinasema imeamua kujenga uwanja wa ndege mpakani eneo la Taveta, takriban kilomita saba tu kutoka uwanja wetu wa *KIA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Magharibi iko nyuma kwa muda mrefu katika maendeleo ya sekta ya utalii, Kambi Rasmi ya Upinzani, pamoja na mambo mengine, tunaishauri Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi, kwa pamoja waharakishe ujenzi wa barabara zinazounganisha maeneo yenye vivutio vya utalii kwenye mikoa hiyo, hususan barabara ya kutoka Iringa Mjini mpaka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, kwa kiwango cha lami na kuboresha Uwanja wa Ndege wa Nduli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wakati umefika sasa kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na ile ya Magharibi, kusogezewa Chuo cha Utalii ili kiweze kuzalisha wataalam wa kutumikia sekta hiyo moja kwa moja kwenye mikoa hiyo, kama ilivyo kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Hifadhi ya Taifa (*TANAPA*), kuhusu viwango vya Malipo ya *Concession Fees*. Kumekuwepo upotetu mkubwa wa Mapato ya Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) kuitia viwango vidogo vya *concession fees* zinazolipwa na wamiliki wa hoteli za kitalii zilizopo hifadhini. Mapato ya *concession fees* yamekuwa ni kidogo sana kulinganisha na yale yanayotokana na upigaji mahema (*camping*) ambapo mtu mmoja hulipa takriban dola 50 za Kimarekani kwa siku, wakati *concession fees* ni wastani wa dola nane mpaka dola 10 za Kimarekani kwa mtu mmoja kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ilisababisha *TANAPA* kupoteza mapato ya shilingi bilioni 19 kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na kuambulia mapato ya shilingi bilioni 2.4 tu. Hasara hii ilitokana na hatua ya Waziri aliyejita kwenda kinyume na mapendekezo ya *TANAPA* ambayo ilitaka viwango vya *concession fees* vitozwe kwa kuzingatia *fixed rate* kwa hoteli zote ili kudhibiti upotetu wa mapato. Hapa Kambi ya Upinzani inahoji, je, Serikali hii ilichukua hatua gani dhidi ya Waziri aliyejita kwa kuisababisha nchi hasara kubwa kiasi hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hasara hiyo iliyosababishwa na Waziri aliyejita, Kamati ya Bunge hili ya Hesabu za Mashirika ya Umma, ililagiza viwango vya *concession fees* vilivokuwa vimependekezwa na *TANAPA* virejeshwe na kwa hiyo, *concession fees* ikaagizwa kuwa dola 40 za Kimarekani kutoka dola 10 za Kimarekani kwa mtu kwa siku. Hata hivyo, uamuzi huo ulipingwa vikali na makampuni yanayofanya kazi za watalii na hata kupelekea kuweka zuio Mahakamani ambalo liliamuliwa tarehe 09/08/2011, kuwa makampuni hayo yanapaswa kwanza kutangaza kwenye magazeti kuhusu kusudio la pingamizi lao ndani ya siku 30 tangu siku ya uamuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya agizo hilo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige aliandika barua yenyewe kumbukumbu AB 315/484/01 ya tarehe 02/08/2011 ambapo aliondoa agizo la awali la kuwataka waendesha biasara wa utalii kulipa wakati wanapokuwa wanaingia na badala yake makampuni haya yaandikiwe *invoice*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, je, uamuzi huo wa Mheshimiwa Waziri Maige wa kutaka mahotelii ya kitalii yaandikiwe *Invoice* badala ya kulipa *concession fees* moja kwa moja, aliutoa kwa maslahi ya nani, ikiwa hata kesi ya msingi ya pingamizi hilo bado haijatolewa hukumu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho yake ajieleze kwa uwazi wote, ni kwa nini amefanya hivyo. Pia tunaitaka Serikali mara moja ianze kutoza *concession fees* kwa mahotelii hayo ya kitalii kwa kiwango cha dola 40 za Kimarekani kwa mtu mmoja kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai kuwa pungozo la viwango vya *concession fees* lina nia njema ya kuhamasisha upatikanaji wa Watalii wengi kama nchi nydingine, hayana msingi, kwani duniani kote mbuga ya Serengeti, Ngorongoro na Mlima wa Kilimanjaro, havipatikani popote isipokuwa nchini Tanzania tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imepata taarifa za uhakika na za kushtusha kuhusu matumizi makubwa ya fedha za umma yanayofanywa na *TANAPA*, kulinganisha na kile inachoingiza. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2008/2009 gharama za uendeshaji za *TANAPA* zilikuwa shilingi bilioni 66.0 wakati shirika lilikusanya kiasi cha shilingi bilioni 70.4. Katika kipindi hicho *TANAPA* ilitumia shilingi bilioni tatu tu kwa ajili ya kusaidia jamii. Mwenendo mzima wa mapato ya *TANAPA* umo katika Kiambatanisho Na. 2 cha hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii, ni dhahiri kuwa mapato mengi ya *TANAPA* yanaishia kwenye kugharamia zaidi utawala wake kuliko kuingia Serikalini na kusaidia jamii. Kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha inadhibiti matumizi makubwa yasiyo ya lazima ya fedha za umma yanayofanywa na *TANAPA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kashfa ya jengo la *TANAPA*, Kambi Rasmi ya Upinzani ina taarifa kuwa Serikali imeliamuru Shirika la *TANAPA* kuhama mara moja kutoka kwenye jengo lao la Makao

Makuu ya Hifadhi za Taifa liitwalo Mwalimu J.K Nyerere *Conservation Centre* ambalo ni mali ya TANAPA. Hatua hiyo imekuja kutokana na Mahakama ya Afrika kumwomba Mheshimiwa Rais Kikwete awapatie jengo hilo, licha ya kuwa lilijengwa mahsus kwa ajili ya shughuli za TANAPA.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema ikakumbukwa kuwa huko nyuma, TANAPA walijenga jengo lao la kitega uchumi (*commercial wing*) mkabala na makao makuu, ambalo Mahakama hiyo ya Afrika walipangishwa, lakini leo taarifa tulizonazo ni kwamba wamepewa jengo hilo kwa nguvu na Rais na TANAPA wametakiwa kutafuta sehemu nyingine ya kupanga kwa ajili ya ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imesikitishwa sana na taarifa hizi na zinaonesha kuwa Serikali yetu ipo tayari kuyapokonya mashirika yetu vitega uchumi vyake, kwa sababu tu ya kuzibeba taasisi za nje. Kuna msemo wa Kiingereza usemao, “*If you dont know where you are going, then any road will take you there*”, “Kama hujui unakokwenda, basi unawenza kuchukuliwa na njia yoyote”. Taarifa za Serikali kutaka kuipokonya TANAPA jengo lake, inadhihirisha kuwa Serikali yetu haijui inakokwenda, kwani jengo hilo halikujengwa kwa ajili ya Mahakama ya Afrika, bali lilijengwa kwa ajili ya TANAPA kwa malengo ya TANAPA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka uamuzi huo usitishwe mara moja na TANAPA waendelee kubaki na jengo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kashfa ya ukwepaji kodi. TANAPA ina mgogoro katika Hifadhi ya Arusha unaohusisha eneo la Mashamba namba 40 na 41 ambayo ni mali ya Shirika hilo. Katika eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 996 kuna mali mbalimbali yakiwemo majengo ya hoteli iJulikanayo kama *Momella Wildlife Lodge* inayoendeshwa na kampuni ya *Lions Safari International (LSI)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, TANAPA ilinunua eneo hilo pamoja na mali zote zilizokuwemo mnamo mwaka 1988 kutoka Serikalini na hivyo kumfanya mwendeshaji wa hoteli hiyo kuwa mpangaji wa Shirika na kwa hiyo, Mwekezaji alipaswa kulipia pango hilo. Hata hivyo, hoteli hiyo haijawahi kulipia pango, ambapo hadi kufikia tarehe 31 Desemba 1998 ilipaswa kulipa jumla ya shilingi bilioni 1.4 na baada ya hapo kuanzia tarehe 1 Januari 1999, ilipaswa kuanza kulipa kiasi cha shilingi milioni 149.3 kwa mwaka, lakini kodi zote hizo hazikulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hoteli ya kitalii ya Bilila iliypopo Serengeti tangu kuanzhishwa kwake, imekuwa hailipi tozo za malazi tangu ilipojengwa mpaka sasa kutokana na Serikali kuisamehe kulipa tozo hizo. Kwa kipindi cha miezi sita iliypita hata baada ya kumaliza muda wa msamaha iliokuwa imepewa (*yaani grace period*), bado imeendelea kutolipa tozo hizo ambazo hoteli nyingine zinalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema, kuwa, Serikali isiyoweza kukusanya kodi ni Serikali iliyonunuliwa na wenye mali, ni Serikali iliyowekwa mfukoni na wenye mali”. Hatua ya Wawekezaji wote hawa kutolipa kodi kwa kipindi chote hicho, inatoa picha mbaya kuwa Wawekezaji hawa bila shaka wana nguvu kubwa inayoifanya Serikali ilainike na kushindwa kukusanya kodi kutoka kwao. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho yake alieleze Bunge hili ni kwa nini kwa kipindi chote hicho, Wawekezaji hao wa hoteli wamekaidi kulipa kodi wakati Serikali ipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa *Group Endowment Scheme Assurance*, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania linao Mfuko Maalum wa kuwasaidia wafanyakazi wake wanapostaafu au kufariki kabla ya kustaafu, ambao unasimamiwa na *African Life Assurance (T) Limited*. Mfuko huo unajulikana kama *Group Endowment Assurance Scheme (GEAS)*. Uamuzi wa kuanzhisha Mfuko huo ultolewa tarehe 17-Agosti, 2007 na madhumuni yake ni kutoa nyongeza kwa mafao yatolewayo na *NSSF/PPF* ambayo ni madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko huu ulikuwa unatoa mafao ya mishahara ya miezi 24 kwa mfanyakazi aliystaa fu kazi kwa umri wa miaka 55 (kwa hiari) au miaka 60 (kwa lazima) na pia akifariki akiwa kazini. Utaratibu huu uliendelea hivyo hadi tarehe 30 Juni, 2010, lakini kuanzia Julai 2010, mafao hayo yalipitiwa upya na kuboreshwa kwa kuwalipa malipo ya mishahara ya miezi 48.

Katika kupitia upya, mkataba huo uligawanywa na kuwa mikataba miwili inayojitegemea, ambayo ni (i) *Group Endowment Fund - GEF* (Mfuko kwa ajili ya wastaafu) na (ii) *Group Life Assurance Policy - GLA* (ambayo ni bima kwa ajili ya vifo).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inashauri kuwa Shirika liachane na huduma ya *Group Life Assurance* ambayo ni Bima kwani wamekuwa wakilipa kiwango cha *premium* ambacho ni kikubwa kwa mwaka lakini idadi ya vifo vya watumishi ni ndogo na pia jumla ya kiasi cha fedha ambacho kilikuwa kinalipwa kwa warithi wa watumishi waliofariki kwa mwaka kama mafao ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchimbaji madini katika hifadhi. Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, tayari imeshaanza mchakato wa utafiti madini ya *Uranium* ndani ya eneo la hifadhi ya Taifa ya Selous kwa kuishirikisha UNESCO, kinyume cha Sheria na bila kulishirikisha Bunge. Hii si tu dharau kwa Bunge, bali pia ni dharau kwa Watanzania wote waliotutuma kuwawakilisha. Tunaitaka Serikali iwaombe radhi Watanzania na kurudi kwanza Bungeni kuomba ridhaa, ili sote tujiridhishe kama kweli kuna maslahi ya Taifa kwa uchimbaji huo kuingilia hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, pamoja na matatizo mengine mengi, Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, inakabiliwa na tatizo la kuwa na Mwenyekiti wa Bodi anayevuka mipaka ya majukumu yake. Tuna ushahidi kuwa, Mheshimiwa Pius Msekwa (Makamu Mwenyekiti wa CCM), ambaye ndiye Mwenyekiti wa Bodi hiyo, amegeuka kuwa Mwenyekiti Mtendaji anayefanya kazi ya kutoa offer kwa Wafanyabiashara wenye mahitaji ya kujenga hoteli za kitalii, huku akiwaelekeza maeneo hayo, kazi ambazo si zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mgongano mkubwa sana wa kimaslahi na wenyewe madhara makubwa sana kwa hifadhi hii. Haiwezekani Mwenyekiti wa Bodi ya Ngorongoro, ambaye moja ya majukumu yake ni kukagua hali halisi ya hifadhi hiyo, ajiingize pia katika shughuli za utendaji tena zilizo nyeti kama hizo. Kambi Rsmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua hatua kali dhidi ya Mwenyekiti huyu wa Bdi mara moja kwa kukiuka mipaka ya majukumu yake. Tunaahidi kuwa tupo tayari kuipa Serikali ushirikiano kuhusiana na tuhuma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upanuzi wa hifadhi na fidia kwa wananchi. Tanzania ina Hifadhi za Taifa, Mapori Tengefu na Mapori ya Akiba takriban 100. Nyingi ya hifadhi hizo zimeanzishwa kwa baada ya kuwahamisha wananchi walilokuwa wakiishi maeneo hayo kabla ya kufanya hifadhi, mara nyingi bila malipo yoyote kwa wananchi hao. Aidha, Serikali imekuwa ikilalamikiwa kupanua maeneo haya kwa kumega ardhi za vijiji kwa visingizio vya kupusha ucharibifu wa mazingira, tena bila kuwalipa wahanga hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalan, ili kupisha mipango ya kupanua ukubwa wa Hifadhi ya Taifa Ruaha kutoka kilomita za mraba 10,300 hadi 20,226, Serikali iliwafukuza wafugaji wa Mbarali Mkoani Mbeya (*Walsh, 2007:11*). Pia, baada ya upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Manyara, ultiotangazwa na Gazeti la Serikali No. 105 la Mei 2009, wakazi wa Kijiji cha Moyo Mayoka Wilayani Babati, waliachwa wakilalamikia kuonewa na Serikali kwa hatua ya kulifanya Ziwa Manyara lote kuwa ndani ya hifadhi hivyo kuwakosesha maelfu ya wavuvi wa samaki katika ziwa hilo chanzo kikuu cha kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuweka mazingira mazuri katika hifadhi hizo, ni vema ikazingatiwa hatma ya yote ili kuwe na ustawi wa jamii. “*We cannot preserve nature, at the expense of human life*”. Hatuwezi kuhifadhi mazingira, kwa gharama ya kupoteza uhai wa mwanadamu”. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwafidie wananchi wote walipoteza ardhi, mifugo yao na vyanzo vyao vya mapato kwa visingizio vya utunzaji mazingira. Tunaitaka Serikali ije na utaratibu mbadala wa kuhakikisha inawianisha haja ya usalama wa maliasili na haja ya usalama wa binadamu kwa pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa Sheria na Taratibu za utalii. Kifungu cha 58, kifungu kidogo cha (1) na (2), cha Sheria ya Utalii ya mwaka 2007, kwa ujumla wake vinaelekeza kwamba shughuli za uwakala wa kusafirisha watalii na kuongoza watalii mlimali zifanywe na

Watanzania tu. Pia, kifungu cha 3 cha Sheria ya *TANAPA* ya mwaka 2003, kinaelekeza *TANAPA* kushughulika tu na Wakala wa Utalii aliyeandikishwa na mwenye leseni (za *TALA*) na ambaye ni mwanachama wa chama kinachoshughulika na masuala ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vifungu hivi vizuri vilivyopitishwa na Bunge hili kwa busara ya kumjali Mtanzania mzawa, Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kuwa bado Watanzania wengi hawafaidiki vya kutosha, kwa sababu sheria hizismamiwi vizuri. Mathalan, kinyume kabisa na kifungu hicho, kampuni nyingi za kigeni zinafunguliwa hapa nchini kwa mbinu ya ubia kati ya wageni na wazawa wakati wenyewe kampuni hizo wanakuwa ni wageni na hivyo wageni wanapata mwanya wa kufanya biashara ya mlimani na faida kubwa inabaki nje badala ya kubaki kwa Watanzania wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inahoji, je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha Sheria ya Utalii ya mwaka 2007 inasimamiwa kwa manufaa ya Watanzania wazawa, ikiwa kampuni za wageni zilizokuwa zikifanya uwakala wa safari za mlimani bado zinaendelea kufanya kazi hiyo, licha ya sheria kutaka ifanywe na wazawa pekee? Je, Serikali imechukua hatua gani dhidi ya kampuni za kigeni zinazotumia mbinu ya kuingia ubia na wazawa kufanya biashara ya utalii ya kupeleka watalii mlimani, ikiwa faida kubwa iliyopaswa kuwa ya Wazawa (kwa busara ya sheria) inaishia kwa wageni?

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ndogo ya misitu na nyuki, Serikali imekuwa ikipoteza mapato mengi yatokanayo na biashara ya uvunaji magogo, kwa sababu ya kuwepo udhaifu katika usimamizi wa sheria zilizopo. Maelekezo yanayotolewa yamekuwa hayazingatiwi. Mathalan, katika msitu wa Sao *Hill* uliopo Wilayani Mufindi, Mkoani Iringa, kampuni ya Mufindi *Paper Mills* tangu mwaka 2007, imekuwa ikiuziwa mita moja ya ujazo wa miti kwa shilingi 10,000 ilhali bei iliyoelekezwa na Serikali ni shilingi 29,000 kwa mita moja ya ujazo wa miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati hali ikiwa hivyo, gharama za kutunza mita moja ya ujazo wa miti kwa miaka 25 ni shilingi 18,000. Wakati huo huo Wawekezaji wengine wakiwemo wananchi wanauziwa mita moja ya ujazo wa miti kwa shilingi 29,000/= na si shilingi 10,000, kama inavyouziwa kampuni hiyo. Kuanzia mwaka 2003 hadi 2006 kampuni hiyo ilikuwa ikiuziwa kwa bei sawa na kampuni nyiningine, lakini ilipofika mwaka 2007, kampuni hiyo ilianza kuuziwa shilingi 10,000 kwa mita moja ya ujazo wa miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii, Kambi rasmi ya Upinzani imebaini kuwa Serikali imeshapoteza mapato ya takriban shilingi bilioni 22 hadi sasa. Wawekezaji wa ndani wanazidi kupoteza imani kwa Serikali kutokana na kutokuwepo kwa usawa katika uwekezaji kwenye msitu wa *Sao Hill*, jambo linaloashiria uwepo wa harufu ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuona Bajeti za Wizara mbalimbali, kama Wizara ya Uchukuzi zikipitishwa, huku zikiwa na fedha kidogo za maendeleo, wakati fedha nyangi zinapotea bure. Kambi Rasmi ya Upinzani inalitaka Bunge hili kupitia Kamati zake za kifedha, ichunguze sababu za kampuni ya *Mufindi Paper Mills* kupewa fursa ya kuvuna hekta 300,000 kila mwaka katika msitu wa *Sao Hill* kwa bei ya shilingi 10,000, ambayo ni chini ya bei inayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia badala ya kuanzisha Mamlaka ya Misitu Tanzania, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa Sheria ya Misitu Na 14 ya mwaka 2002, isimamiwe kikamilifu kwa kuwa inakidhi mahitaji ya uhifadhi endelevu kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema, John Maxwell "Kila kitu kinasimama au kuanguka kutegemeana na kiongozi aliyeopo". Taifa letu lipo katika umaskini wa kutisha katikati ya misitu mkubwa wa rasilimali. Taifa letu linaanguka kwa sababu ya uongozi uliopo. Bunge la Kumi ndilo tumaini pekee la kunusuru Taifa hili. Bunge la Kumi lina hiyari ya kusuka au kunyoa, kwa pamoja tutimize wajibu wetu kuiwajibisha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini kwa umuhimu mkubwa, nawashukuru wote walioniwezesha kuwasilisha maoni haya. Ni jumla ya yale yote niliyofunzwa kutoka kwa wale

walionifundisha, Wakubwa kwa Wadogo. Nawashukuru Marehemu wazazi wangu, Baba yangu Mchungaji Simon Msigwa na Mama Atu Nsyenge, kwa malezi, hekima na busara walizoniachia.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kengele ya pili hiyo!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, huyo ni Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa. Aliyesoma hotuba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii. Yeye ndiye Msemaji Mkuu wa Wizara hiyo. Tunaingia katika eneo la uchangiaji, tunaanza na Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mheshimiwa Hamdan Meghji ajiandae na Mheshimiwa Joyce Nkya atamalizia.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuwa mchangiaji asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza katika masuala mawili muhimu. Kwanza suala la biashara ya utalii wa uwindaji na la pili ni suala la biashara ya utalii ya Mlima wa Kilimanjaro. Aidha, katika hatua ya awali ni vema nika-*declare interest* na nina-*declare interest* kwa sababu mimi ni mfanyabiashara ya utalii katika Mlima na kwa njia moja au nyingine katika pori lakini sifanyi biashara ya vitalu nya kuwinda. Kwa hiyo, nazungumza kwa mchanganyo wa uzoefu wangu kama mfanyabiashara, kama mwekezaji wa ndani na kama mwana siasa na kama kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe nisome tamko ambalo Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati alilizungumza hapa. Tamko la Arusha ambalo lilitamka na Mheshimiwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa sababu tu ya msisitizo na tamko hili nalitamka kwa sababu Mwalimu alilitaja mwaka 1961 tarehe 7 mwezi wa tisa ikiwa ni siku nne kabla mimi sijazaliwa. Mwalimu alizungumza maneno haya. Nitafanua kwa nini niyanukuu maneno haya. 'Kudumu kwa maisha ya wanyama wa porini ni jambo linalotuhusu sana sisi wote katika Bara la Afrika. Viumbe hawa si maajabu na fahari ya nchi yetu tu, bali pia ni sehemu mojawapo ya uchumi wetu wa asili na starehe ya maisha yetu ya leo na kesho. Katika kuchukua dhamana na ulinzi wa wanyama wa porini twathibitisha kwamba tutafanya kila tuwezavyo katika mamlaka yetu kuhakikisha kwamba watoto wetu wa kesho na keshokutwa wanaweza kufaidi utajiri na uhondo wa urithi huu. Utunzaji wa wanyamapori na misitu yake, narudia. Utunzaji wa wanyamapori na misitu yake unahitaji ujuzi maalum, watu waliofundishwa kadhalika na fedha. Kwa hivyo twataraji Mataifa ya kigeni yatashirikiana nasi katika kazi hii muhimu ambayo kutokufaulu kwake licha ya kuwa ni madhara katika Bara zima la Afrika yatakuwa ni madhara katika ulimwengu wote." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema makusudi ninukuu maneno haya ya Baba wa Taifa kwa sababu biashara ya utalii ni biashara ya Kimataifa na ni vema Watanzania tukajenga utamaduni wa kuelewa biashara ya utalii. Tukaja kwamba hakuna biashara ya utalii Tanzania kama hatuwapendi wageni, kwamba hatuna biashara ya utalii Tanzania kama tutawanyanyapaa wageni. Asilimia 98 ya biashara ya utalii katika nchi yetu inatokana na mapato ya wageni. Kwa hiyo, badala ya kuwanyanyapaa wageni ni vema tuisiwaterenge wageni hawa. Tushirikiane nao kimkakati wageni hawa. Tusiwaone wageni hawa ni wezi. Kwa sababu hawa wanaingizia Taifa letu mapato mengi sana ya fedha za kigeni. Ni wajibu wetu sisi kama Taifa sisi kama Viongozi na mamlaka nyingine zote za Kiserikali kuweka mikakati endelevu ya namna ya kuwafaidi wageni wetu hawa wa kimkakati badala ya kuwanyanyapaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo lugha tunazozitumia dhidi ya wageni ni vema tukawa waangalifu sana. Kauli tunazozitoa kwa kuona wageni wote ni wezi katika Taifa letu vile vile ni mambo ya kuangalia kwa makini sana. Ni lazima kama Taifa tusiwe *anti-investment*. Tanzania leo tunakuwa *rated* katika mojawapo ya Mataifa ambayo tunachukia wawekezaji wa nchi za nje.

Tumejenga utamaduni wa kufikiri kwamba uzalendo wetu utaweza kupimika pale ambapo tumewadhalilisha wageni. Hii si sahihi na si kweli. Kwa hiyo, ningependa sana kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naiomba Serikali yetu na Watalaan wengine wote tusaione wageni katika Taifa letu kama wezi, tuwaone kama wabia wenzetu. Tuweke mikakati ya kuwafaidi. Kama tukishindwa kuwafaidi wageni hawa ni uzembe wetu wenyewe. Tukishindwa kuwafaidi wageni hawa ni udhaifu wetu wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sisi tukienda nchi za wenzetu jambo la kwanza unalolitafuta ni ndugu yako Mtanzania yuko wapi. Kila mmoja wetu hapa akienda Marekani, akienda Uingereza, akienda Japan, hata mkienda Afghanistan jambo la kwanza unajiuiliza Mtanzania mwenzako yuko wapi? Hata kwa wageni wanapokuja nchini kwetu hapa jambo la kwanza *security* yao ya kwanza wanayoitafuta ni wapi tuna wawekezaji amba wana asili yetu. Haya ni mambo *natural* na hatuwezi kuya-*avoid*. (*Makofii*)

Kwa hiyo Watanzania wenzangu tuwe zaidi watu wa mikakati na siyo watu wa kunung'unika. Tuwe zaidi watu wa kuweka mikakati endelevu ya kunyonya utajiri wa wenzetu kwa faida ya jamii yetu. Hilo lilikuwa la kwanza la msingi sana. Nilipenda nilizungumze kuhusiana na *attitude* ya Watanzania katika masuala ya *ku-deal* na wageni. Huwezi uka-*deal* na wageni katika biashara ya utalii kama hutaki wageni waingie nchini mwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie katika biashara ya utalii, wawindaji na hapa *nilim-quote* Baba wa Taifa kwa sababu mwaka 1961 alijua suala la biashara ya utalii hatuwezi kulifanya wenyewe bila kuwa na wageni, huo ndiyo ukweli. Kuwafukuza wageni nimeshasema sio kipimo cha uzalendo. Sasa linapokuja hili suala la biashara ya uwekezaji wa utalii. Kwa bahati mbaya sana na ni kweli Mheshimiwa Waziri katika siku za usoni ni vema na Wizara yake ikaandaa Semina kutufahamisha na kufundisha Waheshimiwa ni nini maana ya biashara ya utalii wa uwindaji? Watu wengi wana tabia ya kufikiri unapewa kitalu kama hiki kina wanyama unakwenda kuwinda swala na tembo, biashara imeishia hapo. Uwekezaji wa utalii ni *highly professional*. Ni utalii unahitaji utalaam wa hali ya juu. *Skills* za hali ya juu na ni *capital intensive*. Kuendeleza kitalu kimoja cha uwindaji kwa misingi ya kitaaluma inaweza ikahitaji mtaji wa zaidi ya dola za Kimarekani milioni 100. Kwa hiyo, tunapokuwa tunapitisha Sheria kwamba tufukuze wageni wenye mitaji, tuwakatae wageni wenye mitaji, badala ya kuweka mkakati wetu wa ndani wa kufaidi wageni wenye mitaji, tutakuwa tunakwenda kuua biashara ya uwindaji bila sababu zozote za msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme vitalu hivi kwa mfano, nimeangalia Sheria. Nimesoma Sheria mbalimbali na vitu vingine, tunafanya Watanzania kwa hamaki, kwa hamaki sana. Tunafanya vitu kwa hamaki, hatuwi makini. Sheria tuliyopitisha mwaka jana kwanza hili nitoe angalizo la kwanza Mheshimiwa Waziri ulielewe na Naibu Spika na naomba Bunge hili ilielewe. Sheria ya *Conservation* ya *Wildlife* tuliyopitisha katika Bunge hili. Sikuwepo kwenye Bunge liliopita mlipitisha wenzangu waliokuwa kwenye Bunge liliopita, Bunge la Tisa. Ile Sheria iliyopitishwa na Bunge hili siyo Sheria inayotumika leo, ile Sheria imechakachuliwa. Sheria imechakachuliwa katika misingi ambayo haijawekwa wazi na hii nawaambia Serikali mkalitafakari jambo hili. (*Makofii*)

Sheria iliyopitishwa na Bunge hili siyo Sheria inayotumika leo, Sheria hii baada ya kutoka Bungeni kabla ya kufanyiwa *assent* na Mheshimiwa Rais kuna watu wameifanyia mchezo mchafu na Sheria imebadilishwa baadhi ya vipengele. Haya mambo ni hatari kwa uchumi kwa sababu biashara ya utalii, uwindaji ni biashara kubwa, ina *interest* ya Mataifa makubwa, ina *interest* ya wawekezaji wakubwa. Uchakachuaji umefanyika kwenye Sheria. Kwa hiyo, Sheria hii, pamoja na kwamba, dhana yake ya msingi ililenga kuweka misingi ya kulenga na kujenga wazawa, lakini bado Sheria hii imefanyiwa uwanaharamu amba sio mzuri kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake ni nini? Miongoni mwa migogoro ambayo iko kwenye Sheria hii, wakati Sheria hii inawalinda sana wazawa ambalo ni jambo jema na mimi nasapoti Wazawa wasaidiwe katika kuingia kwenye biashara hii. Lakini sio tuwalinde wazawa kwa kuwafukuza wageni amba wameshawekeza mapesa na mapesa mengi katika uchumi wa Taifa letu. Tuongeze nafasi ya wazawa, kama ni lazima wazawa waingizwe kwenye makampuni ya kigeni basi tuwapandishe wazawa wetu, wasiwe na 20% kama wana uwezo wapandishwe waende 40%, *why not?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tusifukuze utaalalm! Tusifukuze ujuzi! Tusiwe Taifa lisiloaminika! Kwamba, wawekezaji wa biashara ya kitalii wamepewa vibali chini ya *Tanzania Investment Act* ambayo ni Sheria ya mwaka 2004, inafika mwaka 2009 tunabadilisha Sheria, tunaanza Sheria ambayo tunaitaka *i-act retrospectively!* Yaani Sheria itungwe leo, ianze kurudi nyuma kuanza kutumika na kufuta vibali nya watu; tutashitakiwa katika Mahakama za Kimataifa, tutalipa fedha nyingi bila sababu za msingi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu. Serikali iliangularie jambo hili kwa makini sana. Huu mgongano wa Sheria ukaangaliwe, ukiangalia Sheria mbili, vifungu mbalimbali vinagongana katika Sheria hii, ni vema mambo haya yakaangaliwa ili hii biashara ya utalii ikawa na tija kwa Taifa letu na isije ikaenda kuharibu biashara na mahusiano yetu katika jamii ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kwa sababu naona muda unakwenda kwa kasi sana, ningehitaji nusu saa na ni vema tukabadihisa Kanuni, Kiongozi wa Upinzani apewe muda zaidi kama Waziri Mkuu anavyopewa angalau nipewe nusu yake, hii mnani-*limit!* (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Mlima Kilimanjaro. Ndugu zangu, Mlima Kilimanjaro unaingiza mapato makubwa sana katika nchi hii. 99% ya wanaopanda Mlima Kilimanjaro ni hawahawa wageni tunaowanyanyaapaa. Tunatengeneza dola milioni 40 kwa mwaka kwa Mlima Kilimanjaro, ni fedha nyingi sana kwa chanzo kimoja cha utalii. Lakini *KINAPA*, *TANAPA* na Mheshimiwa Waziri, ule Mlima umejaa kinyesi, samahani kwa kutumia lugha hii! Kwa maana ni kwamba, kwa wastani kila mtalii mmoja anayepanda Mlima, anapanda na *Porter* watatu. Kwa wakati wa *season* kama hii, wageni wanaweza wakapanda mpaka wageni 300. Wageni 300 maana yake ni kwamba wageni 300 unazidisha mara *porter* watatu, ina maana watapanda wapagazi 1,200 wasiopungua 1,200 na watalii 300 wanakuwa 1,500 wanapanda mlima kwa siku. Leo wanapanda 1,500 kesho wanapanda 1,500, kila siku 1,500 na wanatumia siku tano mpaka saba kushuka Mlimani, ina maana kwa wakati mmoja Mlima una watu karibu 10,000 wanaopanda mlima na wanahitaji huduma, hakuna vyoo!

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wanajisaidia porini, vyoo havitoshi! *KINAPA* wanashindwa kujenga vyoo! Huduma kama hizi tunatia aibu kwenye Jumuiya ya Kimataifa, tunashindwa kujenga vyoo! Tuna mapato ya \$40,000,000 tunashindwa kujenga vyoo! Watanzania tuko wapi? Matokeo yake sisi tumefanya *research, research* ipo, maji katika Mlima Kilimanjaro leo ni maji yenye kinyesi. Mvua zinaponyesha maji haya yanatiririka kuingia kwenye vyanzo nya maji wanayotumia wakazi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *research* ya maji imefanywa na *Moshi Urban Water Supply and Sewage Authority* tangu 2009, nitampatia Mheshimiwa Waziri. Watu wanajisaidia porini! Watalii wanajisaidia porini! Tuna watu 10,000 katika Mlima, tunashindwa kuwajengea vyoo! Hebu fikiria kinyesi cha watu 10,000 kwa siku ni kilo ngapi za mzigo? Halafu kinyesi kile kinaachiwa kinatiririka, matokeo yake ma-*porter* wanaanza kupata *diarrhoea*, vyanzo nya maji nya Mlima Kilimanjaro vinachafuiliwa na Serikali ipo! *KINAPA* ipo! Mnakusanya mipesa, hatujui mnapeleka wapi pesa! (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunasema nini? Mazingira haya kama hatukuyafanyia kazi, Mheshimiwa Waziri nitampa hii ripoti, haya ni mambo ya aibu. Ukienda katika Mlima ule, watalii hawana mahali pa kujisaidia! Hakuna *dining facility!* Sasa watu wanasema tupunguze watalii! Kupunguza utalii ni kupunguza mapato! Tufanye nini? Ni lazima tubadilishe *strategy* zetu za kupandisha watu mlimani, kwa mfano, kabla kengele haijalia, tunapandisha ma-*porter* wengi ambao wana-*pollute* Mlima pamoja na watalii, kwa sababu hatuna *facility* mlimani. Ni vema sasa *KINAPA* ikatufikiria kuweka *centres* ambako *facility* maalum kama *tents* na vitu vingine vinapatikana kulekule mlimani, kupunguza idadi ya *porters* wanaopanda. Sasa hivi kupanda Mlima Kilimanjaro, wanapanda watu wanne kwa pamoja! Zile *route* zimeshapanuka sana, tunaua mazingira ya Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuwapunguza watalii ni kupunguza mapato ya Serikali! Sishauri, nashauri tupunguze wapagazi, lakini tupunguze wapagazi kwa kufanya nini, tufanye ku-air

lift zile huduma zote muhimu, vyakula, ma-tent, mambo ambayo yanaweza kuwa air lifted na helicopter, tukaweka centre mbalimbali katika Mlima, ambako tunaweka zile huduma zote, wale ma-porter wakifika ama makampuni ya tour yakifika pale yanachukua zile facility wanakwendanazo, wanapunguza idadi ya porters amba ni lazima wapande mlima. Tunajua tunahitaji kutengeneza ajira lakini tutengeneze ajira in a sustainable manner, sio kutengeneza ajira kwa kuua mazingira na environment ya Mlima Kilimanjaro. Hilo ni suala ambalo mkitaka utaaliam wangu, mnaweza mkanishirikisha nikawapa bure ushauri wa bure. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ambalo ningependa kulizungumza hapa katika huo mlima, ni kuhusu hawa watu amba kazi yao ni kulinda ule mlima. Yaani kuna watu amba wanakaa mlimani mle, yaani ma-ranger wale, ma-ranger wanakuwa assigned kukaa mlimani kwa siku kumi. Wanafanya kazi ya ku-rescue na kila mtalii analipiwa dola 20 kwa ajili ya rescue, lakini KINAPA hawa-rescue wageni hawa kwa sababu ma-ranger amba wana kazi ya ku-rescue wanakuwa hawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui mtabadilisha Kanuni kidogo? Naomba kutoa hoja, ahsanteni sana. (Makof)

MHE. ZAKIA H. MEGHJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Moja kwa moja napenda kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Timu yake nzima kwa kuleta bajeti hii ya mwaka 2011/2012. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nitachangia katika maeneo mawili, muda ukiniruhusu nitaendelea katika maeneo mengine. Maeneo haya kwanza kabisa ni juu ya utangazaji wa utalii na sehemu ya pili ni eneo la mafunzo na ubora wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kusema kwamba, tutambue utalii ni bidhaa. Ni bidhaa kama vile bidhaa nyingine ambayo tunauza. Kwa hivyo, kwa upande wa Tanzania, bidhaa hii ya utalii tunayouza ni bidhaa ya wanyamapori, bidhaa ya fukwe, bidhaa ya Mlima Kilimanjaro na kadhalika. Kwa maana hiyo, ili bidhaa hii iweze kuuzika na ili wateja wawewe kuiunuu, kwa maana ya watalii au wale wanaoingia nchini, inabidi bidhaa hii kwanza iwe katika hali nzuri na ya kupendeza na bidhaa hii iwe haijachafuliwa au haichafuki. La pili ni kwamba, bidhaa hii ambayo mara nyingine ni huduma, inabidi huduma hii tunayoitoa iwe nzuri na ya kumpendeza mteja ambaye ni huyu mtalii. Tatu, bidhaa hii ni lazima iwe endelevu, yaani sustainable, iweze kuendelea. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii kwa sasa hivi unachangia zaidi ya 17% ya pato la Taifa na inawezekana kabisa kwamba, ikaweza kuchangia zaidi ya hapa. Kama nilivyosema kwamba, utalii wetu ni lazima uendelee, sustainable, ndio maana sishangai wakati ule ambapo ilisikika kwamba, Serikali labda ingeamua kujenga barabara ndani ya Serengeti, watu walihamasika na wakapiga kelele. Tunashukuru kwamba, Serikali imesema haitajenga barabara hiyo ya lami, lakini hata hiyo barabara ya changarawe itabidi iangaliwe, kwa sababu Serengeti ni nini? Serengeti tunapozungumza zaidi, watalii wanakuja kuangalia ni uhamaji wa nyumbu, yaani migration of wilderbeast. Kwa hiyo, kama barabara hii itajengwa, kama ni ya changarawe na itaingilia mapitio haya ya nyumbu, basi tujue kwamba hatuna Serengeti. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama watalii wanakuja kuangalia tu wanyama, basi wangeweza kwenda Manyara, wangeweza kwenda Katavi, wangeweza kwenda Ruaha, lakini huku wanakuja hasa hasa kuangalia migration! Uhamaji wa nyumbu kila mwaka mara mbili kutoka Tanzania kwenda Masai Mara, ambayo iko Kenya na kurudi tena Tanzania. Kwa hiyo, hili naomba wakati maamuzi yanafanyika suala zima la kuangalia athari ya mazingira ifanyike kwa uwazi na kwa ukweli kabisa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nasema nizungumzie ni juu ya kutangaza utalii wetu. Ili kivutio kijulikane ni lazima ukitangaze. Utangazaji wa utalii unahitaji fedha. Sasa tunaona kwamba, kwa upande wa Tanzania, fedha ambazo zinawekwa katika utangazaji wa utalii ni ndogo sana! Mwaka hadi mwaka ni ndogo sana na hata mwaka huu pia ni fedha ndogo

sana. Ndio maana mara nyingi sana tunaanza kulalamika kwamba, ooh, Kenya wanatangaza Mlima Kilimanjaro, njoo Tanzania kupanda Mlima Kilimanjaro na kadhalika. Lakini ukiangalia bajeti yetu na ukafananisha kwa mfano, na nchi ya wenzetu, nachukua hapa takwimu za utangazaji utalii au *marketing* kwa ujumla wake, kutoka 2009 mpaka 2011, kwa miaka mitatu. Ukichukua bajeti ya Kenya, ya Afrika Kusini, ya Tanzania, sasa tuangalie; Kenya ukichukua kwa bajeti hiyo ya 2009 mpaka 2011 unakuta kwamba Kenya imetumia mara tano ya fedha tunazotumia sisi Tanzania kwa ajili ya *marketing*, kwa ajili ya utangazaji! Wakati Afrika ya Kusini, imetumia mara 35 ya fedha ambazo tunatumia kwa utangazaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo wastani wa miaka mitatu kwa dola za Kimarekani, natoa dola za Kimarekani kwa sababu, tukichukua shilingi inatofautiana kwa nchi ya Uganda, Tanzania na Afrika Kusini. Unakuta kwamba, Afrika ya Kusini, dola milioni 230.1, Kenya dola milioni 29.7 lakini Tanzania tuangalie dola ngapi? Dola milioni 6.3! Hailafika hata dola milioni10! Kwa vyovypote vile, pamoja na utajiri wetu, wanyamapori, fukwe na kadhalika, hatutaweza kushindana na nchi ambayo inatumia mara tano au mara 35 ya fedha katika kujitangaza. Siku zote Tanzania tutakuwa tunalamika na hatutaweza kuuza bidhaa hiyo. Kwa hiyo, nashauri kwamba kuna haja ya kuongeza fedha hizi hasa kwa sababu, utalii kama tulivyosema unachangia kama 17%, lakini unaweza kuchangia zaidi ya 17%. Kwa hiyo, tunategemea mwaka kesho fedha ambazo zitatengwa kwa ajili ya utangazaji wa utalii, kwa kweli ziweze kuongezwa hasa ukichukua kwamba, sasa hivi tuko katika soko la Afrika Mashariki. Kwa hiyo, kwa vyovypote vile tutapitwa na wenzetu ambao wako katika soko la Afrika Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni juu ya mafunzo na ajira kwa Watanzania katika sekta ya utalii. Hapa tumekuwa na kilio kikubwa sana, Wabunge wanazungumza kwamba, kuna baadhi ya mahoteli na tasisi mbalimbali za utalii zinaajiri watu kutoka nje! Lakini tuijulize, ni kwa nini wanafanya hivyo? Ni kwa nini wanaajiri watu kutoka nje na sio Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua kwamba, hakuna mwenye biashara atakayetaka kuajiri mtu ambaye hamuongezei faida au hamuongezei thamani. Watu wengine wanasema hii biashara inakuwa biashara kichaa! Mtu ambaye havutii wateja! Wewe unahudumia wageni, uko umenuna *kwelikwelii!* Hata hutabasamu hata kidogo! Wewe unahudumia mgeni kwenye mgahawa, unaweka supu inamuangukia mteja kwenye koti lake au katika gauni lake zuri kabisa! Wewe uko mbele pale, *front desk* hotelini, anakuja mgeni umenuna kabisa! Kwa kweli, haiwezekani na hakuna mtu yejote ambaye atakubali kwa maana hiyo, kumwajiri tu kwa sababu ni Mtanzania, eti Mtanzania, hakuna uzalendo wa aina hiyo! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tukiingia tunavyokuwa katika soko hili la Afrika Mashariki, napenda tuangalie pia kwa sababu hapa tunazungumzia *Skills development levy*. Ili kuweza kuimarisha uwezo, *skills* kwa watu mbalimbali, sasa unakuta kwamba huku nyuma kulikuwa na *skills development levy* ya 2% ambayo ilikuwa inakwenda *VETA*, 4% ilikuwa inabaki Wizara ya Fedha. Of course matumizi yake yalikuwa tofauti! Sasa hivi kwa mwaka huu, katika 6% hili, tumeambiwa kwamba 2% itakwenda *VETA* na 4% itakwenda kuwalipa wanafunzi. Hii ni *skills development levy*, ya kuongeza ujuzi; kulipa 4% sio kuongeza ujuzi, lazima tuelewe. Ukilipa pia 2% ile *VETA*, unakuta kwamba katika hii 2% hakiendi chochote kile kwenye sekta ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie kwa upande wa nchi pia, nilitaka kuangalia katika hii *skills development levy* katika nchi mbalimbali. Ukiangalia Kenya, Malawi na Afrika ya Kusini, kuna utaratibu wa *skills development levy* kwenda kuendeleza sekta ya utalii. Nchi ya Kenya, nchi ya Malawi na nchi ya Afrika ya Kusini, Kenya ndio jirani yetu, ndio sehemu ya Afrika Mashariki; wao wana utaratibu, Tanzania hatuna utaratibu! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Kenya 2% inawekwa kutokana na mauzo yote katika mahoteli, migahawa, baa, na kadhalika. Hizi fedha zinakwenda kwenye mafunzo katika kukuza vipaji ili wale wanaotoa huduma katika sekta ya utalii, waweze kutoa huduma ya hali ya juu. Kwa hiyo, fedha hizi zinakwenda huko. Upande wa Afrika Kusini, nao pia wanayo *skills development levy* ambayo waajiri hulipa 1% ya mishahara yote ya wafanyakazi wa nchi na fedha

hizi baadaye huzitumia katika kukuza vipaji na huduma inayotokana na biashara zao na kwa utaratibu maalum, Malawi nao wanao utaratibu kama huu. Tujulize, Tanzania itawezaje kutoa ushindani katika huduma za utalii kama hauna utaratibu wowote wa aina hii? Ningependa kwa kweli kuishauri Serikali kwamba, kwa utalii huu ambao unachangia zaidi ya asilimia 17 ya pato la Taifa, basi suala hili liangaliwe na tunaweza kujifunza kwa wenzenzu wa Kenya, Afrika Kusini na upande wa Malawi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda unakwenda. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. JOYCE J. MUKYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia na mimi siku hii ya leo. Hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu, afya hata nimeweza kusimama saa hii. Vilevile nashukuru Chama changu CHADEMA kwa kuniwezesha kunipitia Mkoa wa Arusha kuingia katika Bunge lako hili Tukufu. (*Makofii*)

Pili, napenda kuwashukuru wazazi wangu kushirikiana na mimi moja kwa moja kunipa ushauri hata nimeweza kufanya vizuri katika mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika Wizara hii kuanza na sehemu ya uchimbaji wa madini katika mbuga zetu za wanyama. Mimi sijalipenda hili wala sijalifurahia kabisa na naungana moja kwa moja na Kambi yangu Raskmi ya Upinzani Bungeni, kwa kukemea uchimbaji wa madini katika mbuga hizi za wanyama, kwani zinashindwa kuwapa vizazi vijavyo kuja kuona wanyama hawa ambao Hayati Baba wa Taifa aliweza kutusaidia hadi sisi tukaweza kuviona hadi sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napinga harakati hizi kwani sheria yetu mpaka sasa hivi hairuhusu uchimbaji wa madini katika mbuga zetu za wanyama, kwa hiyo, inakiuka kabisa utaratibu ambao umewekwa na sheria zetu za nchi hii. Sawa mmeshapima, wataalam wameshapima na kuona kwamba kuna madini katika mbuga za wanyama, nakubali kwamba kuna madini katika mbuga za wanyama, lakini mnaua wanyama, kunakuwa hakuna tena utaratibu ambao utaweza kuonyesha vizazi vijavyo kuweza kuona wanyama hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mbuga ya *Selous* mmeamua kugawanya sehamu ambayo itakuwa inachimba *uranium* ambayo itakuwa ni muhimu kwa ajili ya umeme. Naomba nirudie, nakubaliana na nyie kwamba mmepima katika mbuga zetu za wanyama na kuona kuna madini, kwa mfano, sehemu ya *Selous* ni madini ya *uranium* ambayo yatasaidia katika suala zima la umeme, lakini naona kwa sasa hivi mchakato huo usimamishwe, kwani hakuna wazawa ambao wanaweza kufanya kazi hii, kwa sababu nchi yetu ina madini mengi ya kutosha, tumeona madini mengi sana, lakini bado yanaonekana kwamba yanatoka nje ya nchi, kwa mfano nchi ya Kenya, *Tanzanite* inaonekana haitoki Tanzania kwa sababu hatuna wazawa ambao ni wachimbaji wazuri. Kwa hiyo, madini hayo yakichimbwa, tukiruhusu sehemu hizo zichimbwe madini yatapelekwa nje zaidi na tutaonekana Tanzania hatuchimbi madini ya *uranium* bali yanatoka katika nchi nyingine za nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nje katika suala la usafirishaji wa wanyamapori na nyara za Serikali kipeleka nje. Hili pia limenisikitisha sana kwa sababu wanyamapori wanasaferishwa kuititia katika uwanja wa Kilimanjaro *Airport*, kuna ulinzi wa kutosha katika uwanja ule, Serikali ipo, inaangalia, lakini wanyama wale wameweza kusafirisha kuititia katika uwanja ule. Hii ninakemea ni Serikali kwa sababu ilikuwa ikishirikiana nao moja kwa moja, wameshindwa kuangalia, na mbali ya hivyo, kuna viwanja vingine vidogo vidogo katika viwanja vyetu katika mbuga za wanyama. Naamini kabisa kwamba katika viwanja vile vidogo vidogo vya mbuga za wanyama, wanyama hao wamekuwa wakisafirishwa kwa wingi sana bila sisi kujua, na Serikali haiko makini ndiyo maana hata wanyama wameweza kusafirishwa kwa kiwango kikubwa. (*Makofii*)

Kama siyo waandishi wa habari na baadhi ya watu kujua suala hilo la kusafirisha wanyama kuititia uwanja wa Kilimanjaro *Airport* mpaka leo Serikali hii isingejua kama wanyama

wanasafirishwa kupitia uwanja wa Kilimanjaro. Kwa hili, naomba niwapongeze Waandishi wa Habari na wote ambao wameshirikiana nao moja kwa moja katika kufanikisha suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uwanja ambao unaitwa Cleenso kule Loliondo. Uwanja huu umekuwa ukitumika zaidi katika kusafirisha wanyama hawa, labda Serikali nafikiri imekuwa ikishirikiana nao, na uwanja huu Serikali ilisema ufungwe, lakini juhudhi zinaendelea katika kuufungua uwanja huu ili waendelee kufanya uhalifu huo ambao wamezoea kuufanya. Naomba Serikali ishirikiane na watu wa maliasili, ili uwanja huu uendelee kufungwa na wanyama hao wasiendelee kusafirishwa kupitia uwanja huo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja huo ni kilomita chache kutoka nchi ya Kenya, na wageni wamekuwa wakiingia kupitia Kenya kuingia katika uwanja ule kuchukua wanyama na kufanya mambo mengine ambayo siyo mazuri katika uwanja ule. Kwa hiyo, imekuwa ikihariblu maliasili za Tanzania ikichukua wanyama wetu bila wenyewe kujua. Suala hili nalikemea kwa kiasi kikubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la ujenzi holela katika mbuga zetu za wanyama. Tumekuwa tukiwalika wawekezaji wenyewe, tumekuwa tukiwakubalia kupitia katika sheria zetu lakini wawekezaji hao wamekuwa wakijenga kiholela katika mbuga za wanyama wetu na kufanya wanyama waweze kuondoka na kuhama kwa kiwango kikubwa sana.

Naomba zitumike mbinu za kutumia tenti katika sehemu za mbuga za wanyama, kwa sababu tenti zile ni za muda tu, wakishahama, hata kama ni baada ya miaka mitano, nyasi zitaota, mazingira yatakuwa mazuri kuliko wakijenga magorofa na nyumba ambazo ni kubwa ambazo zinaua kabisa sehemu zile. Mfano, katika uwanja wa Kilimanjaro wa *KIA*, zamani ilikuwa ukipita pale barabarani unaona wanyama wakipita barabarani, lakini sasa hivi kwa sababu watu wameshamisha makazi katika sehemu ile, huoni wanyama wala huoni tembo, wala zebra wakivuka barabara. Hii yote ni kwa sababu makazi yameingiliwa. Kwa hiyo, maliasili zetu zinakuwa zinakimbia, zinahamia sehemu nydingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la matumizi mabaya katika *TANAPA*. *TANAPA* imekuwa ikitumia matumizi makubwa sana katika safari zake, katika vikao vyake vinavyofanywa kila siku na imekuwa ikishirikisha watu wengi sana, mtu akijisikia hana hela anawasiliana na watu, wanafanya kikao na wanalipana hela nyingi ambazo siyo sawa na inavyopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la kuimarisha sera za utalii na uchumi kwa wananchi katika sehemu zenyet vivutio vya utalii. Naomba Serikali isaidiane na Wizara ya Maliasili iwasaidie kufundisha wananchi au kutoa vipeperushi vya kueleza vivutio vya utalii vya nchi yetu mfano mlima Kilimanjaro. Watu wengi wanafikiri mlima Kilimanjaro unapatikana katika nchi ya Kenya na hata wageni wanaotoka nje, wamekuwa wakienda kuangalia mlima Kilimanjaro kupitia nchi ya Kenya. Kwa hiyo, naomba Tanzania iweze kuwa na elimu kwa watu wake na iweze kuwa na elimu hiyo pia kwa nchi za nje na kupitia *internet* na kupitia vitu vingine ambavyo vinaweza kusaidia waweze kuingia katika mlima Kilimanjaro na nchi yetu iweze kupata faida. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Safi sana. Zima *microphone*.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joyce Mukya, umejitahidi, sote tulianza hivyo hivyo. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu hauturuhusu kwa mchangiaji mwingine kuongezeka, tutaendelea jioni na wale waliochangia mara moja, na uchangiaji wetu utaendelea, kama nilivyosema orodha yangu imesheheni kweli kweli. Kwa hiyo, nitawaomba kila anayepata nafasi kama atawenza kuokoa dakika mbili au tatu kwa mwenzake au kwa wenzake itakuwa ni jambo ambalo tunalikaribisha sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye Bunge la Tisa, mimi nilikuwa ni Mwenyekiti wa Ardhi, Maliasili na Mazingira ya Bunge, na pamoja na wenzangu, tulifanya kazi kubwa. Moja ya kazi tuliyoifanya ni kuanzishwa kwa Sheria mpya Na. 5 ya mwaka 2009, ambayo ilitoa *pass* kubwa sana kwa Watanzania katika kuwekeza na kufanya shughuli katika *industry* hii ya utalii.

Pili, jambo ambalo tulifanya katika sheria ile, tuliweka sharti ya kwamba paanzishwe mamlaka ya wanyamapori Tanzania (*Tanzania Wildlife Authority*). Matatizo mengi sana ambayo yanaongelewa hapa yanayohusu wanyamapori, kama pangkuwa na imani hii kwa wote wanaohusika, tukaharakisha mchakato wa kuanzisha taasisi hiyo *Tanzania Wildlife Authority*. Sehemu kubwa sana ya matatizo yanayoikumba hifadhi zetu na wanyamapori ambao wako nje ya *TANAPA* na Ngorongoro tungeweza kutatua. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nimesema haya kwa vile wataalam wote wa Idara na Wizara mpo hapa, matarajio yangu, Kamati ambayo mmechukua nafasi kwetu, kila mtakapokutana na Wizara hii agenda ya kudumu itakuwa mmeifikia wapi katika kuanzisha mamlaka? Msipofanya, mtatuletea tu kila siku hotuba za kulalamika. Wenzenu tulishayaona tukayawekea msingi huo. Hakikisheni mamlaka inaanizishwa na haiwezi kuanzishwa kama Kamati hamkushiriki jambo hilo lifanyike. Haitakuwa, nawaambia niko hapa, lakini Kamati mkishirkiana na Bunge tukawaunga mkono mamlaka hiyo katika muda wa miaka miwili, hivi inaweza ikaanzishwa.

Mwisho, naomba niwatambue Wenyeviti wa Bodi ambao tuko nao hapa katika Wizara hii, nao ni pamoja na Mwenyekiti wa Shirika la Makumbusho ya Taifa, Dkt. Constancia Rugumamo, karibu sana. Pia tunaye Mwenyekiti wa Shirika la Hifadhi za Taifa *TANAPA*, Modestus Lilungulu, wamekosea walioniandikia, karibu sana. Tunaye Mwenyekiti wa Taasisi ya Tafiti za Misitu Tanzania (*TAFORI*), Prof. Emmanuel Luoga. Tunaye Mwenyekiti wa Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (*Tanzania Wildlife Research Institute*) - Prof. Gabriel Mbassa. Pia tuna Mwenyekiti mpya wa Mfuko wa Hifadhi ya Wanyamapori Tanzania, unaoitwa Tanzania *Wildlife Protection Fund*, ndugu Michael Mwanda, karibu sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge kwa kufikia hapo na kwa kuwa muda wetu hauturuhusu tuweze kuendelea, naomba nisitishe shughuli hizi hadi saa 10.00 jioni ya leo tutakapoendelea na uchangiaji. Nawakumbusha Wabunge wa CCM kuelekea kule mlikoitwa na Katibu wenu Mheshimiwa Mhagama.

(*Saa 7.11 mchana Bunge lilitfungwa mpaka saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 Bunge lilitrudia*)

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na sasa naomba niwaambie kwamba kwa Mbunge atakayekuwa ni zamu yake kuzungumza akawa hayupo, basi zamu yake itakuwa imeshapita. Kwa hiyo, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kuwa mchangiaji wa kwanza, na Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo atafuatia.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kushukuru kupata nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika kipindi hiki cha mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie kauli yangu ambayo huwa naizungumza mara kwa mara hapa Bungeni. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba ya bajeti aliyotupa asubuhi, lakini naomba niseme ukweli zaidi kwamba naishukuru Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambayo imechambua vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wao ni mzuri sana na ninaomba niisihi Serikali kwamba ninyi na sisi ni kitu kimoja. Kamati ikichambua jambo vizuri, chukueni. Wabunge wakichangia hoja ambazo mnaona zinainsidia nchi, chukueni kwa sababu wote hatuwezi kutazama jambo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niirudie kauli yangu ya kusema kwamba Tanzania siyo maskini! Tanzania siyo nchi maskini hata siku moja! Ukitesema Tanzania ni nchi maskini utakuwa unakosea. Tanzania ni katika nchi ya Afrika kama siyo nchi tano au kumi ambazo zina utajiri na zina raslimali za uhakika, sidhani kama nitakuwa nimekosea nikisema iko katika nchi kumi bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matatizo sisi wenyewe kama nchi, hatulindi raslimali zetu vizuri na sijui huu ugonjwa umetoka wapi! Unanisumbua sana. Raslimali za Tanzania hazilindwi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba Serikali kwamba Mheshimiwa Waziri wakati atakapokuwa anatoa majamuisho yako, uwe makini sana ujue kuwaeleza Watanzania kuhusu ukurasa wa nane wa kitabu cha Kamati juu ya utoroshwaji wa wanyama Novemba, 2010. Mtaani huko kuna vurugu sasa, wananchi wanataka kujua hili limetokea kweli? Kama lilitokea, lilitokeaje? Kama lilitokea, Serikali ilikuwa wapi? Wanataka kujua kama kweli lilitokea, hawataki mtu ashitakiwe bali wanataka wanyama wale warudi. Ndiyo maneno yaliyopo mitaani kama kweli lilitokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze moja kwa moja jambo ambalo limenikera sana. Hii lugha sikuilewa. Lugha ya mgomo wa wenye hoteli za kitalii zilizopo ndani ya Hifadhi kukataa kulipa tozo, yaani *concession fees*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hii lugha siiilewi! Naomba niseme lugha kama hii mimi huwa sina! Mimi huwa sina katikati, hapana! Mimi nina kushoto au kulia, lakini katikati sina! Nikiwa nina maana gani? Nina maana kwamba Serikali inapaswa iwe na msimamo unaoeleweka. Serikali inapaswa isiyumbe. Inapoamua jambo, Serikali isimamie ilichoamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *concession fee*, ni haki yetu ku-charge *concession fee* tunayoona tunastahili kwani ni haki yetu. Mimi ninawaambia hakuna kitu kizuri kama utandawazi. *Nam-support* Mheshimiwa Freeman Mboge, hakuna kitu kizuri kama *globalization*, lakini itategemea mko makini kiasi gani. Ukitesema vitabu vya *globalization*, mataifa makubwa yanafaidi *globalization* sana, lakini mataifa madogo ambayo hayako makini yanaumizwa na utandawazi. Hivi na sisi tunatakiwa tuitwe Taifa ambalo haliko makini!

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vitutio vingi, tuna raslimali na pia tuna mbuga za wanyama. Watalii na wawekezaji tunawaita, njooni, tunakubali utandawazi. Lakini katika utandawazi kuna kitu kimoja kikubwa sana. Wewe unayekwenda kuwekeza kwenye nchi ya mwenzako, unatakiwa ukifika kwenye ile nchi ufuate sheria na *regulations* za ile nchi. Lakini na ile nchi ambayo mmewakaribisha wawekezaji msimamie *regulations* zenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007 aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii -Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe alikuja na *concession fee* hapa. Ile *concession fee* iliweza kutuungezea pato kwenye hii Wizara kwa asilimia 17.2, akaingia Waziri mwingine akai-suspend *concession fee*. Sijui tunakwendaje! Alipoingia akai-suspend tukapata upungufu wa pato kwenye Wizara kwa asilimia 14.4. Sasa Serikali naomba msimame imara, Mheshimiwa Waziri simama imara, ngoja nivue miwani! Mheshimiwa Waziri umekuja na *concession fee* mpya, simama hapo hapo. Bunge lote hili tutakuunga mkono. Ukitetereka tunakuondoa, simama hapo hapo! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya 1990 walikuwa wanatoza kwa kitanda kimoja Dola 100 mpaka 150 kwenye hoteli hizi ambazo miundombinu yote ni sisi tunaishughulikia. Wakawa wanatupa *concession fee* ya less than 10 dollars. Sasa shauri ya kwamba wameona utendaji, utekelezaji na kila kitu kimepanda wanatoza kuanzia Dola 450, Dola 500 mpaka Dola 1000, eti wanataka sisi tuendelee kupokea tozo la Dola 10. Hivi sisi ni wapumbavu kiasi gani? Ni lazima tupandishe, ni lazima twende kama wanavyokwenda wao. *Concession fee* tuliyosema twende nayo aidha ni 60, Mheshimiwa Waziri usisogee hapo, simama hapo hapo. Tunakwambia tunakuunga mkono tena usidhani tunatereka, labda utetereke wewe, na ukitetereka wewe tunakuondoa!

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesimama imara na tunaomba hawa wawekezaji wajue kwamba Bunge limeamua na wajue kwamba hatutaki mchezo. Hawa Serena na mwenzake wanapita wanazungumza kwenye hoteli wanasema kwamba tukatae na wanawashawishi wenzao. Tunaomba leo wasikie kwamba na sisi tumekataa. Tunataka *concession fee* ambayo imepitishwa ndiyo twende nayo. Hivi wanaionaje Tanzania, ni nchi ya kuja na kuvuna na kuondoka! Hapano! Ni nchi ambayo ina Watanzania wenye akili timamu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia Wazungu hawa amba wanafanya *tented camps*, wanatulipa Dola 50 mpaka 60. Mbona hawa Wazungu hawajatusumbua? Hawa wenye hoteli ni akina nani, kwamba sasa eti wamechachamaa wanakataa? Aah! Wasitutawale! (*Makof!*)

Jamani, mnanifanya nisisikike. (*Makof!*)

Wakiona hawataki *regulations* zetu wafungashe, waondoke, *tuta-run* hoteli wenyewe. Lakini Mheshimiwa Waziri, naomba nikwambie, simama imara na ukisimama imara usimame hapo hapo, hakuna kuwa katikati. Unakuwa katikati kwani wewe mzoga? Kuwa katikati ni kwamba mtu Jumatatu umesimama kushoto na Jumanne umesimama kulia. No! Simama imara na Serikali isimame imara, Wabunge tupo imara, *concession fee* haitabadilika, kabisa! Anayeona haitaki, jamani aondoche, mbona watu wako tayari kuendesha zile hoteli! Nafikiri hapo nimeeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupe hii *document*, nitai-table hapo kwako.

NAIBU SPIKA: Hiyo ni kengele ya kwanza Mheshimiwa Anne K. Malecela, nakuthibitishia Bunge hili tuko na Mheshimiwa Waziri, *concession fee* iko pale pale!
Mheshimiwa endelea! (*Makof!*)

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Pale pale! Ahsante! (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ni-table hii karatasi mbele yako na imflikie na *Chief Whip*. Nnakusomea. (*Makof!*)

Hii nimeletewa kutoka *Serengeti National Park*, tarehe 1 - 3 Agosti, 2011 kuwa *concession fee* mpya tumekusanya Dola 110,841 lakini kwa *concession fee* ya zamani ingetuchukua miezi sita. Sijui mmenielewa! Hii ingetuchukua miezi sita. Naomba ifike mbele, vijana chukueni mpelekeni Naibu Spika mpaka na *Chief Whip* aipate.

(*Hapa barua husika iliwasilishwa Mezani kwa Naibu Spika*)

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Waziri usirudi nyuma, tunaomba wale wenye hoteli kama hawajasikia, wasikie vizuri waondoche, wasitufanye wajinga sisi. Hilo limeeleweka. (*Makof!*)

Sasa nakuja kwenye suala la pili ambalo ameliongea Mheshimiwa Freeman Mboge. Namuunga mkono Mheshimiwa Mboge, lakini namwongezea, yaani namrekebisha kidogo. Mheshimiwa Mboge amesema tuisiwanyanyapae wawekezaji na mimi nakubali, hakuna nchi hata moja duniani inayoweza kuishi bila wawekezaji, lakini Mheshimiwa hakumalizia, hao wawekezaji wawindaji wanapokuja kwetu ni kweli hii biashara ya uwindani ni ya matajiri dunia nzima, ni matajiri ndiyo wanaoifanya hii. Lakini wanapokuja tuangalie kitu kimoja.

Naomba nitoe mfano mmoja, hakuna nchi yenyе tembo wazuri kuzidi Tanzania. Hawa wenzetu wa Kusini mwa Afrika tembo wao wanawafugwa kwenye mashamba, lakini wa kwetu wako kwenye *National Parks*, wanaishi vizuri, ndiyo ubora wa ndovu wetu sisi. Lakini utakuta wawindaji wanatulipa eti kati ya Dola 7,000 mpaka dola 13,000 kwa tembo mmoja. Lakini kule Kusini mwa Afrika *fixed rate* tembo moja Dola 20,000, *that is not fare* jamani! Waheshimiwa Wabunge tunaibiwa! Mimi nimekubali hawa wawindaji waje, lakini na sisi tunatoza kiasi gani? Twende sawasawa na wenzetu, sisi kwa nini tutoze kidogo? Kwa nini tutoze kidogo wakati tembo wetu ni bora kuliko wale wa Kusini mwa Afrika? (*Makof!*)

Mheshimiwa Waziri ukitaka kweli tukupende na uishi kwenye Wizara hii na aliyependezwa akakuweka hapo, utuingzie mapato. Wizara hii ina uwezo wa kuingiza fedha nyingi sana, ina uwezo wa kuingiza mapato mengi sana, lakini mianya imekuwa mingi mno. Hapa tayari ni mwanya. Hao wawindaji waje na wakija, tembo wetu mzuri tena amenawiri Dola 7,000, akienda Kusini mwa Afrika tembo amechoka, Dola 20,000, hapana! Haiwezekani! (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali mshirikiane na Bunge hili ili nchi hii iende vizuri. Mheshimiwa Waziri tunakuunga mkono, kwani unajitahidi kufanya kazi nzuri, simamia *concession fee*, tena kuanzia sasa tembea kifua mbele ukijua wote sisi tupo na wewe bila kujali itikadi zetu, hakuna mtu wa kukataa *concession fee* hata, anayetaka afunge mizigo yake aondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kidogo naumwa, ndiyo maana sikuweza kuwa mkali, sauti yangu imekuwa ndogo kidogo, kifua kinaniuma. Lakini katika hili la *concession fee*, kinachoniuma ni kwamba, hawa wenye hizi hoteli ndiyo hawa hawa walioua reli yetu, yaani *RITES*, ndiyo asili hiyo hiyo, ndiyo watu wanaofanana hivyo. Kwa nini wanakuja kuua nchi yetu? Mimi najaribu kuangalia, hivi ni akina nani hao wenye Serena? Nimewatafuta na kuwajua, hawa wengine wenye Sopa ni akina nani nimewajua, hawa waliokuja huku kwenye reli yetu wakaiua ni akina nani? Ni hao hao! Mbona Wazungu wanaokuja na mahema yao wanatupa Dola 60 kwenye *concession fee*? Hawa tuwaangalie, vizuri ukienda kwao huwezi kuwa hata Mwenyekiti wa Kitongoji, kwetu sisi karibu watachukua fomu za Urais. (*Makof!/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Anne K. Malecela, tunakushukuru sana kwa mchango wako na Mheshimiwa Waziri tuko pamoja kwenye *concession fee*.

Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo atafuatiwa na Mheshimiwa Salehe Pamba.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia maoni yangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, aliyoiwasilisha Bungeni kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwanza kwa sababu Mungu ametupa nchi nzuri yenye milima na mabonde, yenye wanyama wazuri wa porini, pia yenye mito na maziwa makubwa. Kwa sababu hiyo, tumeweza kujipatia biashara ya utalii ambayo kimsingi ni biashara endelevu, tunaweza kusema kwamba ni biashara ambayo haina mwisho na kama mtaji upo, siyo mtaji mkubwa sana kwa sababu tayari wanyama wapo, labda itakuwa ni mtaji wa kujenga hoteli na kutengeneza miundombinu. Kwa sababu hiyo, ninayo shukrani nyingi kwa Mungu kwamba alitupa upendeleo, akatupa nchi nzuri. (*Makof!*)

Ukiangalia katika ramani ya Tanzania, utaona mbuga za wanyama, kwa mfano, kuna Selous, Mikumi, Serengeti na Kreta ya Ngorongoro ambayo hivi karibuni Kreta hii imetangazwa kuwa ni urithi wa dunia wa UNESCO. Ni urithi ambao unaweza kuendelea kutuletea pato la Taifa na hivyo tukaweza kujikwamua katika uchumi wetu na tukaweza kuishi maisha mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna changamoto nyingi ambazo zimejitokeza katika mbuga zetu za wanyama. Tunasikia kwamba misitu iliyopo katika mbuga za wanyama inachomwa moto, kuna watu wanafanya kilimo katika mbuga za wanyama na wale wanaochoma moto tunasikia kwamba wengine wanafanya uwindaji haramu. Sasa mimi najiuliza, hivi hatuna Maaskari wa wanyamapori? Kama wapo: Je, na wao wanapokea rushwa kama Askari wa barabarani? Kwa sababu tatizo hili limekuwepo kwa muda mrefu, sasa ninaomba Serikali ifuatilie kwa karibu na kuona kwamba changamoto hizi zinapungua ili mbuga za wanyama zisiwe na usumbufu wa aina yoyote.

Pia changamoto za miundombinu zimeonekana kwa mfano katika *National Park* iliyopo Kigoma. Mkoa wa Kigoma una *park* ya Gombe, *park* ambayo ina Sokwe ambao ni wachache sana duniani na wengi wanapatikana Kigoma Tanzania na tunaambiwa kwamba ni mwanamke

Mwingereza, Jane Goodall ndiye ambaye anaiendeleza *Gombe National Park*. Lakini tatizo ambalo linaikumba au liko mbele ya park ya Gombe tunaambiwa kwamba hakuna usafiri wa uhakika. Gombe iko kilomita 16 tu Kaskazini mwa Kigoma, lakini usafiri unaotumika pale ni usafiri wa boti. Ingawa sijafika kule, lakini nina uhakika Wazungu au Watalii wanakuwa na wasiwasi na wanaogopa kupanda boti za mbao, hivyo basi Serikali langalie ni kweli kwamba Gombe haiwezi ikatuongezea kipato? Ni kweli kwamba hawa Sokwe hakuna watalii wengi ambaeo wanawenza wakavutiuwa zaidi na kuja kuangalia? Lakini tunaona ni wachache na hali hiyo inazidi kudidimiza utalii wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuongelea mali za kale. Tunaambiwa kwamba tuna mali za kale katika maeneo ya Kolo, Amboni Tanga, lakini ukiangalia mazingira ya mali kale zile na maeneo yale ambapo yapo ni hivi majuzi tulipokuwa tunakwenda Arusha, nilipita kule na tukapata bahati kuiona ile Kolo. Kwa kweli inatisha, barabara ile sio nzuri sana. Nadhani inaweza ikarekebishwa na ikatengenezwa zaidi kwa sababu nilijaribu pia kuwaauliza wananchi wanaoishi maeneo yale na wakasema ni kweli kuna watalii wachache wanaofika kule. Lakini wengine wanaogopa barabara ile kwamba siyo nzuri sana. Sijui kama ni utamaduni au haiwezekani kwamba mbuga ikawekwa lami, lakini nimewahi kusikia kwamba ikiwekwa lami eti madereva watakwenda mbio sana. Labda hiyo inaweza kuwa sababu, lakini kwa eneo kama lile lenye barabara, kona zile ambazo zinatisha pengine ikiwekwa lami sidhani kama kuna dereva ambaye akili yake sio timamu atakimbia sana mwendo kasi katika zile kona ambazo zinakwenda kwenye maeneo muhimu kama yale ya Kolo. Hilo ni pendekezo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni uzalishaji wa asali. Kwa sababu ninakumbuka wakati fulani Waziri Mkuu aliwahi kuzungumza kwamba asali ni zao zuri ambalo linaweza kuongeza kipato. Lakini nikajuliza: Je, ni kwa nini basi Watanzania hawaelimishwi? Mbona tunajua kwamba Vyombo vya Habari vina nguvu, kwa nini Wizara isitumie nguvu ile ya Vyombo vya Habari kuwaelimisha hata wakulima?

Kuna wakulima wanaoishi chini ya mlima Meru pale Sakila, Nkwaranga, Tengeru kuna miti mingi pengine badala ya kusubiri zao la kahawa mpaka wapate pato la zao lile labda wangkuwa wamening'iniza mizinga mingi katika msitu ule, pengine ingekuwa ni njia mbadala nyingine ya kuwapatia maisha bora na hivyo kipato chao kikawa juu zaidi. Hivyo, nashauri kwamba Vyombo vya Habari vitumike vizuri. Sio lazima kutumia fedha nyangi sana. Kuna vipindi vya redio ambavyo gharama zake ziko chini kidogo na pia vinaweza vikatengenezwa vipindi vya dakika kumi na tano, kumi na tano au dakika tano, tano ili kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kufanya shughuli hizo za asali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nizungumzie kuhusu utalii mbadala. Ukitisafiri katika Miji mikubwa duniani, kwa mfano ukienda London unaweza kukuta kuna vivutio ambavyo viko katika mji ule wa London na sisi Tanzania tuna Dodoma hapa, ni mji mkuu lakini nashangaa hakuna kivutio chochote cha utalii na sijui lini mtalii atafika hapa Dodoma. Lakini ukifika London kuna kitu kama *Buckingham Palace*, *Tower of London*, ukifika Paris kuna *Tower of Eiffel*, ule mnara wa *Eiffel* ambaeo unaiingizia nchi ya Ufaransa fedha nyangi, ni mnara tu. Lakini ule mnara una shughuli mbalimbali za biashara na hivyo watu hufika na kuangalia.

Sasa nilikuwa najiuliza kwa nini sisi hatuna ubunifu wa kubuni vyanya? Kwa nini tubakie na vyanya vile vile vya zamani ambavyo mababu zetu waliviacha na mpaka leo hatuna vyanya vypya. Labda *Nyerere Square* ni kivutio, lakini kwangu naona bado kipo katika ngazi ya chini. Labda vingeweza kubuniwa vivutio vya ngazi ya juu zaidi ambavyo vitasababisha mtalii aweze kufika hapa Dodoma hata na watu wa Dodoma wakawenza kuchangamka katika utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo, machache, kwa siku ya leo naomba kuishia hapo. Naomba kuwasilisha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mngodo. Nataka kukwambia kwamba kivutio kimojawapo Dodoma ni Bunge la Jamhuri ya Muungano. Sasa namwita Mheshimiwa Saleh Pamba atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Owenya.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa tatu kwa jioni ya leo. Kwanza kabisa, napenda ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na pia nimefanya kazi katika Wizara hii ambayo leo tunajadili na kufikia cheo kikubwa cha Katibu Mkuu wa Wizara. Kwa hiyo, haya ambayo nitakayoyazungumza humu ndani ni yale ambayo yatachanganya uzoefu amba o nimekuwa nao kwa miaka 33 chini ya Wizara hii pamoja na yale mengine ambayo naona kwamba tuwasaidie wenzetu wawze kwenda kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa, napenda kuchukua nafasi hii niweze kuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Kazi ya uhifadhi siyo kazi nyepesi, kwa sababu unahifadhi wenzako wanataka kutumia, unahifadhi wenzako wana shida ambayo inawafanya kwa njia yoyote lazima waingie katika maeneo ambayo umeyahifadhi. Kwa hiyo, wenzetu wa Wizara ya Maliasili pamoja na upungufu wao amba o wamekuwa nao amba o umetokea, lakini kwa miaka yote ambayo wamekuwa wakifanya kazi, wameendelea kufanya kazi nzuri, ndio maana leo tunazungumzia juu ya Serengeti, Ngorongoro, Manyara na ndiyo maana tunazungumzia juu ya misitu ambayo tunayo hapa nchini. Kazi hiyo siyo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya miaka 1960 na 1970 kulikuwa na mzee mmoja ambaye namheshimu sana anaitwa Prof. Grzmick. Yeye ni mtaalam sana wa *conservation*. Kwa hiyo, mwaka wa 1960 wakati wanaanzisha Serengeti baada ya kuona uzuri wa eneo la Serengeti, baada ya kuona idadi ya wanyama walioko wengi pale Serengeti aliandika kitabu ambacho kinaitwa *Serengeti shall not die*, nami naamini kabisa kwa kazi ambayo inafanywa na Wizara ya Maliasili mpaka leo bado tunasema kwamba *Serengeti shall not die*. Kwa sababu Serengeti ndiyo hifadhi mojawapo katika nchi yetu ambayo ni urithi wa dunia, lakini nataka niseme hivyo hivyo kwamba katika Wizara hii kuna maeneo mengine pia ambayo tunasema kwamba *they shall not die*. *Selous shall not die*, *Ruaha shall not die*, *Mikumi shall not die*. Kwa hiyo, ndugu zangu watu wa Wizara ya Maliasili na Utalii mwendelee kufanya kazi kwa sababu mnafanya kazi kubwa ya kulinda na kuhifadhi maliasili yetu kwa ajili ya vizazi vyetu na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumetokea matatizo katika kipindi hiki na matatizo haya yanaletwa na utandawazi, tamaa ya fedha, tamaa ya mali na kadhalika. Nchi yetu imechukua hatua ya kuhifadhi eneo lake asilimia 28 ya nchi yetu ili kusudi tuweze kulinda vizazi hivi. Lakini katikati tunao wananchi wenzetu amba o hilo hawalioni. Kwa hiyo, kuna uvunaji miti ovyo, kuna uchomaji moto ovyo, maeneo ya *catchment* yanavamiwa, maeneo ya misitu nayo yanavamiwa, maeneo ya wanyamapori nayo yanavamiwa, ujangili umezidi na kadhalika. Hilo halivezi kutupeleka katika nchi ambayo tunasema *Serengeti shall not die*. Lazima wenzetu wanaohusika na *conservation* pamoja na Watanzania wote na sisi Wabunge tuwaunge mkono wenzetu katika suala hili la uhifadhi, la sivyo nchi yetu haitakuwa nchi yenyе sifa kama sifa ambazo tunazipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kushauri tu, nimeangalia bajeti ya Wizara ya Maliasili kwa jinsi ambavyo uvamizi wa misitu, uchomaji wa misitu na ujangili unaoendelea katika maeneo mbalimbali ya hifadhi zetu, ningependa kuishauri Serikali kwamba wakati umefika sasa hivi wa kuanza kuchukua hatua na kuwa na operesheni maalum ya kuweza kusafisha majangili katika maeneo yetu ili tuweze kulinda hifadhi zetu. La sivyo, hatutakuja hapa kuzungumzia maeneo haya ambayo sasa hivi tunasema ni maeneo ya vivutio.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nzungumzie juu ya suala lingine ambalo ni muhimu, nalo ni suala la utalii. Kwa upande mmoja suala hili linaungana sana na hifadhi zetu, kwa sababu utalii wa Tanzania ni *Wildlife Based*, unahuksika na wanyamapori. Kama hakuna wanyamapori, Tanzania hakuna utalii. Kwa hiyo, tunahitaji tulinde hizi hifadhi ili utalii wetu uweze kuendelea. Kwa hiyo, nasema kwamba ni lazima tujitahidi kuhakikisha kwamba hizi hifadhi tunazilinda, zinakuwa katika hali ya juu ili kusudi tuweze kuimarisha utalii wetu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia juu ya suala la utalii umekuwa, tumepata dola bilioni 1,200, lakini nataka nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kwamba fedha hizi ambavyo tunazipata kwenye utalii ni kidogo. Kuna *leakage* kubwa sana ya fedha hizi za utalii asilimia 60 ya fedha za utalii zinabaki nje. Nitaeleza kwa nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wote waliojenga mahoteli, fedha zinazokuja katika mahoteli haya na Makampuni haya ya utalii ni fedha za operesheni peke yake. Kwa hiyo, tunaposema kwamba sisi tunapata dola bilioni 1,200 tunatakiwa tupate zaidi ya dola bilioni tatu au kuendelea. Sasa kuna maeneo ambayo yanahitaji yafanyiwe kazi ambayo mimi nilipokuwa katika Wizara hii tuliifanya kazi mwaka 2003. Tulifanya utafiti pamoja na Benki Kuu kugundua *leakages* mbalimbali. La kwanza kabisa ambalo linafanyika ni hili la *prepayment* hizi zinazoitwa *package tours*. Watalii ambao wanakuja wamekwishalipa huko huko, sasa kuna njia za kufanya kuweza kuzuia hii. La kwanza kabisa, ni kuweka sheria ambayo katika aina fulani ya utalii wanafanya wazalendo peke yake ili kusudi muweze kupata angalau asilimia 60 ya mapato yabaki nchini. Hilo tunasema kwamba mwende mkalifanyie kazi, mhakikishe kwamba sheria hii inarekebishwa ili kuhakikisha kwamba kuna maeneo mbalimbali ambayo yanakuwa *specific* kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ni la kiuchumi jumla, tunachotaka ni kuwawezesha Watanzania wajenge mahoteli makubwa makubwa kuanzia nyota tatu mpaka nyota tano ili kusudi fedha zinazopatikana kutokana na utalii ziwe fedha ambazo zinabaki kwa wananchi. Mahoteli yale ya Serengeti mnayosema ya Sopa, Serena yale ni mahoteli *ownership* yake ni *hundred percent* ya watu wa nje. Kwa hiyo, tuwahamasishe wananchi wetu tuwape mikopo wahakikishe kwamba wanajenga mahoteli ya nyota tatu na hoteli kubwa ili kusudi fedha zibaki ndani na hapo ndipo tutakapoona faida ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala moja la mwisho ambalo ningependa kuzungumzia, nataka kuzungumzia kifupi tu kuhusu suala hili linalohusu Sheria Na. 5 ya Uhifadhi wa Wanyamapori. Tumetunga sheria, sheria ni nzuri, lengo lake ni kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanafaidika na maliasili yao. Nasema hii sheria haina matatizo, lakini vile vile tumetunga sheria bila kuangalia mazingira ya nje, "The International Environment" au "International Economic Climate."

Kwa hiyo, nasema kwamba tuwashauri wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwamba sheria hii ifanye kazi, lakini tunapoona tu kwamba sheria hii inakuwa ni kikwazo katika kukuza utalii na uwezekezaji, basi haraka sana wala tuisubiri zaidi ya mwaka mmoja turudishe maeneo ambayo tutaweza kufanya *amendment* hapa ili tuweze kukuza uchumi wetu na kukuza utalii wetu hapa nchini. Kwa hiyo, kuna haja ya kuiangalia sheria hii na tuiangalie kwa mazingira ya nje. Kwa sababu kama tunavyosema utalii sio kwamba tunaufanya Tanzania peke yake, tunashindana na nchi nyingi. Tunashindana na Botswana, Malawi, Zambia, Kenya jirani zetu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kenya wenzetu wanapata zaidi ya watalii milioni mbili. Tusione haya kushirikiana na wenzetu wa nchi jirani ilimradi watalii milioni mbili wanaofika Kenya, watalii milioni mbili pia wafike Tanzania. Tusiwavekee vikwazo kuingia katika nchi yetu. Tunachotakiwa ni kuhakikisha kwamba sisi nasi tunafaidika na wale watalii ambao wanakuja katika nchi yetu. Kwa sababu mtalii anapotembelea duniani anataka kwenda kwenye nchi zaidi ya moja. Kwa hiyo, tunatakiwa tuondoe vikwazo, tukubaliane na Kenya, kwanza sisi tumeshaendelea, tuna vivutio vizuri, tusiwaogope Wakenya, tushirikiane nao tuhakikishe kwamba *tuna-benefit* na tunainua utalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda nirudie tena kwamba Wizara hii inafanya kazi nzuri, Wizara hii naifahamu, Wizara hii ina wafanyakazi wazuri, lakini katika Wizara au katika viazi unaweza kuwa na *rotten potato* moja, hiyo *rotten potato* moja unaiondoa siyo kwamba viazi vyote ni vibovu. Mimi nawafahamu wafanyakazi hawa, wanafanyakazi katika mazingira magumu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwape moyo ili waweze kufanya kazi na kuhakikisha kwamba hifadhi zetu hizi ambazo tumewapa jukumu zinadumu kwa kizazi hiki na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Saleh Pamba. Mheshimiwa Saleh Pamba anaifahamu vizuri Wizara hii, aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Namwita Mheshimiwa Lucy Owenya, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbarouk Salum Ali. Kama atakuwa hayupo Mheshimiwa Vita Kawawa ajiandae.

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote, naomba ku-*declare interest* kwamba mimi ni mdau katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii ni kati ya sekta ambayo inaliingizia Taifa zaidi ya asilimia 25 ya fedha za kigeni. Hivyo, ni wajibu wetu kama sisi wadau na Watanzania kwa pamoja tuhakikishe kwamba tunakuwa na utalii imara na endelevu na wenyewe kujali mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Kiongozi wangu wa Upinzani Bungeni amezungumzia kwa kirefu suala zima la usafi, nami nitasisitiza tu baadhi ya maeneo. Kwa kweli katika hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, vyoo vinatia aibu. Vyoo vile ni vya mashimo. Katika vituo vingi kule Machame Art wataalam nafikiri wanapafahamu Mti Mkubwa, Shira kote vyoo ni vya mashimo na havitoshi. Ni aibu, na watalii wengi huwa wanarudi mara ya pili kutalii, wakirudi wanakuta bado hatujachimba vyoo vingine vya kuongeza. Wizara katika Bunge la Tisa walituahidi kwamba wataleta vyoo vya majaribio kutoka Ujerumanî ambapo ni *chemical toilets*.

Ningependa Mheshimiwa Waziri atueleze mchakato ule umefikia wapi kwa sababu tukikutana na wadau wanatuuliza: Je, vyoo vinakuja? Tunawaambia vinakuja, lakini hatuwezi kusema ni lini vyoo vile vitakuwepo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba atueleze mkakati huo ulikuwa umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanapokwenda ku-*camp* kule *crater*, ni uchafuzi wa hali juu. *Crater hamna choo, crater hamna maji.* Tunalamika kwamba theluji inayeyuka, lakini wale wapishi wanayeyusha zile theluji kwa ajili ya kupikia. Ni kuchafu na kunatisha. Lakini *National Park wanachukua park fee* ya siku sita Dola 630, lakini *Ma-tour Operators* toka nje wanatoza extra kwa ku-*camp crater* katika dola 500 mpaka 1,000 kwa siku. Lakini *National Park fee* inatozwa Dola 630 tu kwa *KINAPA* kwa siku sita. Lakini wenzetu wanasema *if you want to go and climb camp in the crater you have to pay extra.* Kwa hiyo, wao wanajipatia fedha zaidi, lakini sisi tunabaki tunapata faida kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tujali mazingira ya mlima wetu, ni mlima pekee wa tofauti ambao hauhamishiki ambao hauwezi kuibwa kama wanyama walivoibiwa kule Ngorongoro. Kwa hiyo, naomba tuulinde, tuupende na Waheshimiwa Wabunge ambao hamjawahi kufika katika Mlima Kilimanjaro karibuni sana nitawapandisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mlima Kilimanjaro pale *Kibo Hat* pana nyumba za ma-*porter* zilizokuwa zinajengwa. Kwa sasa hivi nyumba zile hazitoshî, ma-*porter* wanalala nje. Tunaomba mharakishe nyumba zile zikamilike ikiwa ni pamoja na *rescue* kuhakikisha kwamba wanahudumia pia ma-*porters*. *National Park* wamejitahidi, wameweka *oxygen* pale Barafu. Lakini ile *oxygen* inatumika zaidi kwa wageni, lakini hata ma-*porter* wanapata zile *attitude sickness*. Kwa hiyo, tunaomba na wao pia wahudumiwe kama wageni kwa sababu ni wao ndiyo wanawahudumia wale wageni. Kwa hiyo, wakipata matatizo na wao wawe *treated* kama wageni wanavyokuwa *treated*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo suala la *volunteers students*. Kuna wanafunzi wanaokuja Tanzania kwa *holiday at the same time* wanataka ku-*interact* na kufanya *project work*.

Nazungumzia hawa wanafunzi, wana miaka kati ya kumi na sita mpaka kumi na nane na huwa wanakuja kati ya mwezi wa saba mpaka wa tisa na wanakuja *groups* tofauti kwa wiki nne nne. Sasa wanafunzi hawa wakija wiki moja wanapanda Mlima na wiki nyingine wanakwenda

safari za Ngorongoro na Serengeti, wiki ya tatu wanakwenda *beach life* kwa kwenda Zanzibar. Lakini ile wiki moja wanafanya *project work*. Wazazi wao huwa wanakusanya pesa, wanakuja wanunua vifaa na kutusaidia kujenga kwenye mashule. Wanaweza kujenga madarasa, wakajenga *dinning* au wakapiga rangi na kadhalika na wakija huwa wanalipa *package* yao yote. Wakipanda mlima hawaombi *discount*, wakienda safari hawaombi *discount* hata wakienda Zanzibar wanalipa *full payment* na wanalipa *visa* ya ndani ya nchi *USD 50* kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi Serikali imesema *volunteers walipe USD 500*. Mimi nafikiri *open off*, hawawezi kulipa *USD 500*, wazazi wao wanachangisha pesa kule, wanakuja wanatusaidia sisi, wanakarabati shule halafu *at the same time tunawachaji USD 500. This is not fair*. Kwa sababu kuna wale *volunteers* wanaokuja kwa miezi sita au mwaka mmoja, mimi sizungumzii na hao walipe, lakini hawa wanafunzi wanaokuja na wanaambiya walipe *USD 500* sidhani kama ni sawa.

Kwa hiyo, naishauri Serikali, maana Serikali ni moja, mkae na watu wa Uhamiaji mliangalie hili ili tusije tuka-lose hawa *clients*. Hapa ninavyoongea sasa hivi mimi tayari nimesha-lose *prominent two operators* ambaao kawaida mwezi wa Saba mpaka wa Nane tunapata wanafunzi mpaka 600. Wanunua vitu kwenye masoko yetu na ukija Moshi unakuta Wazungu wamejaa tele. Lakini sasa hivi wamekwenda Mombasa na Kenya wamewapoeka haraka sana kwa sababu wamewakubalia na wamewaaambia hawatawatoza hiyo *visa fee*. Kwa hiyo naiomba Serikali illangalie na barua tumeshaandika Uhamiaji kulalamika kuhusu hili. Ma-agent pia wamelalamika kuhusu hili kwa sababu kiasi fulani tuta-lose katika sekta hii kwa hawa wanafunzi ambaao wanakuja kutusaidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Mheshimiwa Meghji kuhusu *Tanzania Tourist Board*. Ukitaka upate lazima utangaze na lazima *u-spend*. Sasa *Tanzania Tourist Board* imepewa shilingi bilioni 4.2. Fedha hizi ni ndogo sana kwa kutangaza.

Waheshimiwa Wabunge, wakati ule tulikwenda kutangaza *CNN Wabunge* wengi walipiga kelele pesa ni nydingi, lakini kutangaza ni pesa ndugu zangu na lazima utumie. Kutangaza tangazo moja ni pesa nydingi sana. Sasa kwa hii Shilingi bilioni 4.2 mnazowapa *TTB* wakatangaze na ukizingatia kwamba tunakuja kuingia kwenye soko la *East Africa* wenzetu Wakenya wanawawezesha *Kenya Tourist Board*. Wakienda kwenye *exhibitions* huwa wanawalipia zile *pavilions* lakini wale ma-exhibitors wanalipa tiketi, hela ya hoteli na matumizi yao ya kawaida. Lakini ni jukumu la Serikali kuhakikisha inaandaa maandalizi mazuri kwa sababu ma-tour operators wanakwenda kutangaza nchi. Kwa hiyo, mkiwawezesha *TTB* na sisi tukawa na *uniform*, tukapendeza kama Kenya wanavyopendeza itakuwa ni vizuri na Kenya wanatuzidi kwa sababu wana ndege zao. Inatumiza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgeni anakuja mnazungumza, mnakubaliana anakwambia sasa nitakujaje Tanzania? Una-cross over, unakwenda ku-negotiate na *Kenya Airways*, inatumiza kwa kweli kwa sababu Wakenya wanapata wageni wengi zaidi kwasababu wanafanya *package* ya bei nafuu kwa sababu ndege ni zao. Kwa hiyo, kama kuja Tanzania ni Dola 2000, *Kenya Airways* inaweza ikanfanya Dola 1000 kwenda Kenya. Kwa hiyo, kwenye bei zao wanashusha zaidi. Kwa hiyo, tunaomba na sisi tuangalle ni jinsi gani tunaweza tukafufua Shirika letu la Ndege. Wakati wa Hotuba ya Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Waziri alitueleza kwamba *Air Tanzania* iko njiani inakuja, lakini mpaka leo ndege ile haijafika, sijui imefikia wapi na nasikia imekamatwa *South Africa* kwa sababu wanadaiwa. Sijui ni kweli!

Kwa hiyo, tunaomba mfanye juhudu tuwe na ndege yetu wenyewe *at least* hata kama haiendi huko Ulaya, lakini wakifika Dar es Salaam na Shirika la *KLM* na *British Airways* pawepo na *connection* basi kwenda hata Kigoma. Tunauza Kigoma, lakini mtu atafikaje Kigoma? Utalii siyo lazima kwenda kwenye wanyama. Watu wanataka kwenda *Lake Tanganyika*, watafikaje? Hakuna reli, hakuna ndege. Huwezi kumwambia apande mabasi atumie siku mbili afike Kigoma kwenda kuangalla *Lake Tanganyika*. Watu wana shughuli zao. Kwa hiyo, nafikiri tuangalle jinsi gani tunaweza kuhakikisha kwamba tunakuwa na Shirika letu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hizi ni *KINAPA*, Ngorongoro, *TANAPA* na kadhalika, kwenye hayo maonyesho ambayo tunakwenda nje, mfano ya *World Travel Market* na *International Trade Berlin* huwa wanapeleka Wajumbe wa Bodi kwenye yale Maonyesho. Mimi sioni kama kuna sababu ya kuwapeleka, wale walitakiwa wakae maofisini waangalie shughuli zile. Sasa mnawapeleka wale wazee kule wakafanye nini? Wanatakiwa wataalam ndijo waende kule waweze kujibu maswali yanayoulizwa na watu wanasmama zaidi ya masaa sita wanafanya kazi. Kama mnataka kuwapa *bonus* au *holiday*, naomba walipieni *holiday* waende *holiday* na sidhani kama wananchi watalalamika, lakini naomba suala zima la kupeleka Wenyeviti wa Bodi na Wajumbe kwenye hayo maonyesho mwache kabisa kwa sababu hayasaidii kitu. Wapelekeni *holiday* tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maonyesho ya Karibu *Fairs*, haya ni maonyesho ya kitalii yanayofanyika Arusha kila mwezi wa Tano, lakini Serikali haijaonesha nia ya kusaidia maonyesho hayo kama ilivyo yale maonyesho ya Saba Saba na Maonyesho haya ya Nane Nane, watu wamekuwa wakijisaidia wenyewe *ma-tour operators* wanalipa lakini sasa maonyesho haya yanapanuka yanakuwa ya kimataifa zaidi. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itusaidie kwenye hili kama wanavyosaidia Saba Saba na Nane Nane ili maonyesho haya yazidi kufana.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba niungane na Mheshimiwa Malecela kuhusu *concession fee*. Mimi ni *Tour Operator* na huwa tuna-book hotel well in advance kwenye hoteli zilizoko mbugani. Fee ya Dola 60 ni ndogo sana, kwanza hata ikifika 100 watalipa kwa sababu wanatu-charge fedha nydingi sana. Hakuna sababu ya kuwaonea huruma, *concession fee* ilipwe na walipe na sisi tunaisapoti hiyo kama kuna few *tour operators* ambaao wana-interest zao kule pengine wana-share juu yao lakini sisi tunasema *concession fee* ilipwe. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Owenya sijakusikia hapo ulimaliziaje kwenye *concession fee*!

MHE. LUCY P. OWENYA: Walipe. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Sawa endelea. (*Kicheko*)

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwasaidia wazawa, katika kuwawezesha hii biashara ya *tour operators*. Kuna vigezo vinawekwa wanasma ukitaka kuwa *tour operator* lazima uwe na magari matano mapya na kadhalika. Nafikiri hii Sheria ingelegezwa kidogo. Watueleze kwamba ukitaka kuwa *tour operator as long* unaweza kwenda na kuleta wageni maana magari si tutakodisha kwa sababu keki hii tunagawana. Kuna mwingine anawea kununua magari, ukaleta wageni na ukaenda ukakodisha magari. Kwa hiyo, naomba mlegeze hii sheria kidogo ili wazawa wengi waweze kuwekeza katika Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa na kwa kumalizia, niungane na mse maji aliye pita kwamba katika sekta hii ya uwindaji, naomba tuwe *more careful* kwa sababu unakuta mwindaji anakuja kuwinda samba, hapa tunamchaji Dola 2,500 lakini *South Africa* wanalipa Dola 17,000 kwa simba mmoja. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwenye hili aliangalie kwa uangalifu sana. Baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na nawakaribisha tena Kilimanjato. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

MHE. MBAROUK SALIM ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Maliasili. Kwanza kama kawaida niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalla leo hii, kuweza kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu nami niweze kuchangia bajeti hii. Nitaanza kwa kuipongeza bajeti ya Wizara hii, kwa kweli ni nzuri na watendaji wamefanya kazi ambayo inastahiki. Lakini pia nina taarifa kwamba Serikali kwa kupitia Wizara hii ya Maliasili imeanza kufanya *National Wood Biomass Survey* au *inventory*, nafikiri ni jambo zuri, ni kigezo kizuri na kigezo ambacho kinaweza kitatusaidia kama nchi kuweza kujuu athari ambazo zinapatikana au zinatokea au za ukataji wa miti kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoshauri katika mchakato huu ni kwamba uwe shirikishi. Tujitahidi tuweze kuwashirikisha wadau wote na pia pale ambapo ikifika kutoka ile ripoti ya mwisho, basi tuwashirikishe wadau, tuchukue mawazo yao ili tuweze kuandaa *monitoring system*

ambayo inaweza kutusaidia katika ufuatilaji na kuweza kujua athari ambazo zinatokana na ukataji wa miti kwa kila mwaka. Kwa hatua hiyo, naomba tena niipongeze Wizara hiyo kwa hatua ya kuweza kufanya *National Wild Biomass Survey*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu bado imo katika hali mbaya ya uharibifu wa ukataji wa miti ovyo na hii inatokana na umaskini wa watu. Watu ni maskini na fukara na hawana nishati nyingine mbadala ya kuendesha maisha yao. Kama tunavyoja, karibu asilimia 90 ya Watanzania tunategemea misitu kwa ajili ya maisha yetu. Kwa hiyo, kwa kweli Serikali kupitia Wizara hii tunahitaji kutafuta njia mbadala ya kuwawezesha wananchi ili waweze kupunguza kasi ya ukataji wa miti. Mpaka sasa hivi bado hakujawa na njia mbadala, tunagusagua tu mara majiko sanifu, mara gesi, lakini bado hatujaweka watu mahali ambapo wanaweza wakatumia njia mbadala wasitumie misitu.

Kwa hiyo, hilo ni tatizo na kama tutaliachia liendelee, basi katika kipindi kifupi kijacho tunaweza tukashuhudia kwamba tunapata majanga mengi ambayo yanatokana na uharibifu huu wa raslimali za misitu. Kwa hiyo, nashauri tu kwamba badala ya kupeleka utalii zaidi kwenye hifadhi zetu karibu na mbuga za wanyama, nafikiri pia tungepeleka utalii katika maeneo mengine ya kijamii ambao unaweza ukatumika utalii wa kimaumbile kwa sababu Tanzania ni nzuri na kila mahali ni pazuri na panavutia. Kwa hiyo, kama tutaweza kushawishi na kupeleka utalii katika maeneo yetu ya vijijini na watu wakaweza kupata mapato kutokana na njia hizo za kiutalii inawezekana ukataji wa miti ukapungua. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia biashara ya asali nafikiri ni muhimu sana kwamba watu, pia Wizara iwawezeshe ili waweze kufuga nyuki. Sasa hivi asali ni biashara nzuri sana na ina soko zuri, kwa hiyo, nafikiri wananchi wakiweza kufuga nyuki, basi ukataji wa miti unaweza ukapungua kwa kiasi kikubwa. Hali kadhalika kuna hii biashara ya hewa ukaa ni biashara nzuri ambayo kwa kiasi fulani inaweza ikawanufaisha jamii na wakaachana kabisa na ukataji wa miti ambayo ipo katika maeneo yao. Sasa nashauri Serikali iangalie njia hizo ambazo zinaweza zikasaidia kuboresha maisha ya watu na wakaachana na uharibifu wa mazingira na uharibifu wa ukataji wa miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kidogo ambalo nahisi kwamba *concentration* yetu kubwa ya uhifadhi uko zaidi katika maeneo ya hifadhi, misitu ya hifadhi, mbuga za wanyama na maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya hifadhi hiyo. Lakini tumeachia maeneo mingine mengi katika *public lands*, hakuna *concentration* kubwa ya uhifadhi katika maeneo hayo. Kwa sababu hiyo, tukisema uharibifu wa misitu, uharibifu wa maliasili, basi unakuwa katika maeneo hayo. Ukataji ni mkubwa, uharibifu ni mkubwa na watu wanaishi moja kwa moja kwa kutegemea raslimali za misitu zilizomo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitaja *Miombo Woodlands*, sasa hivi siyo ile Miombo ambayo tulikuwa tukitaja siku za nyuma. Lakini pia katika maeneo ya Shinyanga na Tabora ni maeneo ambayo huko nyuma yalikuwa ni *productive* sana lakini sasa hivi uzalishaji haupo tena. Sasa huo ni mwanzo, lakini tunasogea. Kwa hiyo kama hatukujipanga kuona kwamba uhifadhi pia unaendelea katika maeneo mengine, siyo katika mbuga na misitu ya hifadhi, basi inawezekana hali ikaja ikawa mbaya hapo baadaye. Mimi nashauri tujikite zaidi kwenye hayo maeneo ili tuepukane na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye kipengele kingine ambacho nilitaka nizungumzie ni kuhusu utawala bora katika *resources management*, hasa hizi rasilimali za maliasili, uvuvi, watachanganya hapo misitu na nyinginezo. *Key elements za good governance ni participation na empowerment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matatizo kwamba tunawashirikisha wananchi *at the initial stages* hasa katika uhifadhi na tunawaelimisha wanahifadhi, lakini hatufanyi ile *empowerment* hasa ya kuwawezesha wakaweza *ku-benefit* kutokana na ile misitu ambayo imo katika maeneo yao. Lakini lingine, pia ni kigeugeu cha Serikali, kwa sababu kama watu tayari tumewakatia maeneo, tumeshawaambia kwamba watahifadhi katika maeneo yao rasilimali zilizomo katika maeneo yao, lakini baadaye anatokea mwekezaji anauziwa, anakodishwa. Sasa hivyo ni kuifanya

ile jamii iwe haijui pa kuelekea. Ni utata ambao kwa kweli unawakosesha watu raha na nafikiri matatizo hayo ya wawekezaji yameshaelezwa katika maeneo mengi ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri atakapokuja, nataka njue tu kwa kifupi kwamba kuna hii misitu ambayo tunahifadhi pamoja na jamii (*joint forest management*). Jamii tumeiweka mahali gani au jamii ina-benefit kitu gani katika *joint forest management*? Nakusudia zaidi kwenye *monetary incentive*, yaani kama tunakusanya mapato kutokana na utalii katika misitu hii ya hifadhi, je, jamii inafaidika kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kwenye hii misitu ya *community (community based forest management)*. Hii misitu najua kwamba kuna mradi huu wa hewa ya ukaa ambao nafikiri upo katika mchakato. Nina wasiwasni kwamba kutokana na *ownership* ya misitu hiyo au ya maeneo hayo ya ardhi kwamba jamii haimilishwi, inawezekana baadaye hiyo biashara jamii ikaipoteza na bila shaka mwekezaji ambaye atakuja kufanya biashara na jamii atataka ajue *status* ya huo misitu kama sharti. Sasa nilitaka njue kwamba je, Serikali ina mpango gani wa kuwamilishwa jamii au *group* la jamii ambayo imehifadhi misitu hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru! (*Makofii*)

MHE. VITA M. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vema hotuba yake leo hapa. Pia nawapongeza Katibu Mkuu, Mama Tarishi na maaftisa wote walipo chini yake kwa kuiandaa vizuri hotuba yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Namtumbo ni Wilaya yenye Km^2 20,375. Lakini eneo lisilopungua Km^2 19,000 lote ni eneo la uhifadhi wa misitu na *Selous* ya Kusini na vijiji vyetu vyote vimezungukwa pembeni vinalima pembezoni mwa hifadhi. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Sheria za Uhifadhi zilizopo ambazo zinalinda sifa pekee za maeneo hayo (*outstanding universal value*), nadiriki kusema katika utekelezaji wake zinatusahau wananchi tunaozunguka maeneo hayo. Sisi ndiyo wenye asili ya mapori yale na sisi kama binadamu vile vile kwa kuelewa uhifadhi ule na tunaulinda uhifadhi ule, tuna haja na sisi ya kulindwa vilevile katika maslahi yetu ya msingi. Binadamu au wananchi wa Wilaya ya Namtumbo wanaoishi katika maeneo yale, *outstanding value* yao ni chakula na maisha yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakulima wa Namtumbo ambao vijiji vyao vinapakana na hifadhi hizi wanapolima chakula chao na wanyama wanapokuja kula chakukla chote na tunapoiomba Serikali iweze *ku-respond* au kutoa fidia, Serikali inakuwa na kigugumizi. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali ielewé pia thamani ya maisha ya sisi binadamu ni chakula na mapato yetu tunapata kutokana na kilimo. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali, wanyama hawa pia wakati mwengine wanadhuru mpaka kuua. Kwa hiyo, tunapoleta malalamiko yetu ya kufidiwa, tunaiomba sana Serikali ishirikiane na sisi kwa kuwahi kulipa fidia hiso. Lakini pia inapotokea madhara wanyama wanapokuja, basi kuwe na *quick response* ya kwenda kuwarudisha wanyama wale au kuwaua wale wanyama wakali. Tunaiomba sana katika eneo letu la Namtumbo tunapata shida sana ya kuingiliwa na wanyama hasa kwa kuongezeka. Tunafahamu kabisa umuhimu wa uhifadhi, kwa sababu *outstanding universal value* ya uhifadhi ni *growth* ya wale *wildlife animals*. Lakini pia na sisi mfahamu umuhimu wa thamani ya binadamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba nipongeze na kuiunga mkono Serikali na Bunge Iako Tukufu, Bunge la Tisa Iilipopitisha mwaka 2009 Sheria ya kuruhusu uchimbaji wa Madini ya Urani, Gesi na Mafuta katika uhifadhi. Sisi Namtumbo kule ni maskini kabisa, ni watu ambao toka dunia hii ianze hatujawahi kuona umeme, wala hatujawahi kuona kiwanda chochote kile. Lakini leo hii baada ya Bunge Iako Tukufu la Tisa kupitisha Sheria ile, walikuja wawekezaji wamefanya utafiti na kugundua *deposit* ya *world class* ya *uranium* ambayo sasa leo Namtumbo inajulikana katika ramani ya dunia kwamba ni *potential* kiuchumi, si kwa Tanzania tu, lakini pia na kwa dunia kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo, naipongeza Serikali kwa hatua ilizokubali kuzichukua kuomba mshirika mdau (*UNESCO*) kuona jinsi gani tutakavyoweza kushirikiana kutekeleza mradi ule kwa mujibu wa taratibu zote za sheria. Ninachowea kuishauri Serikali kwa kuiunga mkono Kamati kwamba Serikali ishirikishe Kamati zote mbili za Nishati na Madini na Maliasili katika hatua zake zote za sheria kuhakikisha tunafanikiwa, tunakamilisha taratibu hizo na tunaanza mradi huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo kwa *economics* za haraka haraka, unasema kwamba utakuwa unaweza kutuingizia dola milioni 250 kwa mwaka, na kwa Halmashauri ya Namtumbo kwa mujibu wa sheria, uzuri wa mradi huu kama utaanza utsangukia kwenye sheria mpya ambayo tulipitisha ya madini hapa Bungeni kwamba Halmashauri zetu zitakuwa zinapata kwa mujibu wa sheria ile *District Cess* ya 0.3 percent ambayo kwa haraka haraka, tunaamini kabisa Halmashauri yetu inaweza ikawa inapata dola 750,000. Sasa tunaomba kama zitashirikishwa hizi Kamati zote mbili, basi zisimamie sheria hiyo ili tuweze kupata manufaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini juu ya hilo, ajira, tuna uhakika wa ajira kwa *unskilled labours 4500*, lakini pia *skilled labours 1600*. Kwa hiyo nayo itatusadia sana katika nchi yetu. Lakini pia kodi katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naunga mkono Serikali. Naomba taratibu ziende haraka ili tuweze kukamilisha utaratibu huo na mradi ule uweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mengi, ni hayo tu! (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa. Nakushukuru sana kwa mchango wako. Inaelekea Halmashauri yako itakuwa tajiri kweli kweli! Nilikuwa naangalia hapa *Selous* itapata ngapi, bado sjapata majibu!

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Nibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kuweza kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara Mama Maimuna Tarishi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara kwa jinsi wanavyofanya kazi yao kwa umahiri mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi nijikite kwenye suala la maliasili, lakini hasa nikianza na migogoro. Lakini tu niruhusu kabla ya kuingia kwenye migogoro, nichukue fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge wa Masasi, Mheshimiwa Mama Mariam Kasembe na Mheshimiwa Dunstan Mkapa kwa kumshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige kwa kufanya ziara yenye ufanisi katika Majimbo yetu katika tarehe 6, 7 na 8 mwezi huu. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri ameonyesha mfano dhahiri unaothibitisha jinsi ambavyo Waheshimiwa Mawaziri wanapaswa kuteremka hasa kwenye ngazi ya vijiji. Mheshimiwa Maige amejifunza jinsi gani wananchi wanavyokuwa na hamu ya kuona Mawaziri kwenye maeneo ya vijiji vyao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro mingi inayotawala hasa katika maeneo ambayo kuna mbuga zetu ama kuna hifadhi, kwa muono wangu, yametokana na jinsi ambavyo bado Wizara hajjaweka utaratibu mzuri wa kushirikisha viongozi kule ambako mbuga ama hifadhi hizo zipo. Kwa hivi sasa kuna migogoro mingi.

Kwa rafiki yangu kule Mbarali kwa Mheshimiwa Kilifi, kule kwa Mheshimiwa Telele, kule Ngorongoro, kule *Selous* kule kwa Mheshimiwa Martha na kule Masasi. Lakini migogoro hii ingeweza kuepukwa kama watendaji wa Wizara ya Maliasili kabla hawajaanza kutekeleza jambo wanadolikusudia, kukaa na viongozi wale, kushirikiana na hatimaye kufikia muafaka wa jambo wanafikiri ni sahihi kulifanya katika maeneo hayo.

Kwa mfano, kwenye maeneo mengi tuna tatizo la mipaka na mipaka hii imetokana na jinsi ambavyo idadi ya watu katika maeneo yale yameongezeka, lakini pia shughuli mbalimbali za kiuchumi katika maeneo hayo pia kuongezeka. Na mimi naamini kabisa wananchi wengi wa

Tanzania hasa katika maeneo yetu ambako mbuga ama hifadhi zipo, wanafahamu kabisa juu ya umuhimu wa hifadhi zetu. Lakini kinachopaswa pale ni ushirikishwaji, washirikishwe na hatimaye waweze kujua kile kinachotakiwa kufanywa pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo ni vizuri sana Wizara hii ikaliangalia wakati inapofanya mabadiliko yoyote katika maeneo hayo, ni kuepuka kutoa ahadi ambazo hazitekelezeki. Katika maeneo haya, wananchi wamekuwa na shughuli zao mbalimbali. Wanaweza wakaenda viongozi pale wakaahidi kwamba Wizara yetu itajitahidi kushirikiana na wananchi aidha katika ujenzi wa madarasa ama katika ujenzi wa zahanati ama katika shughuli zozote za maendeleo. Pale ambapo wanaona ahadi zile hazitekelezwi, ndiyo chanzo cha wananchi katika maeneo hayo kuanza kuona kumbe ile hifadhi au mbuga wao kwao ni adhabu na kutotoa ushirikiano mzuri pale ambapo panahitajika kutoa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika Sheria iliyopitishwa mwaka 2010 na Mheshimiwa Waziri kutoa Kanuni zake juu ya wanyama wakali, imewapa faraja kubwa wananchi juu ya maamuzi na jinsi Sheria hiyo inavyotamka. Kama nilivyoeleza mwanzo kwamba Mheshimiwa Waziri kwa mfano katika ziara yake hii aliyofanya, aliiweza kupata fursa ya kufanua juu ya Kanuni na Sheria hii jinsi ambavyo Serikali ilivyodhamiria walau kuanza kupunguza baadhi ya kero ama kushiriki katika maafa mbalimbali ambayo yanawatokea wananchi katika maeneo yao. Sheria hii imewataja baadhi ya wanyama wakali saba ambao wao wakileta madhara, Serikali itatoa walau kifuta jasho ama kifuta machozi. Wanyama hao ni simba, boko, faru, fisi, nyati, mamba na tembo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naishauri Serikali bado kuna wanyama wengine wakali ambao hawakuorodheshwa. Ningeshauri, kwa mfano, chui ni mnyama mkali, lakini hayupo kwenye orodha hii. Nyoka kwa mfano, chatu ni hatari kwa binadamu lakini pia kwa wanyama. Lakini pia kwenye maeneo yale ambayo kuna hifadhi, kuna nyani ambao kama aliyosema Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba wapo wanyama waharibifu wanaoharibu kabisa mazao yale. Mimi nashauri nao wangeingizwa ili uharibifu mkubwa unapofanyika, basi na fidia iweze kutolewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Wizara kwa kuwa utekelezaji wa Sheria hii ndiyo unaanza, ni vizuri kujipanga vizuri Wizarani ili kusiwe na ucheleweshwaji wa malipo pale taarifa zinapofika Wizarani. Vinginevyo itageuka kuwa ni kero na sisi Waheshimiwa Wabunge tutakuwa tunakuja hapa na orodha ndefu ya wananchi wetu ambao wamepeleka malalamiko yao, lakini hayajatekelezwa. Kwa hiyo, naiomba Wizara na kwa kuwa mimi naamini kabisa Mama Maimuna Tarishi, Katibu Mkuu wa Wizara hii ni mahiri kweli, tulikuwa naye TAMISEMI, tumeishi naye kule TAMISEMI, amefanya kazi nzuri sana, pamoja na kwamba pale tayari Mheshimiwa Rais amempeleka *Comrade* Katanga TAMISEMI, naye ni mchapakazi, lakini tunaamini kwamba Mama Tarishi atamsaidia sana Waziri na ataisaidia sana Wizara ile katika kuhakikisha kwamba inaondoa migogoro ambayo ipo katika maeneo mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie kuhusu hifadhi za misitu, bado tunalo tatizo kubwa katika nchi yetu hasa katika hifadhi za misitu. Bahati nzuri tulisafiri na Mheshimiwa Waziri, alijionea mwenyewe jinsi maeneo mengi yakiwa yamechomwa moto, ikiwa ni pamoja na hifadhi za misitu. Nilikuwa nafikiri ipo haja sasa kama Sheria ipo, basi hebu itafutiwe utaratibu wa kurekebishwa vizuri ili wale wanaobainika kuchoma misitu yetu wachukuliwe hatua kazi zaidi. Kwa sababu sasa hivi misitu inachomwa, lakini wala hakuna jitihada zozote zinazofanywa za kuwatafuta wanaochoma misitu na kuchukuliwa hatua.

Mimi naamini Wizara ya Maliasili na Utalii ikishirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kwa Alhaj Kagasheki pale, naamini kabisa kwamba kazi hii ya kuwasaka wale inaweza ikafanyika vizuri na wakapatikana na wakishaanza kupewa adhabu, wananchi wataelewa kwamba kumbe hili jambo ni jambo ambalo halistahili kufanywa. Ninaendelea kusisitiza kwamba mawasiliano kati ya Wizara na wananchi husika katika maeneo ambako kuna hifadhi ni jambo la muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Mkurugenzi wa Wanyamapor kwa jinsi walivyolichukulia umuhimu mkubwa sana suala la tatizo la mamba katika Mto Ruvuma. Kwa takriban sasa miaka 7/8 wananchi wote wanaopitiwa na Mto ule kuanzia kule kwenye Jimbo la Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwenye Jimbo la Tandahimba, Jimbo la Newala, Jimbo la Lulindi, Jimbo la Tunduru pamoja na Nanyumbu, wananchi zaidi ya 35 wamepoteza maisha katika kipindi cha miaka minne/mitsno tu. Na katika kipindi cha 2010/2011, watu tids katika Jimbo la Lulindi wamedhurika na wameuwawa na mamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Wizara kwa jinsi ambavyo ilipeleka ndege ya kufanya utafiti wa kujuu idadi ya mamba na tayari idadi ya mamba imeshapatikana na Wizara imeahidi kuhakikisha kwamba mamba wale wanavunwa, lakini kilichowafurahisha wananchi ni pale Waziri alipobaini kwamba tatizo la wananchi wengi kuuwawa na mamba katika Mto Ruvuma ni kukosekana kwa visima kando kando ya Mto ule yanayopelekea wananchi wote kwenda Mto Ruvuma kwa mahitaji ya maji ya kunywa, maji ya kuoga na maji ya kufulia.

Kwa hiyo, namshukuru sana Waziri kwa niaba ya wananchi na Mnavira, kwa jinsi ulivyoonesha kuchangia katika suala zima la upatikanaji wa visima, lakini pia pale ulipoahidi kuchangia juu ya ujenzi wa vituo vya afya vya Mnavira na Chipolopola ambavyo vitasaidia wale waathirika wanaoumia ili waweze kupata matibabu ya haraka kabla hawajapelekwa kwenye hospitali ya Wilaya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie kumpongeza Waziri, naendelea kumtia nguvu na kumuimarisha zaidi atekelze majukumu yake kama Mama yangu Mama Malecela alivyositisiza kwamba awe imara, asimame hapo hapo, atekelze kazi ya Wizara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani atafuata, baada yake ni Mheshimiwa Faith Mitambo na Mheshimiwa Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro ajiandae. (*Makof*)

Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani karibu.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie katika Wizara hii. Kwanza nianze ku-declare interest kwamba mimi nilikuwa mfanyakazi wa Shirika la Hifadhi ya Taifa kama Daktari Mkuu wa Wanyamapor kwa miaka kumi na nne, lakini vilevile ni Mjumbe wa Bodi ya TWPF. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijasahau niwapongeze kwa kazi inayofanyika kwa hotuba ya Waziri lakini kwa kazi ambayo inafanyika hususan ya Idara ya Nyuki na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapor kitengo cha utafiti wa nyuki kwa sababu ya kazi nzuri wanayoifanya Jimboni kwangu, nawaomba waendelee ili tufanye zao la nyuki kuwa muhimu sana katika Jimbo langu kuondoa umaskini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Maliasili na Utalii ni Wizara muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu, Wizara hii ingeweza sana kuondoa umaskini wa Watanzania kwa jinsi inavyojishirikisha na sekta nyingi kutokana na shughuli zake. Kwa bahati nzuri sana Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi sana ambazo zipo katika Wizara hii, ukiangalia tu maliasili ya wanyamapor iliyopo katika nchi hii Tanzania ina pori la akiba la Selous ambalo ndiyo pori kubwa kabisa Barani Afrika. Ina Hifadhi ya Serengeti ambayo ina upekee kwa sababu ya mamilioni ya wanyama wanaohama kwa takribani kilomita 1,000 kila mwaka kufuata malisho na kufuata mazalia. Hiki kitu hakipo popote kwingine duniani, kiko Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Tanzania ina mambo mengi ya kumbukumbu ya mambo ya kale, tuna Mji Mkongwe wa Zanzibar, tuna mambo ya kumbukumbu ya biashara ya utumwa Bagamoyo, tunayo Ujiji, tuna mafuvu ya *dinasaur* kule Tendaguru ambako iligunduliwa na maeneo mengine kama *Olduvai Gorge*. Maeneo haya kwa kweli ni hazina ya pekee kwa

Tanzania lakini bahati mbaya sana Tanzania haijaweza kunufaika vya kutosha na hazina hii kubwa tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri tatizo kubwa tulilonalo ni kukosa dhamira ya makusudi ya Kitaifa ya kutumia rasilimali hii ili ivate katuondolea umaskini, na ninaona kama Taifa tunakosa dira kwa sababu ya Bajeti ndogo inayotengwa kwa Wizara hii ambayo hailengi kusaidia kunyaanya sekta hii muhimu ili tuweze kujikomboa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nchi ndogo kama Mauritius ambayo haina sifa ya ajabu sana kama visiwa vya Zanzibar vyenye historia ya ajabu, lakini Mauritius wanakusanya dola bilioni moja na nusu kila mwaka kutokana na utalii, sisi hapa nchi nzima na ukubwa wote huu tunakusanya dola milioni 1.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mwambao mkubwa sana wa Pwani, karibu kilomita mia nane kutoka Tanga mpaka Mtwara, lakini Tunisia ambayo ina mwambao mdogo tu na siyo mzuri kama ule ufukwe wa Mtwara, Zanzibar na kwingine lakini inakusanya dola bilioni tatu kila mwaka kutokana na utalii. Kenya nchi ndogo kuliko Tanzania, haina rasilimali nyngi lakini watalii wanaoingia Kenya kila mwaka ni karibu milioni 1.4 sisi tunazungumzia watalii laki saba. Mimi nafikiri tunahitaji kuweka nguvu na msukumo wa makusudi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lingine ninaloona ambalo tuna udhaifu ni namna tunavyopanga mikakati yetu ya *promotion and marketing*. Timu ya Tanzania inapoenda kwenye maonesho ya Kimataifa ni kila mtu anajiondokea kwake, hakuna mkakati wa pamoja kusema sasa tunataka kwenda kufanya nini. Hakuna malengo ya kusema sasa mwaka huu tunataka tuondoke kwenye idadi hii tufikie hii. Tuondoke kwenye mapato haya tufikie haya, hata watu wakitoka kwenye maonesho kila mmoja anasambaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana Mheshimiwa Lucy Owenya alikuwa anasema hata *uniform* hawana, Kenya wanaenda kama timu. Rwanda iliyokuwa kwenye *crisis* juzi juzi tu, lakini sasa hivi imeanza kupata tuzo kwa jinsi inavyotangaza utalii, sasa Tanzania na rasilimali zote hizi! Rwanda wana Sokwe tu pekee. Kwa hiyo, nafikiri ni muhimu sana tukajielekeza kwa makusudi katika kuimarisha utangazaji wa utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi yetu ya Utalii (*TTB*) ambayo sasa ndio tunaipa jukumu kubwa la kutangaza haina uwezo, kwanza Bajeti ndogo, haina watendaji, sasa tunaipa jukumu. Nimesikitika kidogo niliposikia Waziri anatoa maelekezo kwamba Mamlaka ya Ngorongoro, Hifadhi za Taifa wasishiriki kwenye maonesho, sasa hawa watu ndio wanaozifahamu hizi rasilimali, lakini vilevile wana rasilimali watu, sasa ukiwaachia *TTB* ifanye hiyo kazi hata hawazijui wanaziandika tu kwenye vipeperushi ukiwaambia kwa nini Serengeti ni *unique* hawawezi wakaeleza, kwa hiyo, ni muhimu sana kuangalia sana uamuzi alioutoa lazima autathimini upya, vinginevyo tutabaki kulaamu tu Kenya wanatumia Serengeti, Kenya wanatumia Mlima Kilimanjaro. Ni lazima tuweke mikakati yetu ya maksudi na kutumia utalaam. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine kwa utalii wa Tanzania ulivyo, inaonekana kama upo Kaskazini mwa Tanzania tu kama ndio kwenye vivutio pekee. Tuna mwambao mkubwa wa Kusini mwa Tanzania, tuna mwambao mkubwa wa Magharibi mwa Tanzania, tuna mwambao wa Ziwa Victoria una vivutio vya ajabu na vya pekee. Kule Magharibi kwenye Milima ya Mahale ndio kundi kubwa pekee liliobaki duniani la sokwe, wanyama jamii ya binadamu, lakini watu wanaofika Mahale ni wa kuhesabu. Hata Watanzania wenyewe wamefanya wakaamini kwamba Serengeti ipo Arusha wakati Arusha haina hata kipande kidogo ndani ya Hifadhi ya Serengeti, Serengeti ipo Mara, ina kipande cha Mkoo wa Shinyanga, ina kipande kidogo cha Mkoo wa Mwanza. Kuingia Serengeti ni kilomita 140 tu unafika Serengeti kutokea Mwanza lakini kutoka Arusha ni kilomita 332. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini huu mfumo umefanya watu wa Kaskazini tu ndio wanunufaika na utalii, ni nani alete kurekebisha hii hali ili hata watu wa Busega na wenyewe wanufaika na utalii huu? Ni *TTB* na Wizara hii ni lazima ijielekeze kuhakikisha kwamba gawio la utalii linasambaa katika nchi yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo na mimi kuhusu suala la *concession fee*. Suala hili linasikitisha na linakera kwamba mpaka leo hii karne ya 21 wawekezaji wa mahoteli wanazilipa Hifadhi za Taifa na Ngorongoro dola nane kwa mtalii. Haipo popote duniani, haikubaliki kwa namna yoyote ile. Hoteli ambayo wanalaza mtalii kwa dola mia tatu mpaka elfu moja na mia tano, wao wanakulipa dola nane. Gharama za kuwahifadhi na kuwalinda usalama, gharama za kutengeneza barabara, sasa hivi hata wanaweka dawa za kuzuia hata watalii wasiumwe na mbung'o hizo zote ni gharama Wizara hii inawekeza halafu wao wanataka walipe dola nane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilienda kule Kenya wakati ilipokuwa imeshambuliwa sana na maingilio ya Wasomali, ilfikia hatua mahoeli yaliyokuwa yamewekezwa kule *Meru National Park* yakaachwa yakaiza yakawa magofu, hapa wana-enjoy amani halafu wao wanataka walipe dola nane tu siyo sahihi kabisa. Kwa hiyo, Waziri kaza buti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha inaonekana kuna *syndicate* ya kampuni sjui ngapi tatu za watu wa aina moja wanaofanana kwenye nchi yao huwezi ukafanya hivyo, hapa Tanzania wanataka wale dezo. Hizi kampuni ni za Kimataifa uliza kule Kenya wanalipa shilingi ngapi, Tanzania hapa wamefanya shamba la bibi hatuwezi kukubali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusiana na masuala ya Jimboni kwangu, matatizo ya wanyama waharibifu. Wanyama waharibifu wamewtia umaskini mkubwa sana watu wa Jimbo la Busega, kuna wanyama wanaoitwa ndovu kule kwetu wanaitwa tembo wamekuwa kero kubwa katika vijiji vya Lamadi, Lukungu, Mwamalole, Mwabayanda na Mwakiloba imekuwa tatizo kubwa sana, inapofika kipindi cha masika watu hawalali nyumbani kwa sababu ya hawa wanyama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo kubwa ni kuwapata askari wa kuzuia na kufukuza hawa wanyama inakuwa ni taabu hawapatikani. Vilevile kuna wanyama aina ya nyati kwenye Hifadhi ya Msitu wa Sayaka, lile siyo eneo la wanyamapor. Ningeshauri Waziri muangalie utaratibu wa kuwaondoa wale nyati ili watu kule wafanye kazi zao za maendeleo kwa amani. Naamini kuna utalaam wa kutosha katika Wizara na kama wanapungukiwa utalaam mimi niko tayari kuwasaidia ili tuhamishe hao wanyama ili watu waweze kufanya kazi zao kwa uhakika, na mwaka huu ni mwaka wa njaa, wanyama hawa wanawatia umaskini mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo la mipaka kati ya pori la akiba la Kijereshi na vijiji nilivyovitaja, mipaka ile sasa nafahamu imeshakuwa ndani ya sheria, haiwezi ikabadilishwa kirahisi, lakini ilifanywa kihuni huni kwa sababu haikushirikisha wananchi vya kutosha. Mipaka ile imekata maeneo ya vyanzo vya maji vyote vimebakia ndani ya hifadhi, wananchi huku na mifugo hawana mahali pa kupata maji.

Meshimiwa Naibu Spika, Maafisa Wanyamapor walikuja tukafanya mikutano nao kule namna ya kupunguza migogoro hii na nimeandika barua kuomba watutengenezee mabwawa ili wananchi hawa wapate vyanzo vingine vya maji ili tuondokane na mgogoro wa kukaa tunashambuliana, tunaingiliana wananchi na maeneo ya hifadhi. Wajenge mabwawa Mwakiloba, wajenge bwawa Mwabayanda, wajenge bwawa Chabutwa ili kuhakikisha kwamba watu na mifugo yao wana sehemu nydingine ya kupata maji ili tuondokane na kero hii ambayo ilisababishwa na utendaji wa Wizara na utendaji ambao kwa kweli haukizingatia haki ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka vilevile nizungumzie kuhusu wafanyakazi waliopo ndani ya Hifadhi ya Taifa. Hifadhi za Taifa ni rasilimali ya Watanzania wote na wafanyakazi waliopo kule wamepewa dhamana tu ya kusimamia kwa niaba ya Watanzania wote, lakini askari wale wanafanyakazi kwenye mazingira magumu na kazi yao ina *risk* kweli kweli. Kule Magharibi wakimbizi wanakuja na silaha za kivita, kule Kaskazini kuna ndugu zetu wana mishale yenyе sumu kali, sasa kuwadhibiti wale watu kwa nguvu ya kiasi siyo mchezo. Askari wamepoteza maisha na sheria sioni kama inawalinda vya kutosha. Jangili akiuawa Tume ya Haki za Binadamu wanakimbia haraka sana kwenda kuangalia na huyu alikuwa ndani ya pori anafanya uhalifu, mtu mwenye SMG unamdhhibit namna gani kwa nguvu ya kiasi, unamdhhibit namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria lazima zirekebishwe, askari hawa walindwe na wanapodhurika wawe na *insurance* ya kutosha ili familia zao waweze kukaa kwa amani. Mwaka jana kuna askari amekatwakatwa mapanga kule Burigi kama nyama na mwingine amekatwa kule Kitulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Dkt. Titus Kamani Mlengeya, enzi zetu tulikuwa pamoja kule Serengeti. Mheshimiwa Faith Mitambo atafuatiwa na Mheshimiwa Kaika Telele.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kusema yale ambayo nimetumwa na wananchi wa Liwale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Liwale ni mionganoni mwa Wilaya ambazo zimepakana na Pori la Hifadhi ya Selous na inakadirisha kwamba theluthi mbili ya eneo la Wilaya ya Liwale sawa na kilomita 25,586 lipo ndani ya Hifadhi ya Pori hili la Selous. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kuona kwamba Wilaya hii ni wadau wakubwa na tulikuwa tunategemea kabisa kwamba tunaweza kufaidika kwa kiasi kikubwa na mbuga hii ya Selous. Tofauti inayojitokeza ni kwamba sisi ndiyo tumekuwa waathirika wakubwa kwa mambo mengi, wanyamapori wakali na waharibifu, kuna migogoro ya mipaka kule, ile asilimia 25 ambayo Halmashauri tunatakiwa kulipwa vyote hivi sisi tumekuwa waathirika wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakazi wa Wilaya hii wamekuwa wakivamiwa mara kwa mara na wanyama waharibifu na wanyama wakali na hivyo kuharibu mazao yao na kuwaacha wananchi hao wakiwa hawana chakula, hawana kitu na kuwaachia maumivu makubwa na hasara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea hali hii nilikuwa ninategemea kwamba Wizara ya Maliasili ingeweza kufanya haraka kuwapatia fidia wananchi hawa amba wameharibiwa mazao yao na kuwaacha hawana kitu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia au kifuta machozi kwa ajili ya waathirika wa wanyamapori wakali, kwa masikitiko kabisa ninaomba kusema kwamba fidia ya shilingi laki moja kwa ekari ya mazao ni ndogo sana na mbaya zaidi ni kwamba muathirika anatakiwa alipwe hekari tano tu na unaweza ukakuta kwamba wanyama wakali wameingia kwenye mashamba ya wakulima, wameharibu hekari kumi, lakini kwa sheria iliopo sasa ni kwamba mkulima huyu anatakiwa alipwe mwisho kufikia hekari tano tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara ya Maliasili iangalie upya sheria hii na utaratibu huu, kama mtu ameharibiwa mazao yake yote hekari zote kumi ni vema alipwe hekari zote kumi badala ya kumlipa hekari tano, hii siyo sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Niabu Spika, ninaomba kuleta salamu hizi zinazohusiana na kiwango na fidia hizi za kifuta jasho kiangaliwe upya kwa waathiriwa wa mashamba yao na kwa watu waliojeruhiwa au kuuawa na wanyamapori wakali. (*Makofii*)

Mheshimiw Naibu Spika, viwango vilivyopo kwa sasa havitoshelezi na vinaonyesha utu zaidi kwa wanyamapori kuliko binadamu. Pamoja na utaratibu huu uliowekwa na Wizara ya Maliasili na Utalii waathirika bado hawapati fidia zao kwa wakati muafaka, wanatumia muda mrefu sana kufuatilia mafao haya na hatimaye wanakata tama, mafao hawapati, mashamba yao yameliwa na wanyama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, rambirambi kwa mfiwa hutolewa wakati wa msiba. Mimi nilitarajia waathirika hawa walitakiwa walipwe kifuta machozi chao muda si mrefu baada ya tathimini ya uharibifu wa mashamba yao kufanyika na nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Maliasili hiki si kilio cha Liwale tu, kilio hiki ni cha sehemu nyingi. Tunaomba sana mtupatia fidia kwa wakati

na tunaomba Mheshimiwa Waziri anijibu wale waathirika wote wa Wilaya ya Liwale mnawapelekea fedha zao za kifuta machozi lini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niongelee mgogoro wa mipaka uliopo ndani ya Wilaya hii na Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous. Vijiji vinavyopakana na Hifadhi hii ya Selous ni Kikulyungu, Barikiwa, Chimbuko, Mlembwe, Ndapata, Naujombo, Milui, Mpigamiti, Kimambi na vitongoji kadhaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kati ya vijiji hivi na Hifadhi ya Wanyama ya Selous uliwekwa mwaka 1974 kwa Tangazo la Serikali la mwaka huo na pamoja na ramani yake inaonyesha mipaka hiyo. Kijiji cha Kikulyungu kimekuwa na mgogoro wa mpaka kwa muda mrefu huku Wizara ya Maliasili na Utalii ikiusikia mgogoro huu wa mpaka kati ya Kijiji cha Kikulyungu na *Selous Game Reserve* na kutochukua hatua yoyote kumaliza mgogoro huo. Mpaka uliowekwa kwa tangazo na ramani na Serikali mwaka 1974 eneo la Kihurumila linaonyesha kwamba liko ndani ya eneo la kijiji cha Kikulyungu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mwaka 2007 wakati wa maandalizi ya mradi wa mpango wa matumizi bora ya ardhi, bado eneo hili la Kihurumila pamoja na bwawa liliopo ndani ya eneo hilo la Kihurumila limeonyesha kwamba eneo hilo linalogombewa limo ndani ya eneo la kijiji cha Kikulyungu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Novemba, 2009 uongozi wa *Selous Game Reserve* chini ya Wizara yako Mheshimiwa Waziri umepokonya eneo hilo la Kihurumila na kudai kwamba eneo hilo ni mali ya *Selous Games Reserve*. Namuomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake atuambie sisi wananchi wa Liwale na hasa Kijiji cha Kikulyungu ni tangazo namba ngapi la mwaka upi la Serikali ilibadilisha mpaka ule na kulipeleka eneo la Kihurumila na bwawa lake upande wa *Selous* na mchakato kama ulikuwepo kwa nini ulifanyika chini chini bila kuwahuishisha wadau wa upande wa pili amba ni Kijiji cha Kikulyungu na kwa nini Wizara ya Maliasili imefumbia macho tatizo hili la ugomvi wa mpaka wakati ukweli mpaka unaonekana uko wapi. Wananchi hawa wamenituma, wamehanganya sana kwa muda mrefu na mgogoro huu wa mpaka na hawaridhiki jinsi Wizara ya Maliasili na Utalii ilivyowafanya la kuwapokonya eneo lao na kwa niaba yao ninaomba Wizara ya Maliasili na *Selous Games Reserves* mturudishie eneo letu la Kihurumila na bwawa lake mara moja ili mgogoro huu uishe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka huu umekuwa *diverted* pale ulipokuwa kwa sababu zipi, wanakijji wa kijiji cha Kikulyungu wamenyang'anywa eneo lao ambalo mimi kisheria bado nakubaliana na wao kwamba eneo hilo ni eneo la Kijiji cha Kikulyungu na siyo eneo la *Selous Games Reserve*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi eneo walilonyang'anywa wao limepimwa vitalu, eneo ambalo ni *open area* na wananchi wa Kikulyungu walikuwa wanatumia eneo hilo kwa shughuli zao za kujitafutia riziki kwa kuvua samaki ndani ya bwawa hili la Kihurumila. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninahitaji majibu ya ufumbuzi wa mgogoro huu na mimi *personally* ningombwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe pamoja na mimi twende kukagua mpaka huu pamoja na wanakijji wa Kikulyungu ili uone ukweli wa tatizo hili. Katika hili hatutahitaji utume watu waliopo chini yako, tutahitaji wewe mwenyewe *personally* ukatuambie kule *site* tatizo liko wapi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niongelee kuhusu fedha za mgao wa asilimia 25 ya mapato ya uwindaji wa kitalii kwa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale. Kulingana na Sheria na Kanuni za Wanyamapori Wilaya ya Liwale inastahili kupata mgao wa asilimia 25 ya mapato yanayotokana na uwindaji wa kitalii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale haipelekewi mgao huo wa asilimia 25 ya kiwindaji wa kitalii kama inavyostahili na kwa wakati. Asilimia 25 ya mgao wa mwaka 2006/2007 haukuletwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, mgao wa asilimia 25 mwaka

2008/2009 haukuletwa aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ilitegemea kupata shilingi milioni 106 mwaka 2010/2011 kama asilimia 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri hiyo imepelekewa shilingi 40,155,796.37 tu. Kwa hali hii tunaona kwamba kwanza mgao huo haufiki kwa wakati muafaka pili mgao huo ni kidogo haulingani hata kidogo na makusanyo na shughuli za kitalii zinazoendelea ndani ya vitalu viliyoko upande wa Wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Liwale ni wadau wakubwa wa hifadhi hii tunaomba sana Wizara ya Maliasili iwahusise kikamilifu tunapaswa kujua mwaka huu ni kiasi gani kimepatikana na katika kiasi hicho asilimia ya Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ni ipi kuliko utaratibu wa sasa ambao unafanya tunaletewa mahesabu ambayo hatuyafahamu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na asilimia 25 bado ninaiomba Wizara ya Maliasili iongeze kutoka asilimia 25 kwenda asilimia 35. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee sasa kuhusu barabara ya Utete – Liwale. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, nilimuona Mheshimiwa Susan Kiwanga. Mheshimiwa Faith ukae chini kwanza.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako, Kanuni ya 68(7) naona mchangiaji ambaye alikuwa anachangia sasa anasoma mwanzo mwisho. Naomba Mwongozo wako. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa mchangiaji kama ulikuwa unafanya hivyo basi uendelee kwa utaratibu wa Kikanuni malizia Mheshimiwa Faith. Lakini asubuhi tulivumiliana sasa hivi tena tunageukana. (*Makofi*)

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba niongelee barabara ya Utete - Liwale ambayo inakatisha katika Mbuga ya Selous. Mwezi wa nne nilipokuwa nimeuliza swali kuhusu ujenzi wa barabara hii nilijibiwa kwamba wadau ambao ni Wizara ya Maliasili na wadau wengine wanatakiwa wakae na waangalie mchakato mzima wa ujenzi wa barabara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafikiri barabara hii ya Utete – Liwale siyo barabara ya kwanza kukatisha katikati ya Hifadhi. Ngorongoro kuna barabara, Serengeti mmesema asubuhi imezungumzwa si haba kwamba imeshakubaliwa. Hifadhi ya Mikumi barabara imepita pale mimi sioni ni kwa nini barabara kutoka Utete kwenda Liwale ambayo inapitia *Selous Game Reserve* ichukue muda mrefu kufanyiwa mchakato na *logistics* wakati barabara hii inakuja kusaidia Wizara hii ya Utalii licha kwamba inakuja kusaidia pia wasafiri wanaotoka Dar es Salaam kwenda Liwale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Napenda ni-*declare interest* kwamba mimi ni mwenyeji, mzaliwa kabisa wa eneo hili la Ngorongoro na nimefanya kazi Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro miaka saba katika Idara ya Utalii na katika Idara ya *Community Development*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu niwape Waheshimiwa Wabunge picha kidogo kuhusu Ngorongoro. Ngorongoro ni eneo lenye kilomita za mraba 8,300; ni eneo ambalo shughuli za binadamu zinaendelea pamoja na uhifadhi wa wanyama na ufugaji wa mifugo zaidi. Eneo hili

ni urithi wa ulimwengu, *UNESCO* ilitangaza eneo hili kuwa ni urithi wa ulimwengu miaka 1978/1979. *Ngorongoro Crater* ni eneo ambalo ni muhimu sana ulimwenguni ndio maana wageni wengi wanafika kuangalia hii *Crater* ni tofauti na *Crater* zingine duniani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, ina majukumu makuu matatu uhifadhi, utalii na kuendeleza wenyeji wa eneo lile. Wenyeji wale wametolewa kutoka Serengeti na kupewa *Ngorongoro Highlands* na wakoloni na kuambiwa kwamba hakuna tena mtu atakayewagusa hapa ni maskani yenu, kaeni kwa amani milele yote. Sasa ninaona kama mwakilishi wa wananchi hili suala la kuendeleza wenyeji ni jukumu la kisheria. (*Makof*)

Lakini inaonekana kama suala hili ni la hisani, jambo ambalo si kweli. Wenyeji wa pale sasa hivi tunasomesha vijana zaidi ya 300 wamemaliza Vyuo Vikuu wengine wamemaliza Vyuo vya Kati lakini hawapati ajira kabisa. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro hivi karibuni iliajiri askari *game* karibu 25 hata mmoja hakuna aliyajiriwa ambaye ni mwenyeji pale. (*Makof*)

Mimi nashangaa kwa sababu gani hawa wenyeji wa Ngorongoro hawafikiriwi wakati ni watu ambaao ni waaminifu, ni watu ambaao ni jasiri, ni watu ambaao ni wa hifadhi ya asili. Ninyi wote ni mashahidi, ndugu zangu wamekwenda kwenye miji mbalimbali wanafanyakazi ya ulinzi wanalinda katika taasisi, katika makampuni na hata nyumba za watu binafsi. Lakini shirika kubwa kama lile tume-*train* mgambo zaidi ya 100 juzi wali-*apply*, walijaribu kuomba kazi na hawa wamemaliza wengine *form four* lakini hakuna anayewaona katika suala zima la ajira. Halafu Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa awamu nytingine tena iliajiri watu karibu 50 katika fani za uhasibu, utalii na askari *game*. Aliajiriwa kijana mmoja tu kutoka Kata ya Kakesyo ambaye huyu alimaliza *form four* na alimaliza Chuo cha Wanyamaporl kule Pasiansi. Ni mmoja tu katika watu 50 walioajiriwa. (*Makof*)

Sasa watu wanapolalamika, kulalamikia ajira ni jambo la msingi sana na wanawekewa masharti magumu, wawe wamemaliza *form four* au wamepita JKT, wamepita Magereza, wamepita Jeshi la Wananchi lakini hawasemi aliyepita mgambo kwa kiwango cha watu wa pale. Sasa mgambo ni chombo pia ambacho kinatambuliwa na Serikali ya nchi hii. Mkiwaajiri katika hali hiyo muwapeleke *training* watakuwa wazuri tu kama wengine wote walipita katika vyombo hivyo vya Jeshi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uhifadhi ni jambo kubwa sana katika Ngorongoro, mambu yote yanayofanywa pale kama uhifadhi hauzingatiwi kwa kweli hakuna tunachokifanya pale, wala eneo la Ngorongoro halitakuwa maarufu kwa sababu yoyote ile. *Ngorongoro Crater* ni eneo ambalo ni muhimu sana. Lakini eneo hili ndugu zangu walikuwa wanaishi zamani huko *Crater Floor* lakini mwaka 1975 wakatolewa na Jeshi wakasema eneo hili ni dogo sasa wanyamaporl na mifugo eneo ni dogo kwa hiyo, wakaondolewa. Lakini wakati ule faru walikuwa wengi sana pale na leo wako lakini ni wachache siyo kama wakati ule. Pale *Crater* kuna askari karibu 40 ambaao wanapeana zamu kulinda eneo lile. (*Makof*)

Lakini hawa askari mishahara yao inachelewa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inapata hela ya kutosha, *morale* ya askari inakuwa chini. Niwaambie wanaolinda wale faru kwa kweli ni wenyeji wa Hifadhi ya Ngorongoro ambaao ni wa jamii ya Kimasai na hao ndio hamtaki hata kuwaajiri ni walinzi wazuri. Mimi nawaomba hawa watu muwafikirie, muwape ajira ili waweze kufanya hizi kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi faru mmoja alitoka ndani ya *Crater* kupita Layanahi kwenda *Olmoti Crater* kuteremkia Olbalbal kupita Oldpai kwenda mpaka Serengeti. Lakini alipoteremkia maeneo ya wenyeji, wenyewe wakamzingira wakamrudisha *Crater*, ni wahifadhi wazuri. Sasa kwa nini msiwaangalie watu hawa katika suala zima la ajira? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo taarifa kuwa kuna mafuvu karibu matatu yaliokotwa ndani ya *Crater* na kwamba hata ndani ya *Crater* kuna ujangili, sasa yaliokotwa mafuvu matatu ya faru na askari ambaao wanalinda *Crater*, mafuvu yale ya faru ilitolewa taarifa kwa Menejimenti na ilitolewa taarifa kwa Bodi kupitia kwa *Technical Advisor* wa Mradi wa Faru ambaye anafanya kazi na *Frankfurt Zoological Society* lakini tangu wakati huo hakuna *action* yoyote iliyochukuliwa wala

hakuna *investigation* yoyote ambayo inaendelea. Sasa jambo hili kama limefika kwenye bodi, bodi kazi yake ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa hoteli katika *Rim ya Crater* sasa hivi kuna hoteli nne na *General Management Plan* ya Ngorongoro imeshazuia ujenzi wa hoteli zaidi katika *Rim ya Crater*. Lakini hivi karibuni kimetolewa kibali kujenga hoteli kwenye *Rim ya Crater* ndani ya *Crater* ya Ngorongoro. Kujenga hoteli ya nyota tano katika eneo ambalo ni *corridor* kabisa ya faru. Eneo lile ni mapato kabisa ya faru. Sasa tumepigia kelele wanaongoza katika kutoa maeneo hayo ni Mwenyekiti wa Bodii ya Ngorongoro Mheshimiwa Pius Msekwa. Jambo hili kwa kweli linasikitisha na hatutakubali kabisa hoteli ile kujengwa pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama yeze ana nguvu zaidi kuliko sisi wenyeji basi atuonyeshe nguvu yake iko wapi. Kwanza jambo hili aangalie tunaheshimu sana Chama cha Mapinduzi ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na maombi yanavyokuja ya kujenga hoteli wanasema Rais amesema, Rais gani anasema tujenge hoteli *Crater* aende kinyume na taratibu zilizowekwa na wahifadhi na watalaan wa hifadhi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Rais Kikwete hawezikukubali hoteli zijengwe katika *corridor* ya wanyama na hasa faru, mnyama ambaye anaelekea kutoweka. Hatutakubaliana na jambo hilo na huyu mtu kama watu wamekula hela zake aonyeshwe kwingine ndyo utaratibu uliopo na aonyeshwe kule *Oltariani Gorge*, aonyeshwe maeneo ya *Nasera Rock* aonyeshwe maeneo ya Kakesho. Aonyeshwe maeneo ya *Lake Eyasi*, lakini siyo tena katika *Rim ya Crater*. Hilo suala hatutakubaliana. (*Makofi*)

Sisi tulitaka kujenga sekondari ya Nainokanoka pale, tukaambiya kwamba hapana msijenge hapa. Mifugo yetu ilitaka kupita hapa kula chumvi huko *Crater*, tunakatazwa, kwa nini *Five Star Hotel* inajengwa pale? Hilo suala hatutakubaliana hata kidogo. Tatizo ni kwamba wawekezaji hawa wanakwenda wenye kuchagua maeneo ya kuweka hoteli. Wanaonyeshwa maeneo ya kuweka hoteli. Watalaan wako wapi wa hifadhi? Bruno Kawasange yupo hapa ni Mhifadhi aliyebobe, lakini hana nafasi, hasikilizwi. *Ecologist*, Dkt. Victor Runyoro, ni Mhifadhi mzuri, hakuna anayemsikiliza. Sasa atasikilizwa nani? Tukianza kusikilizwa sisi wanasiwa uhifadhi utakufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii. Hii habari ya kwenda kutangaza Ngorongoro huko nje na maeneo mengine, sina ugomvi nao, lakini jamani nendeni kwa staha. Mnakwenda kikosi kizima, kwa nini? Mimi nampongeza sana Mheshimiwa Maige alipozua hii, watu zaidi ya 12 walitaka kwenda huko. Wanakwapua dola zaidi ya 71,000. Ni pesa nyingi sana ni karibu shilingi milioni 120, ingeweza kutusaidia sisi kupata tani za mahindi katika eneo la Ngorongoro ambalo kuna njaa. Ni aibu sana a *World Heritage Site*, una *International Bio Spere Reserve* kusikia kwamba kuna njaa huko wakati mapesa wanayo. Hakuna mtu anayeamini kwamba Ngorongoro haina pesa ya kununua chakula. Ni aibu sana. Hata hao wa nje walitangaza kwamba eneo lile ni urithi wa ulimwengu hawafurahi kusikia kwamba Ngorongoro tuna njaa mpaka ndugu zangu wanaandamana kwenda kwenye vyombo vya habari, ni kitu gani hakuna mtu anayewasikiliza. Mhifadhi wa Ngorongoro yupo hapa hakai ofisini amekuwa mtoro wa ofisi, haendi vijiji. Hajui matatizo, hajui maeneo. Halafu amestaafu tangu mwaka jana, anaongezewa mwaka zaidi kwa kazi gani na ya kazi gani. (*Makofi*)

Hii kwanza ni kuvunja Katiba, watu wanastaafu katika utaratibu uliowekwa na kwa mujibu wa kanuni, unamwongeza mtu hana uwezo wa utawala, ndyo maana kila jambo anajifanya anavyotaka hapa. Hatutakubaliana na wewe, Mwenyekiti Mheshimiwa Lembeli uliwahi kumwambia Mwenyekiti Msekwa kwenye kikao cha Kamati kwamba Ngorongoro itakufia mikononi na kweli itamfia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutakubaliana, Ngorongoro siyo ya Msekwa, siyo ya nani ni ya kwetu wote. Kwanza namwomba Mheshimiwa Rais ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, lakini Wenyevitii wenzake wote wako huku, yeze anakwenda kuwatafutia wale maeneo ya kujenga hoteli yupo anangaika, ni mbaya zaidi. Yes Mwenyekiti wa *TANAPA* yupo

hana, ye ye hayumo humu, labda alijua kwamba tutazungumza huku. Lakini kule aliko anatusikia. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namwomba Mheshimiwa Waziri kama ana uwezo Mheshimiwa Waziri Maige kama una uwezo vunjilia mbali hii Bodi. Vunjilia mbali na wakati huo huo uunde Tume ya kuchunguza uendeshaji wa Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro, mahesabu yake, mambo ya ajira, mambo ya ajabu sana yanafanyika pale. Kama hutafanya hivyo Bunge Ijalo mimi nakuja na hoja binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siungi mkono mpaka nitakapopata maelezo kuhusu haya niliyosema. Lakini Mheshimiwa Maige kaza buti, umetingisha, wametingishika, endelea mbele. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Huyo ni Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, wasiomfahamu huyo ni Kamanda wa Jeshi. Mheshimiwa Juma Nkumba atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kebwe Kebwe.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini kabla sijaendelea naomba nichukue fursa hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanazozifanya. Mimi nina mambo machache sana. (*Makofi*)

La kwanza naomba kwa namna ya pekee nimshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Mbobe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, lakini vilevile Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA leo kwa kukubali kwa dhati siasa ambazo kwa kweli zimekuwa zikizungumzwa sana na uongozi wa Chama cha Mapinduzi kwa kukubali sera za uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yake yanathibitisha kabisa kwamba si kila uwekezaji ni wizi. Uwekezaji ni sera za Chama cha Mapinduzi na mara nydingi hapa tumekuwa tukisikia kwamba wawekezaji wa madini, kumbe wanaokuja kwenye uwekezaji wa utalii wanaweza wakaisaidia nchi. Kwa hiyo, napenda nichukue fursa hii kwa kweli kumshukuru sana Mheshimiwa Mbobe kwa kudhihirisha kabisa kwamba sera za CCM ni sera sahihi, ni sera mahiri ambazo zinaweza zikasaidia kufufua uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nianze kwanza la ushauri. Mimi sisomi, mimi naangalia. Asali inawasaidia wananchi wengi sana kule vijijini na kwetu sisi maeneo ya Sikonge huko, ukienda Mpanda huko maeneo mbalimbali unakuta asali inawasaidia na kuongeza kipato cha wananchi lakini vilevile kipato cha Taifa. Nilikuwa naiomba sana Wizara, imeweka utaratibu kwa sababu asali nydingine zipo zinazofugwa, nyuki wanaofugwa majumbani, lakini wapo nyuki amba kwa kweli lazima uwaafuate katika hifadhi. Utaratibu wa Serikali kwa maana Wizara hii kwa kufungua misitu tarehe 1 Julai kwa watu wote amba wana shughuli ndani ya misitu wakiwemo na warina asali. Unapoteza mapato mengi sana kwa warina asali wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 1 Julai katika maeneo mengine unakuta nyuki wamekwisha kunywa ile asali kwa sababu huwezi ukalinganisha mazingira ya Arusha, ukalinganisha mazingira ya Mwanza, mazingira ya Tabora na mazingira ya Ruvuma. Mazingira yako tofauti na mvua zipo katika misimu tofauti. Nilikuwa naiomba sana Serikali, mimi kila mwaka naenda kupiga hodi kwenye Idara ya Maliasili aidha ya Wilaya au ya Mkoa kuwaomba baadhi ya wafugaji wa nyuki wapate kibali cha kwenda msituni. Hatuwezi tukafanya hivi vipindi vyote. Nilikuwa naiomba Serikali ione, mnahofu nini na warinaji wa asali, mtu anakwenda kule kurina asali, majangili wanajulikana. Tuwaruhusu warina asali waende wakajipatie huduma hii. (*Makofi*)

Sasa liliilonileta leo kubwa ni la *WMA* ya Ipole. Mwaka 2004 zilisajiliwa *WMA* nne, moja ni ya Uyumbu ipo Urambo, nydingine ya Burunge ipo Arusha. Nydingine ipo Ngarambe Rufiji na ya Ipole Sikonge. Taratibu zote za uanzishwaji *WMA* hizi zilizingatiwa ikiwemo ile ya Ipole. Serikali ilitoa muda wa miezi karibu 44 ili kuona kwamba kama mtu anaona *WMA* hii isianzishwe basi atoe malalamiko yake Serikalini, miezi 44 ilipita hakuna aliyejitokeza kwamba *WMA* ile ya Ipole imeanzishwa isivyo halali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya ushirikishwaji umma kulinda hifadhi ni sera ya msingi. Kwa sababu ninyi hapa Wizara hii askari milionao ni wachache, hawawezi wakaenea katika hifadhi zote. Lazima wananchi washiriki katika kuhakikisha kwamba mali zetu za asili zinalindwa. Sasa mimi nashangaa sana na Mheshimiwa Waziri nimeshakuja ofisini kwako. Idara ya Misitu imeamua kupingana na sera hii halali, Serikali hiyo hiyo moja. Nauliza leo kuna Serikali ngapi? Ipo Serikali moja na kiongozi wake Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri mmoja, Waziri wa Maliasili na Utalii, Maige. (*Makofii*)

Sasa huko kama kuna watu wanacheza cheza halafu Mheshimiwa Maige unawaangalia tu, wanakuharibia kazi. Hatuwezi kuwa na utaratibu kama wa kambale kila mmoja ana sharubu kwa hiyo huwezi kujua mkubwa nani. Nataka leo hii Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unaweka mambo yako sawa sawa unipe maelezo hii *WMA* unaifahamu? Unaitambua ama huitambui? Unawaacha watu wanachezea huko wananchi, watu wanajitolea wanafanya kazi ya kulinda maliasili zetu, wanakwenda watu wako wadogo kule wanawavuruga wananchi, hatuwezi kukubali jambo la namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sumaye alipokuwa Waziri Mkuu hapa nilisema, msituchezee sisi, misitu ile sisi tunaifahamu vizuri, ninyi mnachezacheza hapa. Tunaweza mkaamka hapa siku moja msitu ule haupo mtaendelea kulinda linda wapi sasa uwezo huo tunao. Tunawalindia msitu wenu, tunauchunga msitu wenu, halafu bado mnaendelea kutunyanyasa, jambo hili haliwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Juhiwai ile ya Ipole imepata ufadhili. Tuna ujenzi wa *village game scout* hapa tumepata ufadhili kutoka *USA* kwenye *village game scout* tumepata shilingi shilingi 247,377,693. Kwenye ujenzi wa kituo cha habari Ipole na sehemu ya kutunzia asali tumefadhiliwa shilingi 235,80,026. Tuna ujenzi wa miundombinu kuleta maji Ipole na Udongo tumefadhiliwa shilingi 88,181,565, lakini vilevile ili kuweka mipaka sahihi kwenye eneo letu la *WMA* wawekezaji hawa wametusaidia kuweka *beacons* katika mipaka ya Ipole kwa kiasi cha shilingi 96,883,900/=. Tumeweka *beacons* hizi. Lakini Idara ya Misitu imeanza kusumbua wananchi wa eneo lile na bahati mbaya sana mimi nilipoanza kupata matatizo haya nimekuja ofisini kwako Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri imekwenda kule, Tume imeshirikiana na uongozi wa Mkoa na Wilaya wamekwenda kule wamezungumza wakasema matatizo haya ya ishe. Lakini mtumishi wako mmoja anaitwa Create sijui ya nini, amekwenda kule ameng'oa *beacons* nilizoisema kwa gharama hii ambayo niliyoisema hapa zaidi ya shilingi milioni 88, ameng'oa *beacons* zote. Nani anampa jeuri ya namna hii? Nani anampa mamlaka haya? Wizara ipo, Serikali ipo, huyu bwana haheshimu hata Mkuu wangu wa Wilaya. Haheshimu Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, yeye nani? Hatuwezi kukubali. Bwana Mheshimiwa Waziri hatuwezi kukaa na mtumishi wa namna hii anayevuruga watu kwenye Wilaya yetu. (*Makofii*)

Mimi Mbunge sasa awamu ya tatu hii, siwezi kuchezewa chezewa na mtu anakuja anavuruga wananchi pale. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri utoe maelekezo yatakayosaidia kurudisha imani ya wananchi wa Ipole na imani ya wananchi wa Sikonge juu ya Serikali yao na mimi nitafuatilia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri hapa tumesikia hapa habari za wanyama walioibiwa wamepelekwa nje. Hili langu la mwisho hili. Hivi nchi kama hii jamani na vyombo vyote hivi mambo ya namna hii yanafanyakaje? Hailezeki, ni aibu kwanza, ni aibu kwa Taifa letu. Niombe sana Mheshimiwa Waziri naona umeanza kufanya kazi vizuri, maana vijana wanapoanza kuchapa kazi vizuri lazima tuwasifie, unafanya kazi nzuri. Lakini tunataka wanyama wetu hawa warudi. Tulidai fuvu la Marehemu Mzee Mkwawa, likarudi. Tunataka wanyama wawe hai wasiwe hai warudi. Kama hawako hai mafuvu yao tunahitaji hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya nashukuru sana. Ahsante sana na Mungu awabariki sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Juma Nkumba kwa mchango wako. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, dakika zilizobaki hazitoshi sana kuendelea ili tuwatendee haki wachangiaji wanaofuata, itabidi tuendelee tena kesho asubuhi. Kwa hiyo, kesho asubuhi mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mendrad Kigola ataendelea na wengine watafuatia kadri ya utaratibu utakavyokuwa. Nimekuona Mheshimiwa Felix. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka tu kama kuondoa sijui ni unafiki kwa sababu wakati Mbunge wa Ngorongoro anachangia kuna taarifa kwamba na yeze alikuwa ni Mjumbe wa Bodi hii ya Ngorongoro na ameshashiriki ziara mbalimbali. Sasa tungependa kujua haku-*declare interest* na amezungumza mambo mengi na ametaja watu ikiwemo kuvunja hii Bodi. Alikuwa Mjumbe lakini hakusema hilo. Naomba Mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro kama alivyoeleza yeze ni mhifadhi, alishaajiriwa katika Mamlaka hiyo ameelleza na miaka ambayo amefanya kazi. Alishawahwi kuwa Mjumbe wa hiyo Bodi enzi hizo. Sasa hivi si Mjumbe wa hiyo Bodi. Lakini katoa mawazo yake hayana mgongano wowote na jambo lolote lile. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, muwe wazi, muwe huru tu kusema ambayo mnataka kuchangia kwa ajili ya kujenga nchi yetu. (*Makofi*)

Mwisho tangazo, Kaimu Katibu wa Bunge anaomba nikutangazieni Waheshimiwa Wabunge kwamba Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (*LAPF*) umeweka dawati la maelezo (*information desk*) katika viwanja vya Bunge kuanzia leo tarehe 17 Agosti mpaka siku ya mwisho tarehe 26 Agosti.

Kwa hiyo, mnaombwa kufika kwa maelezo ya kijiunga na Mfuko huo kwa wale ambao wanatarajia kufanya hivyo. *LAPF* wana dawati lao kuanzia leo mpaka tarehe 26 kwa Waheshimiwa ambao wangependa kijiunga au kupata maelezo ya *package* walio nayo wako pale Jengo la Utawala.

Baada ya maelezo hayo kwa kuwa sasa kazi zilizopangwa katika utaratibu wetu wa kazi za Kibunge na niwaambie wananchi hapa kwamba katika vyombo ambavyo vinafanya kazi kwa sayansi na teknolojia ya hali ya juu kimojawapo ni Bunge. (*Makofi*)

Shuhuda au shahidi wa jambo hilo ni kwamba kazi zilizopangwa kwa siku ya leo na tarehe ya leo zimekamilika kama ziliviyopangwa kwa mahali pake. Kwa hiyo, Taasisi zetu zote Idara za Serikali nazo zingefanya hivi nadhani tungefika mbali sana, waige mfano wa Bunge. Lakini pia na kwa uendeshaji mzuri wa Naibu Spika. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi. (*Makofi/Kicheko*)

*(Saa 12.20 jioni Bunge lilahirishwa hadi siku ya Alhamisi,
Tarehe 18 Agosti, 2011 saa tatu asubuhi)*